

# Kama Uhukumuvyo

ADRIAN EBENS

Katika kumbukumbu pendwa ya Carolyn Hullquist, Dada mpendwa katika Kristo ambaye alilala mauti Julai 4, 2019

fatheroflove.info

Julai 4, 2020

Mafungu yote ya Biblia yaliyonakiliwa yametoka kwenye toleo la New King James Isipokuwa pale tu ambapo imetajwa vinginevyo.

# YALIYOMO

**Sura Ya 1**
Ni Bora ujihadhari ........ 5

**Sura Ya 2**
Siku ya Hukumu ........ 12

**Sura Ya 3**
Haki na Hukumu ........ 19

**Sura Ya 4**
Chimbuko la Hukumu ya Adhabu ........ 25

**Sura Ya 5**
Mtazamo, Uelekezaji, na Uhalisia ........ 32

**Sura Ya 6**
Kwa ajili Yako Ardhi Imelaaniwa ........ 36

**Sura Ya 7**
Tazama Mtu Huyu ........ 40

**Sura Ya 8**
Kumhukumu Baba ........ 43

**Sura Ya 9**
Ufunuo wa Baba ........ 48

**Sura Ya 10**
Wala Sikuhukumu ........ 55

**Sura Ya 11**
Sheria ni ya Rohoni ........ 61

**Sura Ya 12**
Imeandikwa kwenye vibao vya Moyo ........ 65

**Sura Ya 13**
Mawazo Yangu Si Mawazo Yenu ........ 72

**Sura Ya 14**
Njia yako Ee Mungu i katika Patakatifu ....................77

**Sura Ya 15**
Vitabu Vikafunguliwa na Hukumu ikawekwa ....................85

**Sura Ya 16**
Umeuacha Upendo Wako wa Kwanza ....................97

**Sura Ya 17**
Mto Unaong'aa au Mwali wa Moto? ....................106

**Sura Ya 18**
Lugha ya Majeshi Maovu ....................112

**Sura Ya 19**
Muktadha wa Hukumu kabla ya Marejeo ....................118

**Sura Ya 20**
Wakati wa Taabu ya Yakobo ....................128

**Sura Ya 21**
Hukumu ilikuja kwa kosa la mtu mmoja ....................136

**Sura Ya 22**
Kiti cha Hukumu cha Kristo ....................143

**Sura Ya 23**
Utakaso wa Hekalu na Siku ya Upatanisho ....................151

**Sura Ya 24**
Bila ya Mwombezi ....................164

**Sura Ya 25**
Chronos na Kufungwa kwa Rehema ....................170

**Sura Ya 26**
Kutakasa na Kukamilisha Hekalu la Kiroho ....................181

SURA YA 1

# Ni Bora ujihadhari

Matarajio ya furaha ya mamilioni ya watoto ulimwenguni kote usiku wa Desemba 24 hayawezi kupimika kwa hakika. Miti ya Krismasi inayometameta husimama kwa fahari kwenye pembe za njia na ishara kubwa za *"Karibu Santa"* humkaribisha mtu huyu wa ajabu kutoka Ncha ya Kaskazini kuja na kuwabariki kwa zawadi.

Watoto hawa wote wasio na hatia wanapitia uzoefu ulio sawa na ule wa Mtume Yohana katika kitabu cha Ufunuo. Furaha isiyo na hatia ya Krismasi katika utoto ni tamu kinywani, lakini utambuzi wa kwamba Santa ni udanganyifu mtupu ni uchungu tumboni kwa wengi.

Desturi ya Krismasi hufunua mengi kuhusu ubinadamu. Kwa nini wazazi hutafuta kuwasadikisha watoto wao kuhusu jambo lisilo la kweli? Kwa ufupi, kwa nini wazazi huwadanganya watoto wao ilhali wanajua kwamba hatimaye watoto wao lazima wapitie hali yenye kukatisha tamaa ambayo ilibuniwa tu?

Uzoefu wa Krismasi huko Australia ni wa kushangaza zaidi. Desemba huko Australia ni katikati ya msimu wa joto, kwa hivyo taswira ya kulungu, theluji na Santa mkubwa mwekundu aliyevalia vyema ni ya ajabu sana. Mara nyingi siku ya Krismasi inaweza kufikia viwango vya joto vya nyuzijoto 35 au zaidi, jambo ambalo linapaswa kuyeyusha matarajio ya mashabiki wa Santa, lakini

hapana! Kitu hiki huendelea na hitilafu zake zote, mambo yasiyo ya kawaida na bila shaka zawadi za furaha na vyakula vitamu vya kupendeza kula.

Santa hujumuisha mambo mengi kuhusu saikolojia ya binadamu ambayo yanastahili kutafakariwa. Kando na likizo inayowakilisha matarajio ya kibiashara na nyenzo ya wauzaji na watumiaji, mashairi ya wimbo maarufu wa Santa huzungumzia mitazamo ya wanadamu ya jinsi maisha yanavyoeleweka.

**Santa Claus Anakuja Mjini**

Ni bora ujihadhari
Ni bora usilie
Ni bora usinung'uke
Ninakuambia kwa sababu
Santa Claus anakuja mjini

Anachukua orodha
Anaiangalia mara mbili mbili
Atagundua ni nani aliye mbaya au mwema
Santa Claus anakuja mjini

Anakuona unapokuwa umelala
Na anafamu unapoamka
kama umekuwa mwema au mwovu
Hivyo uwe mwema kwa ajili ya mema

Mtoa zawadi ana kitu cha ncha kali katika mkia wake. Kwa hakika anachukua orodha ya mambo yote unayofanya. Inavyoonekana, ana zawadi ya kuwepo kila mahali na anaweza kukuona unapolala na ukiwa macho. Anaangalia orodha angalau mara mbili ili kujua kama umekuwa mtukutu au mwema.

Tangu miaka yetu ya awali tunafundishwa kwamba tunatazamwa kwa uangalifu na kwamba kila kitu tunachofanya kinarekodiwa katika Ncha ya Kaskazini. Muktadha wote ni wa hofu kwa sababu *bora ujihadhari!* Unatazamwa na kuna hatari kwamba hautapokea zawadi nzuri ikiwa umekuwa mtukutu. Katika matoleo mengine unapokea zawadi mbaya, kama vile makaa ya mawe au mbaya zaidi.

Kitendawili cha asili katika Santa Claus kinaonekana kufichwa kwa wengi. Mzee huyu mcheshi anayebeba zawadi na vinyago anaendesha operesheni ya uchunguzi wa kimataifa na anatumia vipawa vyake kwa njia ya kuleta mabadiliko katika tabia yako ili kukufanya kuwa mtu bora; raia bora wa serikali.

Kitendawili katika Santa Claus huenda kilihusiana na kitendawili sawa na kilichoonwa ndani ya Ukristo na bwana Kames, mwanasheria wa Uskoti, mwanahistoria na mwanafalsafa katika karne ya 18.

> "Dini ya Kikristo," aliandika, "ni mashuhuri kwa ajili ya roho ya upole, ustahimilivu, na upendo wa kindugu; na bado mateso yake hayajawahi kufikiwa kwa jinsi yalivyokuwa ya kutisha na dini nyingine yoyote." Kames aliuta mgongano huo kati ya kanuni ya Kikristo na matendo "jambo la pekee katika historia ya mwanadamu."[1]

Bila shaka, Kames hakuwa mtu wa kwanza au wa mwisho kuona kitendawili hiki. Je, ni kwa jinsi gani dini ya Yesu inayofundisha upendo, rehema, na huruma kwa wote inaweza kuzalisha katika wengi wa wafuasi Wake wanaodaiwa kuwa na tabia kama hiyo ya udhibiti na nguvu?

Tukichimba zaidi katika historia ya Kikristo tunagundua katika kielelezo cha juu cha hoja za Augustine ili kuhalalisha kanuni ya matumizi ya nguvu.

> Pale Augustine (mwanatheolojia wa kwanza Mkristo kusitawisha utetezi wa utaratibu wa mateso) alipoambiwa na wapinzani wake kutaja hata tukio moja ambapo Yesu alitumia nguvu ya kulazimisha badala ya kushawishi, alichomoa bwana ya jembe (usemi utokao katika mchezo wa karata) kutoka kwenye mkono wake. Hili lilikuwa ni kisa maarufu (Matendo 9:1-18) cha safari ya Paulo kwenye barabara ya kwenda Dameski. Alipokuwa njiani kwenda kuwatesa Wakristo, Paulo (wakati huo akiitwa Sauli) alianguka chini aliposikia sauti ya Yesu na kupofushwa na nuru angavu.

[1] https://www.libertarianism.org/publications/essays/excursions/notes-persecution-toleration-history-christianity

> Kugeuzwa huko kwa Paulo, kulingana na Augustine, kwa wazi kulihusisha kulazimishwa, kwa kuwa Kristo "alitumia uwezo wake kumwangusha Paulo chini" na pia "akampiga kwa upofu wa kimwili" (ulemavu uliochukua siku tatu). Hivyo ndivyo Paulo alivyokuja "kwenye injili chini ya kulazimishwa kwa adhabu ya kimwili," na hivyo ndivyo hoja ya kwamba Kristo hakuwahi kutumia nguvu ya kimwili ilivyokanushwa kwa uthabiti—angalau katika akili za Augustino na Wakristo wengi wa baadaye ambao walirudia hoja yake.[2]

Ufafanuzi wa Augustine wa kisa hiki ni wa kustaajabisha kwa kuzingatia maneno ya Yesu kwamba "tusishindwe na uovu," kumaanisha kwamba halijawekwa mikononi mwetu kuwalazimisha wengine kuwa wema.[3]

Bila kujali, Augustine alisitawisha kutokana na nadharia hii ya "vita vya haki" kuwa msingi wa kulinda amani na kuadhibu uovu.[4] Ili kulinda amani, sheria na utulivu, raia wa taifa lolote linalofanya kazi chini ya kanuni hizi hutakiwa kutumia nguvu na adhabu pale manufaa ya wote yanapokiukwa. "…kuna mateso ya haki, ambayo Kanisa la Kristo huwaletea waovu." (Augustine, Letter to Boniface)[5]

Je, ni matunda gani ya kihistoria ya wazo la Augustino la mateso ya haki? Ilikuwa ni ukuzaji wa mawazo ya Augustino katika kanisa la zama za kati pamoja na mateso yake yote ya kidini, vita vya msalaba, na mauaji ya mamilioni ya waliodhaniwa kuwa wazushi. Haukuwa upendo wa Kristo uliowabidisha Wakristo hao, bali tishio la hukumu na kifo. Mifumo yetu ya kiserikali imebadilika, lakini ni kiasi gani cha theolojia na sera yetu ya msingi imebadilika?

Kihistoria katika Ukristo, wanadamu wametaja mara chache juu ya kuzimu (hades na sheol ambapo kwa kawaida hutafsiriwa "kaburi") katika Biblia na kutokana na maneno hayo wameleta dhana za kufikirika za matukio ya

---

[2] Ibid
[3] http://maranathamedia.com/book/view/resist-not-evil
[4] https://en.wikipedia.org/wiki/Just_war_theory
[5] https://egregores.blogspot.com/2010/10/augustine-in-defense-of-torturing.html

kutisha ya mateso yatakayofanywa kwa maadui wa Mungu, ambao ni adui zetu, ambapo kwa kweli huu ni ulimwengu ambao tumeubuni unaoitwa "kuzimu."

Je, mambo yamebadilika leo? Hapana, tunaendelea kuvutiwa na hukumu na kifo, hata ikiwa mandhari ya fikira zetu imebadilika. Tunajua hili ni kweli kwa jinsi tunavyoelekea kufikiria kulipiza kisasi kwa adui zetu. Ni mojawapo ya mistari ya njama ya kizamani ambayo hurudiwa mara kwa mara katika riwaya na filamu, na kwa kawaida huonyeshwa kwa ukali na umwagaji damu iwezekanavyo.

Mtume Paulo anawasilisha kwetu mvuto wa ndani kabisa wa kwanini tunapaswa kutamani kumfuata Kristo badala ya ushurutishwaji wa nje uliotetewa na Augustine.

> Maana, upendo wa Kristo watubidisha; maana tumehukumu hivi, ya kwamba mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi walikufa wote; — 2 Wakorintho 5:14

Fundisho la Kristo linatufundisha kwamba upendo wa ajabu wa agape wa Mungu uliofunuliwa katika Kristo unakuwa msingi wa mvuto wa ndani wa kupenda wote wanaomzunguka. Uzoefu huu hauko ndani yetu kiasilia, kama Paulo anavyoeleza katika kitabu cha Wagalatia kuhusu mtoto ambaye yuko chini ya walezi.

> Ninachosema ni kwamba maadamu mrithi ana umri mdogo hana tofauti na mtumwa japokuwa anamiliki mali yote. Mrithi yuko chini ya walezi na wadhamini mpaka wakati uliowekwa na baba yake. — Wagalatia 4:1-2 ( NIV)

Nafsi ambayo haijaongoka inajihisi ni mtumwa ambaye anatawaliwa na sheria zilizowekwa na walinzi hadi anapofikia utu uzima. Badiliko linalotokea ni kwamba Roho wa Kristo huja ndani ya mwanadamu ili kumfunulia jinsi Baba alivyo hasa.

> Lakini ulipotimia wakati uliowekwa, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye amezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria, kusudi awakomboe wale waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate

> kupokea hali ya kuwa wana. Kwa kuwa ninyi mmekuwa wana wake, **Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, Roho ambaye alia, "Aba, Baba." Basi, wewe si mtumwa tena, bali mwana wa Mungu; na kwa kuwa wewe ni mtoto wake, Mungu amekufanya wewe pia kuwa mrithi**. — Wagalatia 4:4-7 (NIV)

Bila Roho wa Kristo kuja moyoni akilia "Abba Baba," nafsi inabaki katika hali ya kujisikia kama mtumwa anayetawaliwa na wengine. Kwa kutojiamini, mtu ambaye hajaongoka anahisi hitaji la kuwadhibiti wengine na hivyo anakuja kutawaliwa na wengine, kama lilivyo hili ndiyo jamii inayokua kutokana na watu wenye mtazamo huu. Moyo ambao haujaongoka husonga mbele bila kujua unaelekea katika aina ya serikali ya kiimla hata pale unapopinga dhidi yake. Bila mvuto wa ndani wa upendo wa Kristo, ufalme wa Mungu katika moyo usio na Roho yake bila shaka unatawaliwa na magavana na viongozi ambao lazima watoe adhabu kwa mtu ili kuziba pengo la ukosefu wa mvuto wa ndani unaochochewa na upendo.

> Kuanzia Augustine hadi Aquinas hadi Santa akija mjini, hitaji la orodha na woga wa adhabu kutawala jamii zetu limejikita ulimwenguni kote.

Hii ndiyo sababu wafafanuzi wengi wanaoonya kuhusu Agizo la Kiimla la Ulimwengu Mpya linalokuja na kukemea dhidi yake kwa kweli wanasaidia uundaji wa aina kama hizo za serikali. Utamaduni wa kuendelea kulizungumza na kuandaa huongeza ukosefu wa usalama na hali ya wasiwasi, na kuwafanya watu kuwa waangalifu kwa ajili ya mabadiliko hayo ya kiserikali.

Ulimwengu tunaoishi ni matokeo ya maamuzi ambayo wanadamu waliyachukua katika mwitikio wao dhidi ya upendo mpole na wa kujitolea wa Kristo. Miaka elfu mbili iliyopita sisi kama jamii tuliona kwa ufupi mtazamo wa Mungu ambao unaweza kubadilisha kabisa mitazamo yetu ya haki na misukumo yetu ya msingi ya maisha. Sarafu ilitupwa katika karne ya nne baada ya Kristo, wakati Ukristo ulipochukua mfumo wa kanisa la kifalme la ulimwengu wote lililounganishwa na serikali. Mfumo huu unataka mamlaka zaidi ya kudhibiti mawazo na imani za raia wake bila kujali aina ya serikali ambayo itajitokeza, kwa sababu hivi ndivyo mwanadamu anavyotaka kufanya akiwa na

mamlaka ili ajisikie salama. Matokeo yake, kupitia kuongezeka kwa maendeleo katika teknolojia na elimu na uhandisi wa kijamii, sasa tunaishi katika mazingira ya juu zaidi ya uchunguzi ambayo ulimwengu huu haujawahi kuyashuhudia.

Kuanzia Augustine hadi Aquinas hadi Santa akija mjini, hitaji la orodha na woga wa adhabu kutawala jamii zetu limejikita ulimwenguni kote. Katika kitabu hiki tunatoa mtazamo tofauti, lakini kwanza ni lazima tufuatilie maendeleo ya mitazamo ya hukumu ya kimungu. Ikiwa kuwabidisha watu kuwa wakristo kwa kutumia nguvu kutajikita katika akili zetu kama jambo ambacho Mungu alilitaka, hilo lingeathirije mitazamo yetu ya hukumu ya Mungu na kutia rangi usomaji wetu wa Maandiko?

SURA YA 2

# Siku ya Hukumu

Kuna kumbukumbu tofauti niliyo nayo ya kuzungumza na kundi la Wakristo huko Kaskazini Magharibi mwa Marekani. Walikaa wakiwa wamepigwa na butwaa nilipokuwa nikiwasilisha kwao upendo wa Mungu na rehema yake ya milele kwa njia ambayo hawakufikiria hapo awali. Baada ya maelezo yangu msichana mmoja aliniuliza, "Ukiondoa tishio la adhabu, ni nini kitakachosababisha mtenda dhambi kutubu? Je, huhitaji tishio la adhabu ili kumsaidia mwenye dhambi kuelewa kuwa amepotea?"

Nilihisi huzuni ndani niliposikiliza maneno ya Augustine yaliyokuwa yakirudiwa na kijana huyu mpendwa na mkweli. Walakini, hii ndiyo picha ambayo Ukristo umechora kwa zaidi ya miaka 1500. Mmoja wa wahubiri hodari katika karne ya 20, Billy Graham, analiweka wazi jinsi alivyolielewa.

> Biblia hutangaza kwamba Mungu ni Mungu wa hukumu, ghadhabu na hasira. Muda baada ya muda Yesu alionya kuhusu hukumu: "Kila neno lisilo maana watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu" (Mathayo 12:36).
>
> "Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi, na kuwatupa katika tanuru ya moto, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno." (Mathayo 13:41-42)

Mitume walifundisha katika Agano Jipya kwamba hukumu itakuja. Mtume Paulo alisema: "Ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemweka" (Matendo 17:31).

Mwandishi wa Kitabu cha Waebrania aliandika, "Imewekewa watu kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu" (Waebrania 9:27)

Wao "watatoa hesabu kwake yeye aliye tayari kuwahukumu walio hai na waliokufa," alisema Petro katika 1 Petro 4:5 .

Mtume Yohana alilielezea hivi: "Wafalme wa dunia, na wakuu, na matajiri, na makamanda, na wenye nguvu, na kila mtumwa, na kila mtu huru, wakajificha katika mapango na katika miamba ya milima; wakaiambia milima na miamba, Tuangukieni, mkatufiche mbali na uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na mbali na ghadhabu ya Mwana-Kondoo. Kwa maana siku iliyo kuu ya ghadhabu yake imekuja, na ni nani awezaye kusimama?'" (Ufunuo 6:15-17)

Mamia ya vifungu huelekeza kwenye wakati wa hukumu kwa kila mtu ambaye amewahi kuishi—hakuna atakayekweka. Kama ungeondoa rejea zote za hukumu kutoka katika Biblia, ungebakiwa na Biblia ndogo iliyosalia.

Mungu ametoa upendo wake na rehema na msamaha kwa wanadamu. Kutoka msalabani, Mungu ameuambia ulimwengu wote, "Nakupenda." Hata hivyo, upendo huo unapokataliwa kimakusudi, mbadala pekee ni hukumu.[6]

Ukisoma vifungu vya Biblia ambavyo Mchungaji Graham anavinukuu, inaonekana kuwa haiwezi kuepukika kwamba ghadhabu ya Mungu itawashukia wale ambao wamekuwa watukutu na, kama yule mtu mwekundu mwenye ucheshi katika Ncha ya Kaskazini, Mungu wa mbinguni anaweka rekodi ya kina ya shughuli zako ambazo Yeye atazitumia dhidi ya

[6] https://decisionmagazine.com/justice-of-god/

wale wote waliofanya makosa. Ikiwa hutakubali zawadi ya Mwanawe, basi atatumia nguvu kukomesha maisha yako kwa ajili ya uovu wako usiotii.

Haiwezekani kujitosa katika eneo ambalo nguvu haihitajiki kudumisha sheria na utulivu katika jamii. Hili linaonekana kuwa na mantiki, kama Mchungaji Graham anavyoelezea:

> Walakini, mungu wa aina hii angefanya ulimwengu wa kipumbavu. Utakuwa wa machafuko, kutowajibika, kujiangamiza. Haiwezekani kuishi kwa uhakika katika ulimwengu wa aina hiyo. Ili kuwa na maana, maisha lazima yategemezwe juu ya sheria na mtoa sheria.[7]

Unawezaje kuamuru jamii bila tishio la kutoa adhabu kwa kushindwa kutekeleza? Je, Mungu hakuwatisha Adamu na Hawa kwamba ikiwa wangekula matunda ya *mti wa ujuzi wa mema na mabaya* kwamba wangekufa? Vitabu vya Musa vimejaa maagizo ya adhabu ambazo zingetumika kwa watenda maovu katika taifa la Israeli. Inaonekana ni jambo la kimantiki kabisa kwa tishio la adhabu kutumika kwa wale wasiotii.

> Mitazamo yetu ya jinsi Mungu alivyo itaakisiwa katika namna tunavyoishi. Tunaiga namna ya Mungu tunayemuwazia.

Ni adhabu gani ambayo Ukristo huionyesha kwa kawaida inayowangoja wale wasiotii sheria? Katekisimu ya Kikatoliki inasema:

> Mara nyingi Yesu anazungumza juu ya "Gehena" juu ya "moto usiozimika" uliowekwa kwa ajili ya wale ambao hadi mwisho wa maisha yao wanakataa kuamini na kuongoka, ambapo nafsi na mwili vinaweza kupotea. Yesu anatangaza kwa uzito kwamba "atawatuma malaika zake, nao watawakusanya… watenda mabaya wote, na kuwatupa katika tanuru ya moto", na kwamba atatangaza hukumu: "Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele!" Mafundisho ya Kanisa yanathibitisha kuwepo kwa kuzimu na umilele wake. Mara tu baada ya kifo roho za wale wanaokufa katika hali ya dhambi ya mauti hushuka hadi

[7] Ibid

> kuzimu, ambapo hupata adhabu ya jehanamu, "moto wa milele". Adhabu kuu ya Jahannamu ni kutengwa na Mungu milele, ambaye katika yeye peke yake mwanadamu anaweza kumiliki uzima na furaha ambayo aliumbwa nayo na anayoitamani sana.[8]

Mateso ya milele katika moto wa kuzimu ni matumizi ya mwisho ya shurutisho la nje kuwalazimisha watu kunyenyekea chini ya sheria na utaratibu wa Mungu. Kwa asili yake tishio la mateso na adhabu kama hiyo linahitaji uangalizi, uchunguzi na hukumu ikiwa mtu anastahili uzima wa milele pamoja na Mungu mbinguni au hukumu ya milele katika jehanamu.

Watu wengi wanajua usemi huu "tumbili anachokiona, tumbili hukifanya." Mitazamo yetu ya jinsi Mungu alivyo itaakisiwa katika namna tunavyoishi. Tunaiga namna ya Mungu tunayemuwazia. Hata wale wanaokasirishwa na wazo la mungu ambaye angetesa watenda-dhambi milele wanaachwa wachukue nafasi ya ulimwengu wa kimungu na kuweka mwanadamu. Historia ya ubinadamu, iliyochafuliwa na mitazamo ya kidhalimu ya mungu, inadhihirisha mifumo ile ile ya udhalimu, kama inavyothibitishwa katika matukio kama mapinduzi ya Ufaransa, utakaso wa Stalin, Mapinduzi ya Kitamaduni ya Mao, uwanja wa mauaji wa Pol Pot na zingine.

Kuishi katika mazingira ya kitamaduni yaliyojaa mawazo ya ufuatiliaji, uchunguzi, na uamuzi, nilijifunza kuishi maisha ya siri. Ili kujiepusha macho yaonayo wakati wote ya wazazi, walimu, na mamlaka kwa ujumla, bila silika ningeficha mambo. Hofu ya adhabu kupitia ufuatiliaji ilipelekea katika kutafuta njia za kuepuka kutazamwa.

Hofu ya kugunduliwa inaonyeshwa leo kupitia uvujaji wa data kidijitali ambao unafichua siri za ndani tulizonazo. Hakuna aliye salama ambaye anajitosa kwenye mgawanyiko wa kidijitali. Kuna kejeli ya ajabu katika udukuzi na kufichua habari kutoka kwenye uchumba wa mtandaoni na huduma za kusindikiza ambazo hufichua siri zisizo za uaminifu za mamilioni ya watu.[9]

---

[8] https://en.wikipedia.org/wiki/Christian_views_on_Hell
[9] https://en.wikipedia.org/wiki/Ashley_Madison_data_breach

Wengi wetu tumefahamu kwamba programu za kubadili hotuba kwenda kwenye maandishi huendeshwa kwenye simu zetu na kunasa vifungu vya maneno muhimu ambavyo hujitokeza ghafla katika utangazaji wa wavuti au maudhui ya YouTube yanayohusiana na kile ambacho tumekuwa tukijadili kwa faragha. Jamii yetu imejengwa juu ya kukusanya taarifa nyingi iwezekanavyo, zinazotumiwa ama kutangaza na kuuza vitu, kutathmini ubora wa raia au wafanyakazi, au kutuadhibu kwa uhalifu tunaofanya au tunaoweza kuufanya katika siku zijazo.

Katika muktadha huu ni rahisi kusoma Biblia katika hali hii ya akili. Chukua kwa mfano Danieli 7.

> “Nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa, na mmoja aliye mzee wa siku ameketi; mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa chake kama sufu safi; kiti chake cha enzi kilikuwa miali ya moto, na gurudumu zake moto uwakao. Mto kama wa moto ukatoka ukapita mbele zake; maelfu elfu wakamtumikia, na elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele zake; hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa.” — Danieli 7:9-10

Picha hapa inatuonyesha tukio kubwa la mahakama ambapo taarifa zote za uchunguzi uliokusanywa zinakaguliwa na kila mtu atakabiliwa na thawabu yake husika au, kuna uwezekano mkubwa, adhabu yake husika. Huu ndio upande mzito wa kisa cha Santa Claus. Hatushughuliki tena katika viwango rahisi ambavyo ndani yake tunahukumu watoto; tunashughulika na Mungu mweza yote ambaye viwango vyake ni vya juu sana. Danieli 7 inatuletea maono si ya Mungu ambaye amepanda juu ya kulungu kutoka kwenye Ncha ya Kaskazini, bali ni kiti cha enzi cha ajabu cha Mungu ambaye kutoka kwake moto unatoka, pamoja na kundi la watu wa mbinguni tayari kuwasababishia kifo watenda mabaya.

Tunaweza kumgeukia Yesu ili kupata faraja, lakini kisha tunasoma maneno yake na kutetemeka:

> Basi, nawaambia, Kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu. Kwa

> kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa. — Mathayo 12:36-37

> Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache. — Mathayo 7:13-14

Ni katika mstari huu wa mawazo ambapo kijana Martin Luther, akisimamia huduma yake ya kwanza ya kidini, alilemewa na mawazo ya ukuu wa Mungu.

> Nilijisemea moyoni, "Kwa ulimi gani nitazungumza na ukuu kama huu, kwa kuona kwamba watu wote wanapaswa kutetemeka mbele ya mkuu wa kidunia? Mimi ni nani, hata nipate kuinua macho yangu, au kuinua mikono yangu kwa Ukuu wa Mungu? Malaika wanamzunguka. Kwa kutikisa kichwa chake nchi inatetemeka. Na je, mimi, mbwa-mwitu mwenye huzuni, niseme 'Nataka hiki, naomba kile'? Kwa maana mimi ni mavumbi na majivu na nimejaa dhambi na ninasema na Mungu aliye hai, wa milele na wa kweli."[10]

Ni aina hii ya hofu inayopelekea mateso. Katika mwendelezo wa wazo la Luther tunaona likionyesha hitimisho la asili.

> Sikuweza kuamini kwamba jambo lolote nililofikiri au kufanya au kusali lilimtosheleza Mungu. Sikupenda, bali, nilimchukia Mungu mwadilifu ambaye huwaadhibu wenye dhambi.

> Kwa hakika, na kwa manung'uniko makali (pengine hata kukufuru), nilimkasirikia Mungu na kusema, 'Kana kwamba haitoshi kwa hakika wadhambi wabaya ambao wamepotea milele kupitia dhambi ya asili na kupondwa tena na kila balaa kupitia zile

---

[10] Roland Bainton, Here I Stand (NAL, 1978)

> Amri Kumi. Mungu mwenyewe anaongeza uchungu juu ya uchungu katika injili kwa kututishia kwa haki na ghadhabu yake!'[11]

Je, haya si matokeo yasiyoepukika ya kufuatilia mtu, kuangalia kama anafanya jambo baya na kutishia adhabu kwa kushindwa kwake? Je, mchakato mzima hauonyeshi kwamba mungu kama huyo anatarajia kutofaulu na hivyo anaweza kuwezesha mchakato wa kutofaulu?

Ukristo unafikiria kwamba haki ya Mungu inadai adhabu, na kwa hivyo Mungu anamtoa Mwanawe kama dhabihu ya upatanisho. Ili kutosheleza ghadhabu ya Mungu aliyekosewa ambaye sheria yake imekiukwa, Mungu anamtoa Mwanawe mwenyewe ili alipe adhabu yetu ya kifo. Hili linaonyeshwa kama rehema. Kifo tulichokistahili kimelipwa na Mwana wa Mungu.

Swali linalopaswa kuulizwa ni - lilikuwa ni wazo la nani kwamba haki inadai kifo cha mvunja sheria?

[11] Luther's Works, Vol 34, p.336-338

SURA YA 3

# Haki na Hukumu

Kwa wanafunzi wa historia, shindano kati ya haki ya kimungu ya wafalme na utawala wa sheria kama unavyosimamiwa na bunge lililochaguliwa huonekana kuwakilisha dhana mbili tofauti za serikali. Labda ilikuwa zaidi ya tukio la kwamba katika sinema mbili zinazoonyesha maisha ya Julius Caesar na Oliver Cromwell tunapata mwigizaji yuleyule: Richard Harris.[12] Oliver Cromwell aliongoza bunge la Uingereza kumuua mfalme wake, Charles I, kwa uhaini dhidi ya watu. Julius Caesar alienda kinyume dhidi ya jamhuri ya Roma ili kuanzisha mwanzo wa Dola ya Kirumi. Uaminifu wa askari wake na ushindi wake wa kijeshi ulikuwa msingi wa kuchukua kwake madaraka.



Bila kujali taifa linatawaliwa na utawala wa kifalme au demokrasia, kuna jambo moja ambalo wote wanalikubali: matumizi ya nguvu ili kuzipa nguvu sheria zilizotungwa.

[12] https://en.wikipedia.org/wiki/Cromwell_(film), https://en.wikipedia.org/wiki/Julius_Caesar_(miniseries)

Utawala wa sheria unafafanuliwa katika Kamusi ya Kiingereza ya Oxford kama: "Mamlaka na ushawishi wa sheria katika jamii, hasa inapozingatiwa kuwa kikwazo kwa tabia ya mtu binafsi na ya kitaasisi; (kwa hivyo) kanuni ambapo watu wote katika jamii (pamoja na wale walio serikalini) wanachukuliwa kuwa sawa chini ya kanuni na taratibu za kisheria zilizowekwa hadharani." Taswira hii ya musa inaonyesha mwanamke mwenye tawi la mitende ili kutoa thawabu na upanga wa kutoa adhabu kwa wale wanaovunja sheria.

Nadharia ya haki ya kimungu ya kutawala ambayo ilitawala jamii katika Enzi za Kati ilikuwa na mtazano kwamba mfalme alikuwa ni mwakilishi wa Mungu.

> Askofu Jacques-Bénigne Bossuet (1627–1704), mmoja wa wananadharia wakuu wa Kifaransa wa haki ya kimungu, alidai kwamba nafsi na mamlaka ya mfalme yalikuwa matakatifu; kwamba uwezo wake ulifananishwa na ule wa baba na ulikuwa kamili, unaotokana na Mungu; na kwamba alitawaliwa na akili (yaani, desturi na mfano).[13]

Ni katika muktadha huu ambapo watafsiri wa Biblia wakati wa Enzi za Kati waliweka uelewa wao kuhusiana na haki.

> Haki na hukumu ndio maskani ya kiti chako cha enzi, fadhili na kweli zitakutangulia. — Zaburi 89:14 (KJV).

> Mawingu na giza vimemzunguka, Haki na hukumu ndio makao ya kiti chake cha enzi. Moto hutangulia mbele zake na kuwateketeza adui zake pande zote. Umeme wake ukauangazia ulimwengu; nchi iliona, ikatetemeka. Milima ikayeyuka kama nta mbele za uso wa Bwana, Mbele za Bwana wa dunia yote. — Zaburi 97:2-5 (KJV)

Ni kanuni ya nguvu inayoonekana kuunga mkono ukuu wa Mungu.

> Maana nainua mkono wangu mbinguni, na kusema, Ninaishi milele. Nikinoa upanga wangu unaometa, Na mkono wangu

[13] https://www.britannica.com/topic/divine-right-of-kings

> ukishika hukumu; Nitalipiza kisasi kwa adui zangu, na nitawalipa wale wanaonichukia. Nitailevya mishale yangu kwa damu, na upanga wangu utakula nyama; na kwamba kwa damu ya waliouawa na wafungwa, tangu mwanzo wa kisasi juu ya adui. — Kumbukumbu la Torati 32:40-42 (KJV)

Inaaminika karibia ulimwenguni kote kwamba ukuu wa Mungu, na kwa hiyo viongozi wote wa kijamii wanaotawala miongoni mwa watu, huitegemeza haki juu ya uwezo wa kutumia upanga (yaani kutumia nguvu kulazimisha). Uadilifu ni kuhukumu matendo kuwa mema au mabaya na hivyo kuwalipa wema na kuwaadhibu wabaya.

Kwa hiyo ni tishio la adhabu ya kifo ndilo linalohifadhi uhai. Katika kulipanua wazo hili, tunasoma mambo kama haya katika mawazo ya Kikristo:

Katika kiini cha theolojia ya Kikristo ni dhana kwamba kifo kilicholetwa kwa mvunjaji wa sheria yake ni haki ya Mungu.

> Akiwa amejikita katika msingi wa tabia Yake ya haki, hitaji la Mungu la uzima wa milele halijabadilika kamwe. Mungu habadilishi kiwango chake cha haki kwa sababu tunakataa kuitii kama vile hakimu anavyobadilisha kikomo cha mwendo kasi tunapopata tiketi ya mwendo kasi. Badala yake, dhambi ya Adamu iliongeza adhabu ya kifo cha kimwili na cha kiroho kwa kutotii deni la utii mkamilifu. Bila ubaguzi, msamaha wa dhambi na uzima wa milele hauwezekani bila kuiridhisha kikamilifu haki ya Mungu. **Mwenyezi Mungu asingekuwa Mungu kama angeachana na uadilifu wake ili kuokoa nafsi moja.[14]**

Katika kiini cha theolojia ya Kikristo ni dhana kwamba kifo kilicholetwa kwa mvunjaji wa sheria yake ni haki ya Mungu. Wazo hili linatokana na wazo kwamba kiti cha enzi cha Mungu kimejengwa juu ya tishio la kifo. Kiti chake cha enzi pia kimejengwa juu ya hukumu na laana ya wale wanaovunja sheria yake.

---

[14] https://bible.org/article/god-s-perfect-and-unchanging-justice-ground-gospel

Hata hivyo, katika Zaburi ya 89 tunasoma kwamba rehema huenda mbele ya uso wa Mungu. Je, tunaingizaje rehema katika dhana hii ya haki inayodai kifo cha mkosaji? Hebu tuangazie maana ya msingi ya neno la Kiingereza *mercy-rehema*.

> Rehema (Kiingereza cha kati, kutoka Anglo-French merci, kutoka Medieval Latin merced-, merces, kutoka Kilatini, "bei iliyolipwa, mshahara", kutoka merc-, merxi "merchandise") ni ukarimu, msamaha, na fadhili katika anuwai ya maadili. , muktadha wa kidini, kijamii na kisheria.[15]

Rehema hupatikana kupitia bei au ujira unaolipwa. Kwa hivyo, katika ufafanuzi huu, rehema inaweza kutolewa ikiwa deni la haki litafikiwa. Haki lazima itosheke ili kudumisha heshima na uadilifu wake. Kwa hivyo, ikiwa mshahara wa deni umelipwa, bila kujali ni nani aliyelipa, basi haki hudumisha uadilifu wake, na rehema inaweza kutolewa. Hili huleta nadharia ya Kikristo ya upatanisho iitwayo 'Adhabu ya Mbadala (Penal Substitution)'.

> Adhabu ya mbadala (wakati mwingine, hasa katika maandishi ya zamani, inayoitwa nadharia ya uchunguzi) ni nadharia ya upatanisho ndani ya theolojia ya Kikristo, ambayo inabisha kwamba Kristo, kwa chaguo lake la dhabihu, aliadhibiwa (kuadhibiwa) mahali pa wenye dhambi (mbadala), hivyo kukidhi matakwa ya haki ili Mungu aweze kusamehe dhambi kwa haki.[16]

Maana ya neno rehema linatoa wazo hili la mshahara au deni kulipwa. Katika mapokeo ya Kiprotestanti deni hili linaweza tu kulipwa kupitia kifo cha Kristo kwa niaba yetu. Katika mapokeo ya Kirumi mtu anaweza kuongeza sifa kupitia matendo mema ili kusaidia katika wokovu wa roho zao.[17]

Kwa muhtasari, tunaona kwamba mitazamo ya wanadamu kuhusu haki, yote kutoka kwenye Maandiko na kwa wanadamu kwa ujumla, inatokana na kanuni kwamba adhabu kali au hata kifo inahitajika ili kutekeleza kanuni za sheria.

---

[15] https://en.wikipedia.org/wiki/Mercy
[16] https://en.wikipedia.org/wiki/Penal_substitution
[17] https://en.wikipedia.org/wiki/Merit_(Christianity)

Kwa hiyo mfumo huu unahitaji uangalizi, hukumu, laana na kifo. Mambo haya ni ya asili katika dhana hii ya haki. Swali linalopaswa kuulizwa ni je, mfumo huu wa haki unaweza kuzalisha jamii huru bila woga? Ikiwa Mungu katika asili Yake hasa ndiye msanifu wa kifo na ndiye mwenye enzi kuu zaidi ambaye husababisha kifo, basi je, si Mungu Mwenyewe, katika kiini Chake hasa, mfano wa kifo? Ikiwa Mungu anafuatilia kila kitendo chetu na kukipima dhidi ya kiwango chake cha kimungu ili kuona kama tunakifikia, basi kunawezaje kuwa na mahali ambapo raia Wake watakuwa huru kutokana na hofu ya kifo? Katika mfumo huu Mungu anahusishwa milele na hukumu, laana na kifo.

Tofauti na Santa Claus ambaye ana orodha ya walio wema na wabaya, Mungu "hatunzi rekodi ya makosa yoyote." Ikiwa hatatunza orodha, basi jumla ya kanuni zote ambazo ubinadamu huzichukulia na kuzielewa kuhusiana na haki na hukumu yake si sahihi.

Ni katika uwanja huu ambapo ningependa kuweka mbele yenu mafungu matatu ya Biblia kama utangulizi katika sehemu nyingine ya kitabu hiki.

> Tena Baba **hamhukumu** mtu ye yote, bali amempa Mwana hukumu yote; — Yohana 5:22
>
> Ninyi mwahukumu kwa kufuata mambo ya mwili; mimi [Yesu] **simhukumu** mtu. — Yohana 8:15
>
> Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; **hauhesabu mabaya**; 1 Wakorintho 13:4-5 (NIV).

Mafungu haya matatu yanapinga moja kwa moja mawazo ya haki na hukumu yanayojikita juu ya tishio la kifo. Yesu anatuambia kwamba Baba Yake wala Yeye Mwenyewe hahukumu, halaani, hajaribu, au kumwadhibu yeyote.[18] Sura kuu ya upendo katika Biblia inatuambia kwamba upendo

[18] The Greek word for judge here is Krino which in this case means to decide, try, condemn, punish.

hautunzi kumbukumbu ya makosa. Mungu ni upendo, na upendo huu mkamilifu wa Mungu huitupa nje au kuondoa woga wote (1 Yohana 4:8,18). Tofauti na Santa Claus ambaye ana orodha ya walio wema na wabaya, Mungu "hatunzi rekodi ya makosa yoyote." Ikiwa hatatunza orodha, basi jumla ya kanuni zote ambazo ubinadamu huzichukulia na kuzielewa kuhusiana na haki na hukumu yake si sahihi. Kama Yesu alivyotuambia, "mnahukumu kulingana na mwili." Biblia inatuambia:

> Mtu mbaya na aache njia yake, na mtu asiye haki aache mawazo yake; na amrudie BWANA, naye atamrehemu; na kwa Mungu wetu, kwa maana atamsamehe kabisa. Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu, asema BWANA. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu. — Isaya 55:7-9 ( KJV)

Je, tuna uhakika kwamba tunaelewa haki ya Mungu kwa usahihi? Tunawezaje kufafanua maandiko haya ya Biblia na kuyafanya kupatana na mengine mengi ambayo yanaonekana kusema kinyume? Upendo unawezaje kuweka rekodi ya makosa wakati mfumo wa haki ambao tumeuona unadai mchakato kama huo? Mawazo haya yanapingana, na kazi yetu ni kutatua mkanganyiko huu kwa maombi ili kwamba haki na rehema ya kweli ya Mungu iweze kufunuliwa kwetu.

SURA YA 4

# Chimbuko la Hukumu ya Adhabu

Maisha na maneno ya Yesu yanatufunulia mwanga wa utukufu wa jinsi Mungu Baba alivyo hasa. Yesu aliposema kwamba Yeye wala Baba Yake hahukumu, hajaribu, au kumwadhibu mtu ye yote, swali la haraka linalohitaji kushughulikiwa ni: ikiwa hamhukumu mtu yeyote, basi kwa nini ulimwengu umejaa hukumu na adhabu? Kwa nini watu huwahukumu wengine sana na haya yote yalianzia wapi?

Mungu alipowakaribia Adamu na Hawa katika bustani ya Edeni baada ya kula tunda walilokatazwa, walikimbia na kujificha mbele zake kwa hofu. Waliogopa hukumu na adhabu ya Mungu inayoweza kutokea kwa matendo ambayo walijua si mazuri. Alipoulizwa juu ya kile alichokifanya, Adamu alijibu kwa kusema:

> Mwanamke uliyemweka hapa pamoja nami - alinipa matunda ya mti huo, nikala. — Mwanzo 3:12 (NIV)

Adamu alihukumu kwamba Mungu alikuwa na makosa kwa kumleta mwanamke ambaye alimshawishi aende katika njia mbaya. Ni wazi kwamba Adamu alimlaumu Mungu kwa matendo yake. Adamu alifikiri kwamba Mungu alikuwa amekuja kukomesha maisha yake kama adhabu kwa ajili ya tendo alilofanya. Je! Mungu hakusema, "Kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika?" (Mwanzo 2:17).

Tunajua kwamba Adamu aliogopa kifo kutokana na kifungu kifuatacho:

> Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi, **awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa**. — Waebrania 2:14-15

Kama wanadamu kwa asili tunaogopa kifo. Hii ni sehemu ya urithi wetu kutoka kwa Adamu. Adamu alifikiri kwamba Mungu alitaka kumuua kwa kushindwa kufuata maagizo yake. Adamu alimhukumu Mungu kuwa ndiye aliyesababisha tatizo hilo na kwa hiyo akashtaki kwamba Mungu alipaswa kulipa hukumu ya kifo kwa kosa lililofanywa. Hakusema hivi moja kwa moja, lakini Biblia inatuambia yaliyotokea tangu mwanzo.

> Na watu wote wakaao juu ya nchi watamsujudu, kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo, **aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia.** — Ufunuo wa Yohana 13:8

Je, tunaweza kuwa na uhakika kwamba kwa kweli Adamu alihisi hivyo kumhusu Mungu na Mwana Wake?

> **Akili yenye dhambi iko vitani na Mungu**. Haitii sheria ya Mungu. Haiwezi. — Warumi 8:7 ( NIV)

Adamu alipovunja amri ya Mungu, alianguka katika dhambi. Akili yake ikawa katika vita na Mungu. Hakutamani tena kutii sheria ya Mungu. Akili yake ilikuwa imejaa shutuma na hukumu kwa Mungu. Hii ni kwa sababu alikuwa amemchagua Shetani kuwa bwana wake na kwa hiyo akaanza kuwaza kama Shetani. Shetani aliwaza nini tangu mwanzo? Sikiliza kile Yesu anachowaambia viongozi wa Kiyahudi waliokuwa wakijaribu kumuua:

> Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi, na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. **Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli**, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo, na baba wa huo. — Yohana 8:44

Shetani alitamani kumwua Mwana wa Mungu tangu mwanzo. Alitamani kuchukua nafasi ya Kristo na kuwa sawa na Mungu.

> Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, Ewe uliyewaangusha mataifa! Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, Katika pande za mwisho za kaskazini. **Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye Aliye juu.** — Isaya 14:12-14

Katika maneno na matendo ya viongozi wa Kiyahudi tunaona ikidhihirishwa roho ya Shetani kwa Yesu. Katika chuki yao na tamaa ya kumuua Mwana wa Mungu tunaona tamaa za Shetani ambaye alitaka kumuua Mwana wa Mungu tangu mwanzo na kuchukua nafasi yake ya kuwa sawa na Baba; aliye juu.

Shetani ndiye aliyeanzisha roho ya mashtaka na hukumu. Biblia inamwita "mshitaki wa ndugu zetu."

> Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye. Nikasikia sauti kuu mbinguni, ikisema, Sasa kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake; **kwa maana ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu, mchana na usiku.** — Ufunuo wa Yohana 12:9-10

Roho ya mshitaki iliingia ndani ya moyo wa Adamu na akahukumu, akamshtaki, na kumlaumu Mwana wa Mungu kwa kumuumba[19] Hawa kuwa mjaribu wake. Ni kwa njia ya Adamu kwamba roho ya hukumu na kulaumu ilikuja ulimwenguni. Adamu hakumwomba Mungu amsamehe; Adamu hakufikiri dhambi yake inaweza kusamehewa. Tofauti na Nuhu, hadi wakati huu Adamu hakupata neema machoni pa Mungu (Mwanzo 6:8). Adamu alijawa na mashtaka na kutoamini (roho ya Shetani), badala ya toba na imani

[19] God created all things through Jesus Christ. Ephesians 3:9

(roho ya Kristo). Mtume Paulo anaeleza ukweli huu wa kina katika mstari huu:

> Wala karama ile si kama ilivyokuwa kwa mtu mmoja aliyetenda dhambi; **kwa maana hukumu ilikuja kwa mmoja kuleta hukumu;** bali karama ya bure inatokana na makosa mengi hata kuhesabiwa haki. — Warumi 5:16(KJV).

Tunahitaji kuuchunguza mstari huo kwa makini kwa sababu wengi wanaona mstari huu kuwa ni Mungu anayemhukumu Adamu. Hapa kuna maoni maarufu:

Hukumu - Hukumu; adhabu iliyotangazwa. Neno hueleza vizuri hukumu ambayo hupitishwa na hakimu. Hapa ina maana ya hukumu ambayo Mungu aliitoa, kama hakimu, juu ya Adamu kwa kosa moja, lililohusisha yeye mwenyewe na uzao wake katika uharibifu, Mwanzo 2:17; Mwanzo 3:17-19. *Albert Barnes Commentary*

Matoleo kadhaa ya Biblia yanaonekana kuunga mkono wazo la kwamba ni Mungu anayemhukumu Adamu.

> Na zawadi si kama ile iliyotolewa na yule aliyetenda dhambi. **Kwa maana hukumu iliyotokana na kosa moja ilileta adhabu**, lakini zawadi ya bure iliyotokana na makosa mengi ilileta kuhesabiwa haki. — Warumi 5:16
>
> Wala karama ya Mungu haiwezi kulinganishwa na matokeo ya dhambi ya mtu mmoja: **Hukumu ilifuata dhambi ya mtu mmoja na kuleta adhabu**, lakini zawadi hiyo ilifuata makosa mengi na kuleta kuhesabiwa haki. — Warumi 5:16 ( NIV)

Tafsiri hizi zinaonyesha kwamba kosa la Adamu lilimletea hukumu ya Mungu. Hata hivyo, tunakumbuka kwamba Yesu alituambia kwamba Baba hamlaumu yeyote katika Yohana 5:22, kwa hiyo hii haiwezi kuwa kweli. Fikiria Tafsiri ya Young’s Literal Translation:

> Wala si kama vile karama ya mtu mmoja aliyetenda dhambi ilivyo bure; **kwa maana hukumu inaleta adhabu**, bali karama hiyo ni

> kwa ajili ya makosa mengi hata kutangazwa kuwa mwenye haki,
> — Warumi 5:16. (YLT)

Tunaona kutokana na tafsiri hii kwamba hukumu inaleta adhabu. Neno la Kigiriki lililotafsiriwa hapa ofis ek ambalo linamaanisha:

Kihusishi cha msingi kinachoashiria asili (mahali ambapo mwendo au kitendo hutoka), kutoka, nje. *Strong's Concordance*

Hili husema kwamba hukumu ilitoka kwa mtu mmoja, Adamu, hadi Adhabu. Adamu ndiye chimbuko la hukumu na adhabu ya kibinadamu. Kristo anatofautishwa na hili akitoa zawadi ya bure ya haki yake kama mbadala wa makosa mengi. Kristo ni kinyume na Adamu. Kristo anatoa bure neema na haki huku Adamu akitoa hukumu na adhabu. Wengi wa ulimwengu wa Kikristo wamekosa kabisa maana ya mstari huu.

> Adamu ndiye chimbuko la hukumu na adhabu ya kibinadamu.

Katika aya za awali za Warumi sura ya 5 tunaona tatizo hili hili likitokea kuhusu ni nani anayehukumu.

> Bali **Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi**, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi. Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, **tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye**. — Warumi 5:8-9

Je, tunaokolewa kutoka kwenye ghadhabu ya nani? Wacha tuangalie matoleo machache:

> Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu ***ya Mungu*** kwa yeye. — Warumi 5:9 (NASB)

> Kwa kuwa sasa tumehesabiwa haki kwa damu yake, si zaidi sana tutaokolewa na **ghadhabu ya Mungu** kwa yeye! — Warumi 5:9 (NIV)

Maneno "ya Mungu" yameongezwa na mfasiri katika NASB na wanakubali hili kwa maandishi, lakini katika NIV na tafsiri zingine inaonyeshwa kwa

urahisi kama ghadhabu ya Mungu. Kigiriki hakina neno Mungu hata kidogo. Ikiwa kauli 'ghadhabu ya Mungu' ipo katika mstari wa 9, basi inachanganya maana ya mstari wa 8 ambapo Mungu anaonyesha upendo wake kwetu. Je, unaweza kuonyesha upendo na hasira kwa mtu kwa wakati mmoja? Je, unaweza kutamani kuokoa na kuua mtu kwa wakati mmoja?

Toleo la New King James pamoja na King James wanalitafsiri kwa usahihi. Matoleo haya yanasema tu kwamba tutaokolewa kutoka kwenye ghadhabu. Je, tunaokolewa kutoka kwenye ghadhabu ya nani? Mstari wa 10 unatuambia kwamba sisi tulikuwa maadui wa Mungu. Mistari iliyotajwa hapo juu ya Warumi 5:16, 17 inatuambia kwamba Adhabu ilitoka kwa Adamu. Kwa hiyo, kwa njia ya Kristo, tunaokolewa kutoka katika adhabu tuliyoirithi kutoka kwa Adamu.

Katika muktadha huu fungu maarufu la Warumi 8:1 linaleta maana zaidi.

> Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, wasioenenda kwa kufuata mwili bali kwa kufuata Roho. — Warumi 8:1

Hakuwezi kuwa na hukumu wakati umejazwa na Roho wa Kristo kwa sababu Kristo hahukumu. Unapokuwa na Roho wake basi hutahukumu. Hivi ndivyo Yesu alivyotufundisha.

> Msihukumu, msije mkahukumiwa. — Mathayo 7:1

Watu wengi wanaamini kwamba sababu ya sisi kutohukumiwa tukiwa ndani ya Kristo ni kwa sababu Yesu anatukinga na hukumu ya Mungu. Haya ni mawazo ya kutisha kuhusu jinsi Mungu alivyo, na ni ya uongo, kwa kuwa Yesu alituambia kwamba Baba hahukumu wala kumwadhibu mtu yeyote.

Tunapokuwa ndani ya Kristo, roho ya kuhukumu inatutoka na nafasi yake inachukuliwa na Roho wa Baba na Mwanawe; Roho ambayo haiwahukumu wengine na kwa hiyo sisi pia tunaacha kuwahukumu wengine.

Je, unaweza kuona kwamba ni Adamu aliyemhukumu na kumwadhibu Mwana wa Mungu tangu mwanzo, na kwa sababu hukumu hutangulia mauaji, Mwana-Kondoo alichinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu?

Tunapowazia andiko la Warumi 5:16 likisema kwamba Mungu alikuwa akimhukumu na kumwadhibu Adamu, tunaonyesha kwamba tunafikiri kama Adamu; tunamwazia Mungu kama anayehukumu wakati ukweli ni sisi. Tunaelekeza mawazo yetu kwa Mungu na kumwazia kuwa kama sisi.

> Tunapokuwa ndani ya Kristo, roho ya kuhukumu inatutoka na nafasi yake inachukuliwa na Roho wa Baba na Mwanawe; Roho ambayo haiwahukumu wengine na kwa hiyo sisi pia tunaacha kuwahukumu wengine.

> Mambo haya umeyafanya, nami nikanyamaza; ulidhani mimi ni kama wewe... — Zaburi 50:21

SURA YA 5

# Mtazamo, Uelekezaji, na Uhalisia

Hivi majuzi nilikuwa nikisoma maoni kutoka kwa watu baada ya kuandika kauli hii na kuitafuta katika mtandao, "Wewe si mtu niliyefikiri kuwa." Nilisoma hadithi kadhaa za watu wakionyesha hasira, huzuni na masikitiko yao kwa kutambua mtu waliyekuwa naye kwenye uhusiano sio mtu aliyemdhania kuwa. Mtazamo na uhalisia ulikuwa tofauti kabisa.

Matukio ambayo yanaunganishwa na kusababisha watu wawili kupendana mara nyingi hutafsiriwa tofauti kabisa na pande hizo mbili. Tabasamu, zawadi na miguso ambayo kwa kawaida hueleweka na mwanamke kumaanisha kwamba mvulana anayependezwa naye kweli anamjali inaweza kumaanisha kitu kingine. Cha kusikitisha ni kwamba mara nyingi matukio haya ni mambo ambayo mwanamume yuko tayari kuyafanya ili kupata kile anachokitaka. Hili bila shaka linaweza kutokea kinyume chake pia, na kuna uwezekano wa kudanganywa katika uhusiano wowote katika ulimwengu wetu.

Mambo haya hutokea mara nyingi pale unapoamua kuwa karibu na mtu kwa haraka kabla ya kupata muda wa kutambua tabia yake.

Nilipokuwa nikisoma hadithi hizo nilikutana na hadithi tofauti inayozungumzia baadhi ya changamoto ambazo Baba yetu wa mbinguni hukabiliana nazo katika kushughulika na jamii ya wanadamu:

> Kwa afisa wa polisi aliyenipeleka hospitalini
>
> Nilikuwa na hofu kwamba ungenifokea, ukanitusi, na kuniambia jinsi ilivyokuwa ni ubinafsi na woga kwa kujaribu kujiua mwenyewe. Badala yake, uliniacha niketi kwenye kiti cha mbele ulipokuwa ukiendesha gari na kuniuliza ikiwa nilipenda muziki uliokuwa ukipigwa redioni. Ulijifanya hukuniona nikilia.[20]

Afisa wa polisi alipomkaribia mwanamke huyu, aliwazia kwamba angemhukumu na angemwadhibu kwa matendo yake. Katika hadithi hii aliacha mtazamo wake wa asili wa polisi na akaanza kutafsiri matendo yake kama mwenye fadhili na kujali.

Hadithi hii inaweza kuwa na mwisho tofauti. Pale polisi walipomwomba aingie ndani ya gari, huenda alifikiri kwamba alitaka kumwadhibu na kumweka wazi kwa yale aliyofanya. Huenda alimfokea polisi huyo na kumwambia amwache peke yake. Matendo yake yote yangetegemea jinsi alivyowaona polisi, na mtazamo wake ungekuwa na athari kubwa kwa kile kilichotokea.

Vipi kama mwanamke huyu angeenda nyumbani na kumwambia binti yake kuhusu huyu "polisi wa kutisha" ambaye alijaribu kumdhuru, na kumpa binti yake mtazamo wa jinsi polisi walivyo? Mtazamo huo unakuwa wa kurithi na kupitishwa kwa kizazi kijacho na dhana potofu inadumishwa.

Adamu alipokula tunda la mti, alifanya hivyo akiwa na mtazamo usiyofaa kwamba Mungu angemuua mke wake kwa ajili ya kosa lake. Alielewa maneno ya Mungu kwamba - ikiwa utakula *matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya*, basi utakufa - kumaanisha kwamba Mungu atawaua (Mwanzo 2:17).

Maana halisi ya maneno ya Kiebrania ni *kufa utakufa*. Hawa aliponukuu maneno ya Mungu kwa nyoka, alibadilisha maana kidogo tu kusema tukila matunda ya kwamba ni lazima tufe (Mwanzo 3:3). Mtazamo huo ndio

[20] www.reddit.com/r/UnsentLetters/comments/gg2lps/to_the_police_officer_who_drove_me_to_the/

uliomfanya Adamu kufikia hitimisho kwamba Mungu alitaka kumuua mke wake. Alichukua tunda kwa uasi na kuamua kukabiliana na matokeo.

Hawa alidanganywa lakini Adamu hakudanganywa. Kitendo chake kilikuwa katika ukaidi wa moja kwa moja kwa Mungu uliojikita kwenye dhana potofu ya tabia ya Mungu. Adamu hakungoja kuongea na Mungu ili kumwomba mwongozo wa kile alichopaswa kufanya. Alichukua mambo mikononi mwake na kuhukumu hali hiyo. Alihukumu kwamba Mungu aliwahukumu ambapo kwa uhalisia ndiye aliyemhukumu Mungu. Adamu alielekeza kwa Mungu kile ambacho yeye mwenyewe alikuwa akikiwazia. Walakini, mtazamo wake haukuwa halisia.

Adamu alidhania kwamba Mungu alikuwa ni mtu anayehukumu, kulaumu, na kuadhibu. Alitambua hili kwa sababu ndivyo alivyokuwa amefanya katika akili yake dhidi ya Mungu.

1. Alikuwa amemhukumu Mungu kuwa si wa haki.
2. Alimhukumu Mungu kuwa anastahili kifo.

Kuwazia mambo haya kumhusu Mungu kulimaanisha tu kwamba Alipomwona Mungu, kile ambacho alikuwa amekitamani kumfanyia Mungu, alifikiri kwamba Mungu angemtendea hicho. Hili linatupeleka kwenye kanuni muhimu:

Mitazamo potofu ya watu katika maisha yetu hutenda kazi kama kioo tunapoishi nao na kuhusiana nao.

Dhana potofu ya Adamu juu ya tabia ya Mungu ilizaa uasi katika akili ya Adamu, ambao ulichipuka na kuwa na tamaa isiyoonekana ya kumuua Mwana wa Mungu. Kwa hiyo, Mwana wa Mungu alipokuja kwa Adamu katika bustani, Adamu aliogopa jambo alilowazia kumfanyia Mwana wa Mungu. Adamu alimchukia na kumhukumu Mwana wa Mungu kwa hali aliyokuwa nayo na alitaka Kristo afe, kwa hiyo Adamu aliogopa kwamba Mwana wa Mungu alimchukia, alimhukumu na kutaka afe. Wazo hili ni muhimu sana kulielewa ikiwa tunataka kuelewa hitaji, na maana ya, hukumu.

Tunaona kanuni hii kwa Kaini. Baada ya Kaini kumuua ndugu yake, aliogopa kwamba wengine wangetaka kumuua.

> Tazama, umenifukuza leo katika uso wa ardhi, nitasitirika mbali na uso wako, nami nitakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani; hata itakuwa **kila anionaye ataniua**. — Mwanzo 4:14

Katika ulimwengu wa saikolojia mchakato huu unaitwa uelekezaji wa kisaikolojia:

> Makisio ya kisaikolojia ni utaratibu wa kujilinda ambapo nafsi ya mwanadamu hujilinda dhidi ya msukumo usio wa hiari au sifa (zote chanya na hasi) kwa kukataa kuwepo kwazo ndani yao wenyewe huku ukizihusisha na wengine.[21]

Wakati Mwana wa Mungu anakuja kwa Adamu katika bustani na moyo wa Adamu umejaa hukumu, ghadhabu na kifo dhidi yake, katika kujilinda Adamu anaelekeza mawazo yake kwa Mwana wa Mungu na kwa hivyo kwa Mungu Mwenyewe. Adamu hakuwa na fahamu kuhusu misukumo iliyokuwa ndani yake. Alikataa kuwepo kwazo ndani yake mwenyewe, na badala yake akazihusisha na Mwana wa Mungu.

Je, Adamu angewezaje kufikiwa? Je, angewezaje kuletwa katika uelewa wa hisia zake za asili dhidi ya Mwana wa Mungu na hatimaye Baba Yake?

Adamu, mwanzilishi wa kibinadamu wa kuhukumu wengine, alipitisha hili kwa watoto wake, nao wakawapitishia watoto wao. Hivyo hukumu ya adhabu inafanywa na watu wote, kwa maana wote wamefanya dhambi katika hatua hii. Hukumu hii inapelekea katika kila aina ya uovu uliopo duniani.

Ni mchakato gani ungehitajika kumfunulia Adamu hali yake ya kweli, wakati huohuo kumfunulia rehema na msamaha wa Mungu, Ambaye alikuwa tayari kabisa kumsamehe bila fedha na bila gharama? (Isaya 55:1). Dhana mbaya ya mwanadamu iliyokita mizizi juu ya Mungu ingeponywaje?

[21] https://en.wikipedia.org/wiki/Psychological_projection

SURA YA 6

# Kwa ajili Yako Ardhi Imelaaniwa

Je, umewahi kushika aina tofauti za mbegu mkononi mwako? Je, unaweza kujua kila mbegu itazaa nini? Linahitajika jicho la uchunguzi kuweza kutambua kile ambacho mbegu husika itakizaa. Ikiwa hatuna ufahamu wa hapo awali wa kile kilicho ndani ya mbegu, ni lazima tuipande na kuimwagilia maji na kuiangalia ikikua ili kujifunza kile kilicho ndani ya mbegu. Maua yake au matunda yanapochipuka, ndipo tunaweza kuona matunda yake na kuonja matokeo yake na kujua kama ni mazuri au mabaya (Mathayo 7:16-20).

Mbegu mbaya iliyokuwa ndani ya Adamu ilihitaji kukua, na alihitaji kuonja tunda lake la kiroho ili kutambua utambulisho/tabia ya mbegu hiyo na kujua kama ilikuwa nzuri au mbaya.

> Akamwambia Adamu, Kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nalikuagiza, nikisema, Usiyale; **ardhi imelaaniwa kwa ajili yako**; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako; michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni; kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi. — Mwanzo 3:17-19

Laana iliyoanguka juu ya ardhi haikutoka kwa Mungu; laana ilikuwepo ndani ya moyo wa Adamu na ikaingia ardhini kupitia jukumu lake kama kichwa chenye mamlaka juu ya ardhi. Lakini Adamu hakujua kwamba moyo wake ulikuwa umejaa laana.

Shetani alipokuwa akishindana na Mungu kuhusu tabia ya Ayubu, alihisi hakika kwamba angeweza kumsababisha Ayubu atoe maneno ya laana kama hii. Haya ni maneno ya Shetani kwa Mungu:

> Wewe hukumzingira[Ayubu] kwa ukigo pande zote, pamoja na nyumba yake, na vitu vyote alivyo navyo? Kazi za mikono yake umezibarikia, nayo mali yake imeongezeka katika nchi. Lakini nyosha mkono wako sasa, uyaguse hayo yote aliyo nayo, naye atakukufuru mbele za uso wako. — Ayubu 1:10-11

Mungu alimbariki sana Ayubu. Shetani alitumaini kwamba kwa kuruhusu maafa kumwangukia Ayubu angeweza kutoa kutoka kwa Ayubu laana ambayo alikuwa amerithi kutoka kwa Adamu. Baada ya Ayubu kupoteza kila kitu, pamoja na watoto wake, laana ilitoka katika midomo ya mke wa Ayubu:

> Ndipo mkewe akamwambia, "Je! Wewe hata sasa washikamana na utimilifu wako? Umkufuru Mungu, ukafe." — Ayubu 2:9

Akizungumzia hali ya mwanadamu, Paulo anaiweka wazi:

> Kama ilivyoandikwa: "Hakuna mwenye haki, hata mmoja; hakuna aelewaye; hakuna amtafutaye Mungu. Wote wamekengeuka, wamepotea pamoja; hakuna atendaye mema, hata mmoja." "Makoo yao ni makaburi wazi; ndimi zao hutenda hila." "Sumu ya nyoka-nyoka iko kwenye midomo yao." **"Vinywa vyao vimejaa laana na uchungu."** — Warumi 3:10-14. (NIV)

Mungu alijua kwamba laana na uchungu moyoni mwa Adamu ungedhihirika katika mbegu alizozipanda; Iwe kwamba zilikuwa mbegu za maneno yake, mbegu za uzazi wake, au mbegu za ulimwengu wa mimea. Haya yote yangedhihirisha laana moyoni mwake kwa Mungu. Kwa upendo, Mungu alimpa Adamu wakati wa kuona matokeo ya mbegu iliyokuwa ndani yake. Ili kumpa Adamu wakati huu, Roho wa Mungu alipaswa kukaa

na Adamu na kuvumilia laana na uchungu wake wa kila siku ili kumweka hai kwa muda wa kutosha kuelewa mbegu ndani yake.

Adamu alipanda mbegu ndani ya mkewe, ambaye alifanywa kwa ubavu kutoka kwake mwenyewe, aliyeumbwa kwa ardhi. Kutokea kwenye hii "dunia mama" alitoka Kaini kwa mfano wa baba yake Adamu na mama yake Hawa. Adamu alipojitetea kwa kumwambia Mungu kwamba mwanamke aliyemfanya ndiye aliyesababisha tatizo hilo, Adamu alilaani mbingu na nchi. Ardhi ambayo Hawa aliumbwa kwayo ililaaniwa na Adamu. Mwanamke wa kidunia angekuza mbegu hiyo ya Adamu na matokeo yangeonekana.

Adamu alipotazama umbo lenye damu la mwanawe Abeli, alishuhudia kwa hofu matunda ya laana iliyokuwa ndani yake. Ndani yake Kaini ilikuzwa mbegu ya baba yake, ambaye alikuwa amemhukumu na kumlaani Mungu, na kujidhihirisha katika kuhukumu, kulaani, na kumuua ndugu yake Habili. Adamu sasa angeweza kuonja tunda la mbegu yake mwenyewe iliyopandwa.

Je, Adamu angeona katika tendo hili tunda lililokuzwa la uzao wake mwenyewe mwovu? Au angeendelea kuruhusu uovu huu ukue kwa kumhukumu na kumlaani Kaini kwa ajili ya uovu wake?

Kila kiumbe hai katika bustani kiliishi chini ya laana ya Adamu. Hapakuwa na mahali ambapo sauti yake haikusikika katika bustani. Kila alichofanya matokeo yake yangefika katika bustani nzima na maneno yake hadi ukingo wake. (tazama Zaburi 19:3,4). Chini ya ushawishi wa sauti ya Adamu, mawimbi ya sauti ambayo yalibebwa kutoka kwake yaligonga uumbaji maridadi ambao ulikusudiwa kupokea sauti ya baraka.

> Tazama, nimepokea amri ya kubariki, naye amebariki; nami siwezi kuligeuza. — Hesabu 23:20 (KJV)

Muda mrefu kabla ya Kaini kumhukumu na kumuua Abeli, Mungu alimfunulia Adamu mwonekano mwingine wa laana iliyokuwa ndani yake. Katika ishara ya laana juu ya mtini, Yesu aliwafundisha wanafunzi juu ya laana ya kujiamulia ambayo ilikuwa juu ya taifa la Kiyahudi ambayo ingepelekea kwenye uharibifu wao isipokuwa watubu. Kwa namna ileile ambayo Kristo alivyotumia laana juu ya mtini kufundisha somo, Mungu alitumia ishara ya mwana-kondoo aliyechinjwa ili kufunua laana ya

kujiamulia ambayo ilikuwa juu ya Adamu ambayo ingesababisha maangamivu yake asipotubu.

> Bwana Mungu akawafanyia Adamu na mkewe mavazi ya ngozi, akawavika. — Mwanzo 3:21 (KJV).

Ngozi hizi walizopewa Adamu na Hawa zilipatikana kwa gharama ya maisha ya mnyama asiye na hatia. Tunajifunza punde tu baada ya tukio hili kwamba Habili alileta wana-kondoo wa kundi lake ili kumtolea Bwana kama dhabihu. Habili alijifunza kuhusu mchakato wa kutoa dhabihu ya mwana-kondoo kutoka kwa baba yake. Mungu alimwonyesha Adamu kile alichokuwa akimfanyia Mwanawe katika kumfundisha kuchinja mwana-kondoo.

Mungu hakuhitaji sadaka hii ili kumpendeza; Mungu kwa rehema zake kwa Adamu alimuonyesha yaliyokuwa moyoni mwake. Hili lilimpa Adamu nafasi ya kutubu.

> Dhabihu na matoleo hukupendezwa nazo, Masikio yangu umeyazibua, Kafara na sadaka za dhambi hukuzitaka. — Zaburi 40:6

> Maana sikusema na baba zenu, wala sikuwaamuru kwa habari za sadaka za kuteketezwa na dhabihu, siku ile nilipowatoa katika nchi ya Misri; lakini naliwaamuru neno hili, nikisema, Sikilizeni sauti yangu, nami nitakuwa Mungu wenu nanyi mtakuwa watu wangu; mkaende katika njia ile yote nitakayowaamuru mpate kufanikiwa. — Yeremia 7:22-23

Mungu hakuhitaji sadaka hii ili kumpendeza; Mungu kwa rehema zake kwa Adamu alimuonyesha yaliyokuwa moyoni mwake.[22] Hili lilimpa Adamu nafasi ya kutubu. Katika mwana-kondoo aliyechinjwa, Adamu angeweza kuona matunda ya hukumu yake ya adhabu - ilisababisha kifo na mbaya zaidi, kifo cha asiye na hatia.

Mbegu iliyokuwa ndani ya moyo wa Adamu ilidhihirishwa katika kifo cha mwana-kondoo. Katika kifo cha mwana-kondoo kulikuwa na ufunuo wa nia iliyofichwa ya Adamu ya kumhukumu, kumlaani na kumuua Mwana wa Mungu.

[22] For more on this subject read Cross Examined and Cross Encountered available at fatheroflove.info

SURA YA 7

# Tazama Mtu Huyu

Akiwa na umbo lililotapakaa damu Mwana wa Mungu alipoonekana kwa watu baada ya kuchapwa viboko, kudhihakiwa, kupigwa na kunyanyaswa, Pilato aliwaita sio tu wale waliokusanyika Yerusalemu siku ile bali wanadamu wote: *tazama mtu huyu*. ( Yohana 19:5 ).

Tunapomwona Mwana wa thamani wa Mungu, akisimama kwa heshima mbele ya washtaki Wake walipokuwa wakipiga mayowe kwa ajili ya kifo Chake, tunajifunza asili ya kweli ya miili yetu. Katika Kristo Yesu, kujaribiwa kwake, hukumu yake, na kifo chake tunaona mbegu mbaya iliyopandwa ndani ya Adamu na Shetani ikidhihirishwa kikamilifu.

Kristo, kama Mwana wa Adamu, aliyezaliwa na mwanamke, (Wagalatia 4:4), aliyefanyika kwa udongo, alilaaniwa kwa ajili yetu ili tuweze kutambua asili ya uovu ulio ndani yetu. Kwa ujuzi huu Mungu anatamani kwamba tuweze kutubu dhambi zetu na kutokumwamini kwetu, na badala yake kuamini kwamba ana nia njema na sisi.

Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake (2 Wakorintho 5:19). Kama vile Mungu alivyomruhusu Adamu kuua mwana-kondoo asiye na hatia kama onyo la kile kilichokuwa ndani ya mwanadamu, vivyo hivyo Mungu alimtoa Mwanawe kwetu, ili tupate kujua hali yetu halisi na kuitubu.

Watu wanapokuja Msalabani katika hali yao ya kuanguka, wanaona na kuridhika kwa sababu ya kile wanachokichukulia kupitia giza kuwa haki ya kimungu na hukumu kwa ajili ya dhambi zao.

> BWANA ametawala, nchi na ishangilie; wacha mwambao wa mbali ufurahi. Mawingu na giza nene vinamzunguka; haki na hukumu ndio msingi wa kiti chake cha enzi. Moto hutangulia mbele zake na kuwateketeza adui zake kila upande. — Zaburi 97:1-3 ( NIV)

> Kristo alitukomboa katika laana **ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu** (maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti). — Wagalatia 3:13

Sheria ya Mungu ni chemchemi ya uzima kwa wenye hekima (Mithali 13:14), lakini sheria hii huleta laana juu ya wale waliojawa na laana na uchungu.

> Basi torati ni takatifu, na ile amri ni takatifu, na ya haki, na njema. Basi je! Ile iliyo njema ilikuwa mauti kwangu mimi? Hasha! Bali dhambi, ili ionekane kuwa ni dhambi hasa, ilifanya mauti ndani yangu kwa njia ya ile njema, kusudi kwa ile amri dhambi izidi kuwa mbaya mno. — Warumi 7:12-13

Adamu ndiye aliyeikubali sheria ya dhambi na mauti iliyodai hukumu na kifo kwa ajili ya kosa. Adamu katika kujidanganya kwake alimtupia sheria hii Mungu na kuamini kuwa ni sheria ya Mungu.

> Je! Kiti cha udhalimu kishirikiane nawe, Kitungacho madhara kwa njia ya sheria? — Zaburi 94:20

Mwanadamu wa asili huchukulia vitu vyote kupitia mtazamo wa Adamu wa hukumu na kifo. Kwa hiyo, Msalaba wa Kristo unatazamwa kama hukumu ya Mungu na hitaji la kifo lililowekwa juu ya Mwanawe kama mbadala wa makosa yetu. Mungu alikuwa tayari kukutana nasi katika mahali pa ufahamu wetu ili kutusadikisha juu ya rehema na msamaha wake wa milele, kwa matumaini kwamba tunaweza kutoka gizani na kuona kwamba sio yeye aliyetuhukumu, lakini badala yake tulijihukumu wenyewe kuwa tunastahili

kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Hili linathibitishwa na uhalisia wa hukumu zetu na matamanio ya adhabu kwa wengine.

Katika hukumu, adhabu, na kifo cha Yesu tunajifunza asili ya kweli ya miili yetu na laana ambayo kwa kawaida inakaa katika mfumo wetu wa kidunia. Hivi ndivyo wanadamu hutatua matatizo yao - kwa njia ya mateso, hukumu na adhabu.

Kama wanadamu wangejifunza kweli somo la Msalaba, ambalo lilionyesha upotovu wetu wa kweli wa kibinadamu, tungepitia historia tofauti kabisa katika miaka 2000 iliyopita. Badala yake, mbegu ya ukweli ambayo Kristo alidhihirisha miaka 2000 iliyopita imekusudiwa tena kukabili hukumu, adhabu na kifo kama sehemu ya kukataliwa kwa mwisho kwa Mwana wa Mungu katika watu wake na ujumbe Wake na wanadamu wengi sana.

Tutafuatilia baadhi ya vipimo vya mchakato huu wa hukumu; jinsi tunavyochukulia hii kama hukumu ya Mungu kwetu wakati kwa kweli ni hukumu yetu kwa wengine inayotupwa kwa Mungu.

Kama vile Mungu alivyomtoa Mwanawe ili atuonyeshe jinsi tulivyo katika kisa cha Msalaba, Mungu vivyo hivyo yuko tayari kuacha sifa yake ichukuliwe vibaya kama hakimu anayehukumu ili tujione jinsi tulivyo kwa matumaini kwamba katika mchakato huu tupate tutubu mawazo yetu ya upotovu dhidi kwake.

## SURA YA 8

# Kumhukumu Baba

> Akasema, Mtu mmoja alikuwa na wana wawili; yule mdogo akamwambia babaye, Baba, nipe sehemu ya mali inayoniangukia. Akawagawia vitu vyake. Hata baada ya siku si nyingi, yule mdogo akakusanya vyote, akasafiri kwenda nchi ya mbali; akatapanya mali zake huko kwa maisha ya uasherati. — Luka 15:11-13

Kilichompata baba katika mfano wa Mwana Mpotevu ni uzoefu wa wazazi wengi. Katika mwingiliano na wenzao, watoto huanza kuona wazazi wao katika mtazamo tofauti.

Shauku ya kuwaokoa watoto wetu kutokana na hatari nyingi inafasiriwa kuwa kizuizi na udhibiti. Ni kweli kwamba wazazi wengi huwadhibiti watoto wao kupita kiasi, lakini haikuwa hivyo katika simulizi ambayo Yesu alisimulia.

Kwa kijana kuomba urithi wake mapema na kutaka kuondoka katika uangalizi wa baba yake hufunua hukumu ya kijana dhidi ya baba yake. Ombi la urithi linasema, "Siwezi kungoja ufe, nipe kilicho changu sasa."

Katika kisa hiki baba halipi kisasi au kumlaani mwana. Kinasema kwamba aliwagawia, wanawe wawili, riziki yake. Neno katika Kigiriki ni bios, maana yake uhai. Moyo wa baba ungevunjwa na ukweli wa kusikitisha kwamba mtoto wake mdogo alitaka kumwacha. Baba aliwapenda sana watoto wake na hili lilimuuma sana kujua mtoto wake alitaka kuondoka nyumbani, hasa

kwa vile ajuavyo kwamba mwanae bado hajakomaa na angeteseka sana peke yake. Kwa gharama kubwa juu yake mwenyewe, baba anampa mwanawe kile anachokitaka.

Mwana haonyeshi shukrani yoyote kwa zawadi hii na hivyo hathamini kile anachokipewa. Kwa hiyo anatumia pesa kwa uhuru kwa maana hathamini gharama zake. Hili limeuponda moyo wa baba kumpa mwanawe zawadi hii na bado mwana huyo hakuithamini hata kidogo.

Baada ya muda fulani, mwana huyo anapoteza urithi aliopewa na kuanza kuteseka kwa matokeo ya maamuzi yake mabaya. Mambo yalipozidi kuwa mabaya, alianza kufikiria nyumbani.

> Alipozingatia moyoni mwake, alisema, Ni watumishi wangapi wa baba yangu wanaokula chakula na kusaza, na mimi hapa ninakufa kwa njaa. Nitaondoka, nitakwenda kwa baba yangu na kumwambia, Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena; nifanye kama mmoja wa watumishi wako. — Luka 15:17-19

Tunapata ufahamu kutoka kwenye fikra za mwana. Haamini kwamba anaweza kuhusiana na baba yake kama mwana, lakini lazima ahusiane naye kama mtumishi au mtumwa. Wakati mwana alipokuwa akiishi nyumbani na kufanya kazi kwa baba, alikuwa akimchukulia baba yake kama bwana wa watumwa. Alihisi kwamba baba yake alikuwa akitafuta kumdhibiti na kuzuia uhuru wake, kwa hiyo alitaka kuondoka.

Mwana anaporudi nyumbani, anadhihirisha mawazo yake kwa baba yake. Hakuna mawazo ya msamaha katika akili yake. Anawazia tu adhabu kwa ajili ya dhambi yake. Yeye ndiye anayetoa hukumu na wakati huu ni juu yake mwenyewe. Anakubali kwamba hawezi kuishi bila baba yake, lakini anaamini kwamba lazima sasa aadhibiwe kulingana na matendo yake mabaya. Ingawa hali yake imebadilika, mtazamo wake kwa baba yake unabaki kama vile alivyokuwa hapo awali. Bado anamwona baba yake kama bwana mtumwa.

> Akaondoka, akaenda kwa babaye. Alipokuwa angali mbali, baba yake alimwona, akamwonea huruma, akaenda mbio akamwangukia shingoni, akambusu sana. — Luka 15:20

Hukumu ya mtoto kwa baba yake ilikuwa ya uongo kabisa. Baba alikuwa akikesha na kumwombea mwanawe kila siku. Alitamani arudi. Hakumhukumu mwanawe kwa kile alichokifanya. Alimsamehe kwa hiari kwa sababu ya upendo wake mkubwa kwa mtoto wake mpendwa.

Je, unaweza kumwazia mtu mzima tena mzee akimkimbilia mwanawe huku machozi ya furaha yakimtoka? Anamkumbatia na kumbusu mwanawe mpendwa. Hakuna hasira, hakuna hukumu wala hakuna lawama; kuna upendo tu. Je! Mwana anaitikia vipi vitendo hivi vya baba?

> Yule mwana akamwambia, Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena. — Luka 15:21

> Baba yetu aliye mbinguni hajawahi kukuhukumu. Amekupa maisha yake ili uweze kuyafanya upendavyo. Hajawahi kukuhukumu kwa hili.

Ikiwa atakubali kutulia kikamilifu katika mikono ya baba yake na kukubali msamaha wake, atanguka chini na kulia kama baba yake na kuanza kukiri maumivu makubwa ambayo amemsababishia. Kiburi chake bado hakimruhusu kukubali matendo ya baba yake. Badala yake, anatoa hotuba aliyoifanyia mazoezi kabla. Anatamani kuingia katika uhusiano wa bwana/mtumishi. Anatamani kumridhisha baba yake katika kulipia deni kubwa alilokuwa nalo na kuishi kama mtumwa. Kwa wakati huu haukubali upendo wa kusamehe wa baba.

> Lakini baba aliwaambia watumwa wake, Leteni upesi vazi lililo bora, mkamvike; mtieni na pete kidoleni, na viatu miguuni; mleteni ndama yule aliyenona mkamchinje; nasi tule na kufurahi; kwa kuwa huyu mwanangu alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana. Wakaanza kushangilia. — Luka 15:22-24

Baba anaendelea kummiminia mtoto wake upendo na mahaba, huku mwana akiendelea kuhusiana na baba yake kwa njia ambayo angejitendea

mwenyewe ikiwa angekuwa mahali pa baba yake. Mfumo wake wa hukumu sasa unamjia mwenyewe, na bado hawezi kukumbatia upendo wa kusamehe wa baba yake.

Hapa ndipo hadithi ya kijana mdogo inaishia. Tunamwona akiwa amekaa kwenye meza ya baba yake akiwa amevalia vazi zuri huku sherehe kubwa ikifanyika. Uamuzi wa mwisho wa mwana umeachwa kwako, msomaji. Je, utakubali matendo ya upendo ya baba yako kwako, au utabaki kuwa mtumwa kwa siri moyoni mwako? Baba yetu aliye mbinguni hajawahi kukuhukumu. Amekupa maisha yake ili uweze kuyafanya upendavyo. Hajawahi kukuhukumu kwa hili. Je, unamwona kuwa bwana mtumwa? Je, unahisi kumbatio Lake la uchangamfu unaporudi Kwake ukikiri kwamba huwezi kuishi bila Yeye? Je, utakubali uwana au ubinti wako kwa Baba yako?

> Lakini nasema ya kuwa mrithi, wakati wote awapo mtoto, hana tofauti na mtumwa, angawa ni bwana wa yote; bali yu chini ya mawakili na watunzaji, hata wakati uliokwisha kuamriwa na baba. Kadhalika na sisi, tulipokuwa watoto, tulikuwa tukitumikishwa na kawaida za kwanza za dunia. Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye amezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria, kusudi awakomboe hao waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana. Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba. Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu. — Wagalatia 4:1-7

Kijana mkubwa anaonekana kuwa na masuala yahusuyo hukumu yanayofanana na ya kijana mdogo. Ona jinsi mfumo ule ule wa haki ulivyo kwa kijana mkubwa, lakini unajidhihirisha kwa njia tofauti kwa sababu ya nafasi tofauti aliyokuwa nayo kuhusiana na baba yake.

> Basi, yule mwanawe mkubwa alikuwako shamba na alipokuwa akija na kuikaribia nyumba, alisikia sauti ya nyimbo na machezo. Akaita mtumishi mmoja, akamwuliza, Mambo haya, maana yake nini? Akamwambia, Ndugu yako amekuja, na baba yako amemchinja ndama aliyenona, kwa sababu amempata tena, yu

> mzima. Akakasirika, akakataa kuingia ndani. Basi babaye alitoka nje, akamsihi. Akamjibu baba yake, akasema, Tazama, mimi nimekutumikia miaka mingapi hii, wala sijakosa amri yako wakati wo wote, lakini hujanipa mimi mwana-mbuzi, nifanye furaha na rafiki zangu; lakini, alipokuja huyu mwana wako aliyekula vitu vyako pamoja na makahaba, umemchinjia yeye ndama aliyenona. Akamwambia, Mwanangu, wewe u pamoja nami sikuzote, na vyote nilivyo navyo ni vyako. Tena, kufanya furaha na shangwe ilipasa, kwa kuwa huyu ndugu yako alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana. — Luka 15:25-32

Kijana mkubwa pia alimhukumu Baba kuwa mkatili na asiye na haki. Alimtumikia Baba yake kama mtumwa na si kama mwana. Baba alipoonyesha upendo mwingi kwa mwanawe mdogo, kijana mkubwa alimhukumu kuwa mfujaji na asiye na hekima. Mwana mkubwa anawakilisha sehemu kubwa ya kanisa la Kikristo linalomtumikia Mungu kama mtumwa likitumaini kupata thawabu kwa ajili ya jitihada zao. Wanawadharau wale wanaoingia duniani na kuharibu maisha yao kwa makahaba na uovu. Wanapata faraja katika kuwahukumu walio duniani; wanatofautisha maisha yao mema na walio nje na hawatawachukulia kwa upendo na kuwasamehe kwa maisha yao ya kidunia. Nani alikuwa amepotea zaidi; kijana mdogo au mkubwa? Kijana mdogo alijua amepotea lakini mkubwa hakujua.

Katika visa vyote viwili vijana walimhukumu Baba kama bwana mtumwa. Katika hali zote mbili wana hawakuona mahali popote pa rehema. Baba aliwasihi wana wote wawili wakubali upendo wake na kuridhika na upendo huo. Wana wote wawili walihitaji ufunuo wa kweli wa tabia ya Baba ili kupindua mitazamo yao ya kuhukumu na ya kulaani ambayo walikuwa wamepokea kutoka kwa Adamu.

SURA YA 9

# Ufunuo wa Baba

Kama tulivyosema hapo awali, Warumi 5:16 inatuambia kwamba hukumu inayopelekea adhabu ilitoka kwa Adamu. Kwa hiyo, tunaona kwamba kifo kilikuja ulimwenguni kwa njia ya mtu mmoja.

> Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi; — Warumi 5:12

Dhambi ambayo Adamu aliifanya ilikuwa ni kutoa hukumu ya adhabu. Hili halipatani kabisa na tabia ya Mungu. Hukumu ya adhabu huwapelekea watu kutoa hukumu ya kifo kwa wengine. Hivi ndivyo kifo kilikuja ulimwenguni.

> Ndugu, msisingiziane; amsingiziaye ndugu yake, au kumhukumu ndugu yake, huisingizia sheria na kuihukumu sheria. Lakini ukiihukumu sheria, huwi mtenda sheria, bali umekuwa hakimu. — Yakobo 4:11

Katika hali hii ya akili iliyoanguka, wanadamu huelekeza sifa hizi kwa Mungu na kumwona Yeye isivyo sahihi.

> Ndivyo ulivyofanya, nami nikanyamaza; **Ukadhani ya kuwa Mimi ni kama wewe.** Walakini nitakukemea; Nitayapanga hayo mbele ya macho yako. — Zaburi 50:21

Ili kurekebisha mitazamo isiyo ya kweli ya wanadamu kumhusu Mungu, Baba yetu wa mbinguni alimtuma Mwanawe ulimwenguni ili kutuonyesha jinsi Baba alivyo. Yesu anatuambia kusudi la utume wake.

> **Mimi nimekutukuza duniani**, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye. — Yohana 17:4

Yesu alimtukuza Baba, kumaanisha kwamba alifunua tabia yake halisi alipokuwa duniani. Alipokuwa akizungumza na mmoja wa wanafunzi Wake alisema:

> .....Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? **Aliyeniona mimi amemwona Baba**; basi wewe wasemaje, Utuonyeshe Baba? — Yohana 14:9

Yesu alisema kwamba kile ambacho Filipo alikuwa amekiona kwake ndivyo Baba alivyokuwa. Ili wanadamu wapatanishwe na Mungu ni lazima wamjue jinsi alivyo. Bila ufunuo wa Yesu kwa ulimwengu hatungeweza kamwe kumjua Mungu, na badala yake tungemwazia kuwa mwenye kuhukumu na kuadhibu kama sisi.

> Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. **Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu**, bali ulimwengu uokolewe katika yeye. — Yohana 3:16-17

Mungu hakumtuma Yesu katika ulimwengu huu ili kuuhukumu kwa sababu Mungu hamhukumu mtu yeyote. Alimtuma Mwanawe ili kutuonyesha jinsi alivyo na kwa hiyo atuokoe kutokana na mitazamo yetu ya kuhukumu kupitia maarifa haya juu yake.

> Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu. — Yohana 3:18

Sababu inayowafanya wale wanaoliamini jina au tabia ya Yesu wasihukumiwe ni kwa sababu unapomjua Yesu, ambaye hajawahi

kuhukumu au kumwadhibu mtu yeyote, unajua pia kwamba Mungu hahukumu au kuadhibu. Wale wasiomwamini Yesu hawawezi kuuona ukweli kwamba Mungu hamhukumu mtu yeyote, na hivyo urithi tunaopokea sisi sote kutoka kwa Adamu unawafanya wale wasioamini kuwahukumu wengine na kuamini kwa uongo kwamba Mungu huwahukumu wenye dhambi kwa ajili ya dhambi zao. .

Ni lazima uamini katika tabia ya Yesu kama mtu ambaye hahukumu ili uamini kwamba wewe hujahukumiwa na Mungu. Ukweli huu pekee unaweza kutuweka huru kutokana na roho ya hukumu inayosumbua maisha yetu.

Wengi hufundisha kwamba Yesu alikuja kufa Msalabani na wale wasiokubali Msalaba watahukumiwa na Mungu na kuangamizwa kuzimu. Ikiwa hii ilikuwa kweli, basi lazima isemwe kwamba Mungu alimtuma Mwanawe ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu. Ikiwa Mungu angemhukumu hata mtu mmoja kwa kuukataa Msalaba, basi matokeo ya Msalaba ni kusababisha hukumu kutoka kwa Mungu.

> Mimi nimekutukuza duniani, hali **nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye**. — Yohana 17:4

Je, inawezekanaje kwamba Yesu angeweza kumaliza kazi ambayo Mungu alimpa kuifanya usiku kabla ya kufa kwake Msalabani?

> Yesu akawaambia wakuu wa makuhani, na maakida wa hekalu, na wazee, waliokuja juu yake, Je! "Mmekuja wenye panga na marungu kama kukamata mnyang'anyi? Kila siku nilipokuwa pamoja nanyi hekaluni hamkuninyoshea mikono, **lakini hii ndiyo saa yenu, na mamlaka ya giza.**" — Luka 22:52-53

Kusulubishwa kwa Yesu ilikuwa ni kazi ya giza. Ilikuwa ni utimilifu wa tamaa ya Shetani tangu mwanzo, pamoja na udhihirisho wa kile ambacho Adamu alikihisi dhidi ya Mwana wa Mungu kutokana na kuanguka kwake katika dhambi.

Msalaba wa Kristo unaonyesha kwa wanadamu kile kilicho ndani ya mioyo yetu; unadhihirisha chuki yetu ya asili tusiyoifahamu dhidi ya Mungu

(Warumi 8:7). Katika kuruhusu jamii ya wanadamu kumuua Mwanawe, Mungu alituleta tukutane uso kwa uso na uovu uliomo ndani yetu kwa sababu ya urithi wetu wa hukumu kutoka kwa Adamu.

Ni Upendo usioeleweka wake Mungu kuruhusu jamii yetu kufanya hivi kwa Mwanawe. La kushangaza zaidi ni kwamba baada ya sisi kufanya hivi, bado hakutuhukumu. Maneno ya Yesu Msalabani ndiyo matamanio hasa ya Mungu mwenyewe:

> Kisha Yesu akasema, "Baba, uwasamehe, kwa maana hawajui watendalo."— Luka 23:34

> …Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao,… — 2 Wakorintho 5:19

Msalaba unatuonyesha kwamba Mungu alikuwa tayari kutusamehe hata baada ya sisi kumuua Mwana wake. Kristo alifunua kwa ulimwengu wote kwamba Mungu bado alikataa kutuhukumu lakini akatupatia rehema yake bure.

> Kwa kukubali mwenyewe kuhukumiwa, kuadhibiwa, na kuuawa, Yesu alifunua yale yaliyokuwa mioyoni mwetu, sio kutuhukumu, lakini wakati wa kutambua hali yetu mbaya sana, ili kutupatia rehema na neema.

> Mmesikia kwamba imenenwa, Umpende jirani yako, na, Umchukie adui yako; lakini mimi nawaambia, **Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi, ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni;** maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki. — Mathayo 5:43-45

Baba yetu anawapenda wale wanaomwona kuwa adui; Anawabariki wale wanaomlaani. Yesu alionyesha hili waziwazi duniani. Yesu hakuwahukumu, hakuwalaumu, au kuwaua wale waliomkataa - badala yake alihukumiwa, kuadhibiwa, na kuuawa na watoto wa Adamu.

Kwa kukubali mwenyewe kuhukumiwa, kuadhibiwa, na kuuawa, Yesu alifunua yale yaliyokuwa mioyoni mwetu, sio kutuhukumu, lakini wakati wa kutambua hali yetu mbaya sana, ili kutupatia rehema na neema.

> Lakini sheria iliingia ili kosa lile liwe kubwa sana; na dhambi ilipozidi, neema ilikuwa nyingi zaidi; — Warumi 5:20

Sote tunajua kwamba Yesu hakuwa na hatia ya uhalifu aliotuhumiwa nao. Alikuwa chanzo cha furaha na baraka kwa wote waliomzunguka. Aliponya wagonjwa, alifufua wafu, akawabariki watoto na kuwaambia watu wote kuhusu upendo wa Baba yake kwao.

Aliwaonya wale waliokuwa karibu naye waliokuwa wakitembea katika dhambi na akawahimiza watubu. Alizungumza makemeo yake kwa upendo na huzuni kwa wale waliokataa kusikiliza.

Maisha yake makamilifu hutupatia kipimo pekee cha kweli cha jinsi Mungu alivyo. Tabia yake ndiyo inayotufafanulia ukweli na uongo. Bila kukubali ufunuo huu wa Baba, tutachanganyikiwa tunaposoma Maandiko kwa sababu ya mwelekeo wa kurithi wa kuelekeza hatia kwa Mungu.

Lawama ambazo Adamu aliweka juu ya Mungu alipoulizwa kwa nini alikula tunda la mti humkalia kila msomaji wa Biblia. Jinsi tunavyosoma visa vya Agano la Kale huathiriwa hasa na mwelekeo wetu wa asili wa kuhukumu na kulaani.

Ni maisha ya Yesu pekee yaliyodhihirishwa duniani ambayo yanaweza kutusaidia kusoma visa vya Agano la Kale kwa usahihi. Ikiwa hatufanyi hivi, tukiamua badala yake kukataa utukufu wa tabia ya Mungu kama inavyofunuliwa katika Mwanawe, tunaweka utaji juu ya macho yetu tunaposoma Maandiko.

> Basi, kwa kuwa mna taraja la namna hii, twatumia ujasiri mwingi; nasi si kama Musa alivyotia utaji juu ya uso wake, ili kwamba Waisraeli wasitazame sana mwisho wa ile iliyokuwa ikibatilika; ila fikira zao zilitiwa uzito. **Kwa maana hata leo hivi, wakati lisomwapo Agano la Kale, utaji uo huo wakaa; yaani, haikufunuliwa kwamba huondolewa katika Kristo**; ila hata

> leo, torati ya Musa isomwapo, utaji huikalia mioyo yao. **Lakini wakati wo wote watakapomgeukia Bwana, ule utaji huondolewa**. Basi "Bwana" ndiye Roho; walakini alipo Roho wa Bwana, hapo ndipo penye uhuru. **Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho.** — 2 Wakorintho 3:12-18

Wakati wowote unapotaka kujua jinsi Mungu ambavyo angetenda, soma vitabu vinne vya kwanza vya Agano Jipya vinavyozungumzia injili ya Yesu Kristo. Hivi ndivyo vipimo halisi vya kupimia tabia ya Mungu.

Yesu anatuonyesha jinsi ambavyo Baba hahukumu katika kisa cha wana wawili wapotevu. Wana ndio waliomhukumu baba. Lakini vipi kuhusu maandisho kama haya?

> Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu, nawe uzishike amri zake, Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu. **Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi,** pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya. — Mhubiri 12:13-14

> Basi, nawaambia, Kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, **watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu**. Kwa kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa. — Mathayo 12:36-37

> **Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo**, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya. — 2 Wakorintho 5:10

Ingekuwa jambo la kuleta ushawishi kusoma mistari hii na kuhitimisha kwamba Mungu atahukumu kila jambo tunalofanya, lakini je, tunapatanishaje wazo kama hilo na yale ambayo Yesu aliyaonyesha katika maisha yake na yale aliyotuambia?

> Tena Baba hamhukumu mtu ye yote, bali amempa Mwana hukumu yote; — Yohana 5:22

> Ninyi mwahukumu kwa kufuata mambo ya mwili; mimi[Yesu] simhukumu mtu. — Yohana 8:15

Ni hakika kwamba kutakuwa na hukumu. Ni kweli kwamba tutakabiliana na kila jambo ambalo tumewahi kulifanya. Swali ni nani atafanya hukumu? Je, inawezekana kwamba Mungu anaweza kuleta kila kitu katika mchakato wa hukumu bila kumhukumu yeyote?

Ndiyo, kwa hakika kutakuwa na hukumu, na Yesu anafunua kabisa jinsi hukumu hiyo itakavyotukia.

SURA YA 10

# Wala Sikuhukumu

Huu hapa ni ushauri rahisi zaidi wa kukuwezesha kupita hukumuni bila woga.

> Msihukumu, msije mkahukumiwa ninyi. Kwa kuwa hukumu ile mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa; na kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakachopimiwa. — Mathayo 7:1-2

Hapo awali nilikuwa nimesoma mstari huu kupitia ufahamu wangu wa Santa Claus. Ni bora ujiangalie maana Mungu anatunza orodha ya matendo yako yote na anakuja kukulipa. Kupitia mtazamo huu wa hukumu ambayo nilikuwa nimerithi kutoka kwa Adamu, niliona mstari huu ukisema kwamba Mungu atawahukumu na kuwadhibu wale wanaohukumu na kulaumu. Kuandika tu maneno hayo kunanifanya nishangae kwamba sikuweza kuona kutoendana kwa aina hii ya kufikiri.

Je, ingewezekanaje basi kwa Mungu kuhusika katika hukumu bila Yeye kumhukumu mtu yeyote? Hebu tutazame kisa kifuatacho:

> Lakini Yesu akaenda kwenye Mlima wa Mizeituni. Asubuhi na mapema Yesu alikwenda tena Hekaluni, na watu wote wakamwendea; naye akaketi na kuwafundisha. Kisha walimu wa Sheria na Mafarisayo wakamletea mwanamke aliyekamatwa akizini. Wakamweka katikati, wakamwambia, Mwalimu,

> mwanamke huyu amekamatwa akizini. Katika torati, Musa alituamuru watu kama hao wapigwe mawe. Lakini unasemaje?" — Yohana 8:1-5

Baadhi ya viongozi wa Kiyahudi walikuwa wamemleta mwanamke huyu kwa Yesu ili ahukumu kesi yake. Maneno yao yalionyesha kwamba tayari walikuwa wamemhukumu na kumlaani kwa uzinzi wake. Kumshika katika kitendo hicho kunaonyesha kuwa watu hawa walikuwa wamehusika katika kupanga kitendo hicho na mahali kitakapotokea. Hata hivyo, alikuwa amefanya uzinzi na kulingana na sheria hili lilikuwa kosa, na ilionekana wazi kutokana na maandiko ya Musa kwamba alistahili kifo.

> Nao wakasema neno hilo wakimjaribu, ili wapate sababu ya kumshitaki. Lakini Yesu akainama, akaandika kwa kidole chake katika nchi. Nao walipozidi kumhoji, alijiinua, akawaambia, "Yeye asiye na dhambi miongoni mwenu na awe wa kwanza wa kumtupia jiwe." — Yohana 8:6-7

Watu hawa wajanja walikuwa wakitafuta kumnasa Yesu kati ya sheria za Musa na sheria za Kaisari. Kwa vyovyote vile Yesu hasemi neno kwao. Huenda angefichua njama yao mbaya na kufichua matendo yao yote maovu na kuwahukumu kifo kwa ajili ya mambo waliyofanya, lakini Yesu hasemi chochote. Badala yake, Anaandika ardhini. Watu walimshinikiza Yesu kujibu, na hatimaye anawaambia kwamba yeyote asiye na dhambi yuko katika nafasi ya kwanza kumtupia jiwe mwanamke huyo.

Kama Mwana wa Mungu, aliyejaa uungu wa Baba Yake, aliweza kusoma siri za maisha ya watu hawa. Alionyesha uwezo wake wa kufanya hivi mahali pengine.

> Yesu akamwambia, Nenda ukamwite mumeo, uje hapa. Mwanamke akajibu, akasema, Sina mume. Yesu akamwambia, "Umesema vema, 'Sina mume,' kwa maana umekuwa na waume watano, na uliye naye sasa si mume wako; kwa hilo umesema kweli." — Yohana 4:16-18

Yesu hakumhukumu kwa sababu ya mwenendo wake wa kuwa na waume watano na kuishi nje ya ndoa na wa sita. Alimjulisha tu kwamba Alijua

kuhusu historia ya maisha yake. Vivyo hivyo Yesu aliandika ardhini; Alifunua kwamba alijua historia ya maisha ya watu hawa lakini tena Hakuwahukumu au kuwalaani. Kama vile Yesu alivyomwuliza yule mwanamke mahali ambapo mume wake alipokuwa, akijua kwamba hakuwa katika uhusiano wa ndoa, vivyo hivyo alijua kwamba watu hawa ambao walikuwa wamemleta mwanamke huyu kwajili ya hukumu walikuwa na dhambi. Alikuwa akiwapa nafasi ya kutubu, na bado alikataa kuwahukumu.

> Akainama tena, akaandika kwa kidole chake katika nchi. Nao waliposikia, **wakashitakiwa na dhamiri zao, wakatoka mmoja mmoja, wakianzia tangu wazee hata wa mwisho wao**; akabaki Yesu peke yake, na yule mwanamke amesimama katikati. — Yohana 8:8-9

Mambo ambayo Yesu aliandika kwenye mchanga yaliwafanya watu hao wasadiki. Haya hayakuwa maneno ya shutuma au hukumu, bali ni kuwakumbusha mambo ya zamani ili apate kuwaponya. Yesu alifunua kwamba alijua umri wao kwa ukweli kwamba waliondoka kwa mpangilio wa umri wao. Watu hawa waliletwa hukumuni kwa nia yao ya kumhukumu Yesu na yule mwanamke. Ni ukumbusho wa kile kilichotokea kwenye bustani hapo mwanzo. Hawa alikuwa ametoa moyo wake kwa Lusifa na kupokea mbegu zake katika kuukubali uongo wake, hivyo kufanya uzinzi wa kiroho. Adamu alimhukumu na kumlaani Mwana wa Mungu kupitia mwanamke ili kuhalalisha makosa yake mwenyewe. Ni kwa njia ya hukumu ya Adamu mwenyewe kwamba alileta hukumu juu yake mwenyewe. Kisa katika Yohana sura ya 8 ni fumbo katika maisha halisi ya kile kilichotokea hapo mwanzo.

Watu hawa waliomleta yule mwanamke waliamua wakati wa hukumu kwa sababu walimwendea Yesu wakiwa na yule mwanamke na kumtupa miguuni pake. Yesu hakuwa amewaita watu hao ili kuwahukumu. Walimwendea kumhukumu Yeye na yule mwanamke.

Hivi ndivyo Baba aletavyo kila kitu hukumuni; Anaturuhusu kupokea matokeo ya uchaguzi wetu wenyewe. Ikiwa tunataka kuhukumu, hali za maisha zitatokea kwa namna ambayo tutajihukumu wenyewe kwa njia sawa na kwa nguvu sawa na jinsi tulivyowahukumu wengine.

Watu hawa walisadikishwa na dhamiri zao wenyewe na wakajihukumu wenyewe kwa kwenda mbali na Yesu. Hawakuomba rehema kutoka Kwake kwa sababu hawakuwa wamemwonea huruma yeye wala mwanamke. Kama vile walivyohukumu dhambi za wengine, ndivyo walivyohukumu dhambi zao wenyewe, na kwenda mbali na Nuru ya ulimwengu wakiwa hawajasamehewa.

Yesu hakuwahukumu au kuwashutumu. Kwa kuja mbele za Yeye ambaye alikuwa pamoja nao maisha yao yote kwa Roho Wake, walikutana uso kwa uso na rekodi yao ya maisha. Walipoona maandishi hayo katika nuru ya kuwapo kwa Kristo, walijihukumu wenyewe na kwenda mbali na kuwapo Kwake ili waweze kusahau yale waliyokuwa wamekumbushwa, badala yake wakachagua kuzama tena gizani.

> Kwa maana kila mtu atendaye mabaya huichukia nuru, wala haji kwenye nuru, matendo yake yasije yakakemewa. — Yohana 3:20 (KJV)

Wakati haya yote yanafanyika, maskini mwanamke asiyejiweza amesikia maneno kwamba wale wasio na dhambi wampige mawe. Alishawishiwa kufikiri kwamba maneno ya Yesu yalikuwa hukumu ya kifo. Alipokumbuka mambo yote aliyoyafanya, ilionekana kwamba sasa maisha yake yangefikia kikomo.

> Yesu akajiinua asimwone mtu ila yule mwanamke, akamwambia, Mama, wako wapi wale washitaki wako? Hakuna aliyekuhukumu?” Akasema, “Hakuna, Bwana.” Yesu akamwambia, “Wala mimi sikuhukumu; enenda zako na usitende dhambi tena.” — Yohana 8:10-11

Katika kumuuliza mwanamke yule washitaki wake walikuwa wapi, Yesu alikuwa akimwambia mwanamke huyo ahukumu mwenyewe hali hiyo. Je, angepiga kelele kwa hasira yake dhidu ya watu waliokuwa wamemnasa na kumtumia kumnasa Yesu? Katika kuwahukumu wale waliokuwa wamemzunguka, angejihukumu kuwa aliyelaaniwa na asiyekuwa na tumaini.

Alipotazama huku na huku na kuona hakuna hata mmoja wa viongozi wa kanisa pale, kisha akatazama usoni pa Yesu, akapata ujasiri. Imani iliijaza nafsi yake alipoutazama uso mzuri wa Mwokozi wake. Akamuuliza, "Je, hakuna yeyote aliyekuhukumu?" Swali linakwenda moyoni; sasa lazima ahukumu kesi yake mwenyewe. Matukio ya mwonekano wake wa zamani mbele yake, giza la maisha yake linatafuta kumshusha katika huzuni tena, lakini upendo katika uso huo na upole wa tabasamu Lake huleta hukumu yake juu yake mwenyewe. "Hakuna mtu Bwana."

Jinsi alivyohukumu kesi yake mwenyewe, ndiyo iliyokuwa hukumu aliyopewa na Yesu. Alisema, "wala mimi sikuhukumu." Alitafakari tena hukumu ileile ambayo alikuwa ametoa kuhusu kesi yake. Hivi ndivyo Mungu anatuleta hukumuni. Hivi ndivyo tutakavyotoa hesabu kwa kila neno tulilolinena.

Sababu inayotulazimu kuja mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo ni kwamba Adamu na wanawe waliamua kwamba lazima kuwe na hukumu hiyo kwa kuhukumu na kushutumu tabia ya Mungu kuwa kinyume na jinsi ilivyo. Kristo hakatai kushiriki katika hukumu hii, lakini anafanya kazi kwa njia ambayo kila mtu ataamua kesi yake mwenyewe.

> Usipoangalia maandiko yahusuyo hukumu katika Biblia kupitia maisha ya Yesu, basi mwangaza wa utukufu wa Baba utakuwa na utaji wa giza juu yake unaposoma Maandiko.

> Maana, watu wa mataifa wasio na sheria watakapoweza kufanya yaliyo ya sheria kwa asili, hao wasio na sheria ni sheria kwao wenyewe. waionyeshao kazi ya torati iliyoandikwa mioyoni mwao, **dhamiri ikishuhudia pamoja nao, na mawazo kati ya mtu na mwenzake, ikishitakiana au kuwatetea, katika siku ile Mungu atakapozihukumu siri za wanadamu, sawasawa na Injili yangu kwa Yesu Kristo.** — Warumi 2:14-16 (YLT)

Hii ni habari njema sana ikiwa tunaamini mambo mawili.

1. Tunaamini kwamba Mungu anatupenda na anatusamehe.
2. Tunaamini Yesu duniani anafunua ufunuo mzima wa tabia ya Baba.

Usipoangalia maandiko yahusuyo hukumu katika Biblia kupitia maisha ya Yesu, basi mwangaza wa utukufu wa Baba utakuwa na utaji wa giza juu yake unaposoma Maandiko.

Swali linaloibuka kutokana na kisa hiki ni je Yesu anazijuaje dhambi za wale watu waliokuja kwa ajili ya hukumu? Je, hiyo haimaanishi kuwa anatunza kumbukumbu? Je, Biblia haisemi kuhusu vitabu katika hukumu na kwamba ni lazima tutoe hesabu kwa kila neno tunalosema? Basi je, hiyo haimaanishi kwamba Mungu ameyaandika yote ili yatumike katika hukumu?

SURA YA 11

# Sheria ni ya Rohoni

Katika sura ya pili ya kitabu hiki tulichunguza athari za matumizi ya ufuatiliaji na tishio la kutumia nguvu ili kutunza sheria na utaratibu katika jamii. Katika mazingira hayo sheria inawekwa kwa raia wake. Wanashika sheria si kwa sababu wameshawishiwa kuhusu wema wake, bali kwa sababu wanaogopa adhabu ambazo zingetolewa na chombo chenye nguvu kwa kuiasi.

Ninataka kurejea kifungu cha Biblia tulichokuwa tumekitambulisha hapo awali, kisha nitembee katika mchakato wa kupatanisha hili na kauli za Kristo.

> Nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa, na **mmoja aliye mzee wa siku ameketi**; mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa chake kama sufu safi; kiti chake cha enzi kilikuwa miali ya moto, na gurudumu zake moto uwakao. Mto kama wa moto ukatoka ukapita mbele zake; maelfu elfu wakamtumikia, na elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele zake; **hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa**. — Danieli 7:9-10

Mandhari ya eneo la mahakama yenye vitabu vya ushahidi vinavyotolewa inafahamika sana kwetu. Ikiwa eneo hili la mahakama ya mbinguni kwa hakika ni Mzee wa Siku, i.e. Mungu Baba, akipitia mchakato wa hukumu

ambayo huamua ni nani anayeishi na nani anayekufa kwa kushindwa kutii sheria yake, basi maneno yafuatayo ya Kristo lazima yachukuliwe kuwa ya uongo.

> Kwa maana Baba hamhukumu mtu yeyote… — Yohana 5:22

Hapa lazima tutambulishe kiungo muhimu ambacho kimekosekana hadi sasa kuhusiana na sheria kutoka kwenye mtazamo wa mbinguni.

> Kwa maana twajua ya kuwa **torati asili yake ni ya rohoni**; bali mimi ni mtu wa mwilini, nimeuzwa chini ya dhambi. — Warumi 7:14

Sheria ya Mungu ni kitu ambacho kinahusiana na roho ya mtu. Sheria ya Mungu kwa asili ni ya mahusiano. Ni sheria inayokuambia matokeo ya Roho wa Mungu kukaa ndani yako kuliko kukuambia hivi ndivyo unavyopaswa kufanya ili kumpendeza Mungu.

> **Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru**, na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake. — Yakobo 1:25

Sheria inayotumika kulazimisha utii si sheria ya uhuru bali ni sheria ya kulazimisha. Sheria ya Mungu ni unabii wa kile kinachotokea kwa wale wanaompenda Mungu na kujazwa na maisha yake.

> Hili ndilo agano nitakalofanya na wana wa Israeli baada ya wakati huo, asema Bwana. Nitaweka sheria zangu katika nia zao na kuziandika katika mioyo yao. Nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. — Waebrania 8:10 ( NIV)

Je, unaandikaje sheria kwenye moyo wa mtu? Hii inaweza kufanyika tu kupitia uhusiano binafsi. Mtu anapomjua Mungu na kuanza kumpenda na kumwomba Roho wake, Roho huanza kubadilisha moyo wa mtu huyo na sheria ya Mungu huanza kufanya kazi ndani yetu moja kwa moja. Hii ndiyo njia pekee ya sheria kutoa uhuru.

Kwa nini basi wanadamu wanaelewa sheria inayowekwa kwa mabavu na kwamba tutaadhibiwa na Mungu ikiwa tutaivunja?

> Kwa maana dhambi, kwa kupata nafasi kwa ile amri, ilinidanganya, na kwa hiyo ikaniua. — Warumi 7:11

Je, dhambi ilitudanganyaje kwa njia ya sheria? Dhambi yenyewe si mtu anayetudanganya, bali dhambi ilianzishwa na Shetani na kupitia dhambi Shetani alibadilisha jinsi wanadamu wanavyoitazama sheria. Alifanyaje hili?

> Nyoka akamwambia mwanamke, "Hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya." — Mwanzo 3:4-5

Shetani aliwasadikisha Adamu na Hawa kwamba maisha yao hayakumtegemea Mungu. Aliwasadikisha kwamba uhai wao ulikuwa wa asili na kwamba walikuwa na hali ya kutokufa. Hata kama wangelikula matunda ya mti huu, wasingelikufa kamwe. Ikiwa kile Shetani alichokisema kilikuwa kweli, basi amri zozote zinazotolewa na Mungu zingeonekana zisizokuwa na maana na zenye kudhibiti. Iwapo sisi wanadamu tungeweza kuwepo bila kuhitaji kumtegemea Mungu, basi harakati zozote za upande Wake za kutuelekeza au kutuongoza zingeweza kuchukuliwa kuwa ni kutumia nguvu.[23]

Kupitia uongo huu ambao Shetani aliusema, aliweza kubadilisha mtazamo wetu wa sheria ya Mungu kutoka kwenye sheria ya baraka na uhuru hadi sheria ya udhibiti na udhalimu. Sisi kama jamii tulianza kuiona sheria kama orodha ambayo Mungu aliweka juu yetu sisi, na kwamba atatupima kwa sheria hii ili kuamua kama atatuweka hai au la.

Mtazamo huu mbaya wa sheria ndio unaoleta hitaji la uangalizi, hukumu na adhabu mara moja. Tunajikumbusha kwamba Paulo anatuambia kwamba aina hii ya hukumu ya adhabu ilitoka kwa Adamu na sio kutoka kwa Kristo au Baba yake (Warumi 5:16).

Kwa hiyo, msingi wa ufalme wa Shetani ni uongo kwamba mwanadamu hawezi kufa, au moja kwa moja zaidi, kwamba nafsi yake haiwezi kufa. Inalifanya neno la Mungu, kwamba tunaweza kufa ikiwa tunajitenga na Yeye

[23] For more on this subject see the book Life Matters available at fatheroflove.info

kupitia kutotii, uongo; hutulazimisha tuingie mahali ambapo njia pekee ya kufa ni kupitia Mungu kutuua moja kwa moja. Hii ndiyo kanuni kuu ambayo hutoka kwenye ufuatiliaji, hukumu, na adhabu. Ni kwa njia ya uongo huu kwamba Shetani alitenda upotovu kwa sheria ya Mungu na kuanzisha kiti cha uovu.

> Je! Kiti cha uovu, ambacho hupanga uovu [upotovu - KJV] kwa sheria, kitashirikiana nawe? — Zaburi 94:20

Ikiwa sheria basi ni ya rohoni na ni udhihirisho wa jinsi mahusiano hai yanavyofanya kazi, basi ili mahusiano haya yasitawi inabidi kuwe na njia ya kuhifadhi matukio ya mahusiano haya ili yaweze kukua na kuendelea, kwa maana mahusiano yanaendelezwa kwa mfululizo wa kumbukumbu za matukio ya pamoja.

SURA YA 12

# Imeandikwa kwenye vibao vya Moyo

Katika sura iliyotangulia tuliona kwamba Mungu ana uwezo wa kuandika sheria yake juu ya mioyo yetu, akiweka kanuni Zake za upendo katika akili zetu hasa, kwa sababu kwa asili sheria ni ya rohoni na inazungumzia mambo ya nafsi.

Mungu aliumba ulimwengu wetu kwa njia ambayo kumbukumbu za mwingiliano wetu wote zingerekodiwa. Macho yetu, masikio, na hisi nyinginezo ni vifaa vya kurekodi vya kiroho ambavyo huhifadhi kumbukumbu katika mioyo yetu. Kila mtu ana historia yake yote ya maisha iliyoandikwa ndani ya moyo wake. Ni kutokana na rekodi hii ambapo tunaweza kutambua kama uso au sauti inatambulika au la. Mtume Paulo anadokeza jambo hili kwa njia ifuatayo.

> Ninyi ndinyi barua yetu, iliyoandikwa mioyoni mwetu, inajulikana na kusomwa na watu wote; mnadhihirishwa kwamba mmekuwa barua ya Kristo tuliyoikatibu, iliyoandikwa si kwa wino, bali kwa Roho wa Mungu aliye hai; si katika vibao vya mawe, ila katika vibao ambavyo ni mioyo ya nyama. — 2 Wakorintho 3:2-3

Wakati Paulo alipohubiri injili kwa wengine na wao kuikumbatia, Roho wa Mungu alianza kuandika juu ya mioyo yao furaha ya haki kwa imani. Watu

walianza kubadilika, na kumbukumbu ya badiliko hili ikaandikwa mioyoni mwao na Roho wa Mungu.

Roho wa Mungu anatajwa na Yesu kama kidole cha Mungu. Zingatia ulinganifu huu:

> Lakini mimi nikitoa pepo **kwa Roho wa Mungu,** basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia. — Mathayo 12:28

> Lakini, ikiwa mimi natoa pepo **kwa kidole cha Mungu**, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia. — Luka 11:20

Macho yetu, masikio, na hisi nyinginezo ni vifaa vya kurekodi vya kiroho ambavyo huhifadhi kumbukumbu katika mioyo yetu.

Yesu anaandika kwa kidole chake kwenye vibao vya mioyo yetu rekodi ya maisha yetu. Kupitia hisia ambazo Mungu ametupa, rekodi hii imeandikwa katika akili zetu. Haina makosa katika usahihi wake. Macho yetu hayawezi kutoona mambo ambayo tumeyaona na kufanya na masikio yetu hayawezi kutosikia mambo ambayo tumeyasikia katika maisha yetu yote. Tunaweza kujaribu kusahau mambo tuliyofanya, lakini rekodi itabaki kuandikwa mioyoni mwetu sikuzote. Rekodi hii, bila shaka, imetengenezwa na sisi wenyewe kwa sababu sisi ndio tunaamua hatua tutakazozichukua na kuzitekeleza.

Tunapokuwa na uzoefu wenye baraka kumbukumbu huwa tamu, lakini tunapofanya mambo ambayo yanakiuka mahusiano matakatifu tuliyo nayo na Mungu na kila mmoja wetu mambo haya yanarekodiwa kwa kalamu ya chuma.

> Dhambi ya Yuda imeandikwa kwa **kalamu ya chuma, na kwa ncha ya almasi; imechorwa katika kibao cha moyo wao**, na katika pembe za madhabahu zenu; — Yeremia 17:1

Neno la almasi kwa kweli linamaanisha mwiba unaochoma kama mchomo wa dhamiri yetu. Kwa nini imeandikwa kwa kalamu ya chuma? Wakati dhamiri yetu inapochomwa na wazo kwamba tunafanya jambo baya, ikiwa tutaendelea, matendo yetu yanatiwa makovu ndani ya mioyo yetu na hisia

za hatia. Wakati huo huo kovu la dhambi huifanya mioyo yetu kuwa migumu na tunakuwa na hisia kidogo kwa dhambi. Kwa kadri tunavyotenda dhambi, ndivyo mioyo yetu inavyozidi kuwa migumu, hadi mioyo yetu inakuwa kama chuma kabisa.

Tunakumbuka kwamba mambo haya yameandikwa ndani ya mioyo yetu kwa kidole cha Mungu. Sisi ndio tunafanya matendo, lakini Mungu kupitia Roho wake ametengeneza utaratibu ambao kila kitu huandikwa ndani yetu. Mungu alitengeneza mfumo huu ili kutubariki ili kumbukumbu zetu tamu za mema ziwe nasi daima. Hakutuumba ili kubeba kumbukumbu za huzuni na hatia. Lakini tunapotenda dhambi, maombi ya Roho wa Mungu yanayokataliwa yanaandikwa katika kumbukumbu zetu. Kadiri tunavyopinga kusihi kwa Roho, ndivyo mioyo yetu inavyozidi kuwa migumu hadi tunaweza kuwa kama Farao ambaye moyo wake ulikuwa mgumu kabisa, kumaanisha kutomkubali kabisa Roho wa Mungu.

Ni kwa njia hii kwamba inaweza kueleweka kwamba Mungu anaweza kumvunja mwenye dhambi vipande vipande.

> Utawaponda kwa fimbo ya chuma, Na kuwavunja kama chombo cha mfinyanzi. — Zaburi 2:9

Fimbo ya chuma ni pigo la kalamu ya chuma tunapopinga kusihi kwa Roho na kufanya kile tunachotaka katika uasi dhidi ya Mungu. Uasi unaoendelea na upinzani dhidi ya Mungu hufanya moyo kuwa mgumu sana kiasi kwamba mtu amejitayarisha kwa ajili ya uharibifu. Wanavunjwa vipande-vipande kwa fimbo au kalamu ya chuma ambayo imeandika hatia na uovu mwingi ndani ya nafsi kiasi kwamba inamhuzunisha Roho wa Mungu kabisa na kuichoma dhamiri kwa chuma cha moto.

> Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani; kwa unafiki wa watu wasemao uongo, **wakichomwa moto dhamiri zao wenyewe;** — 1 Timotheo 4:1-2

Ninaweza kukumbuka matukio fulani maishani mwangu nilipojaribiwa kwenda kinyume na dhamiri na kutenda dhambi, na hisia ndani yangu

ikawa moto sana. Inahitajika juhudi kupinga maombi ya Roho. Ni lazima uipinge dhamiri ili kuweza kufanya hivi. Ukifanya hivyo tena na tena, hatimaye moyo unakuwa mgumu sana kiasi kwamba unakuwa si mtu imara na kisha kuvunjika vipande vipande.

Kwa hiyo, tunaona kwamba kuna kumbukumbu ya kila mtu iliyofanywa ndani ya moyo wao wenyewe. Ni rekodi ambayo hakuna anayeweza kuipinga kwa sababu kila mmoja wetu ameiandika kwa hiari yake. Rekodi hii ni rekodi ya kiroho. Haijaandikwa kwa kalamu au wino au juu ya kitu chochote kilichoundwa na mwanadamu. Wakati huo huo kuna rekodi ya yale tuliyofanya mbinguni, lakini haijaandikwa katika kitabu halisi bali imeandikwa katika mikono ya Mungu.

> Tazama, nimekuchora katika vitanga vya mikono yangu; kuta zako ziko mbele zangu daima. — Isaya 49:16

Hii ni kwa sababu Baba yetu aliye mbinguni kupitia Roho wake ameshuhudia kila tukio la maisha yetu. Mambo tunayofanya yanashuhudiwa na kuhisiwa Naye. Yameandikwa katika moyo wake kwa njia ile ile ambayo yameandikwa katika mioyo yetu. Fikiria jinsi ambavyo mzazi hubeba kumbukumbu takatifu ya kila mtoto wao katika mioyo yao. Rekodi ambayo Mungu anatuwekea ni ya thamani zaidi kwake. Nywele zenyewe za vichwa vyetu zimehesabiwa na Yeye.

> Je! Mashomoro watano hawauzwi kwa senti mbili? Wala hasahauliwi hata mmojawapo mbele za Mungu. **Lakini hata nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa zote. Msiogope basi, bora ninyi kuliko mashomoro wengi.** — Luka 12:6-7

Baba yetu na Mwokozi wetu hawaandiki mambo ili kutuadhibu; wanarekodi mambo ili kubaki katika uhusiano wa karibu nasi. Maisha yetu daima yako mikononi mwao na kwa hivyo wanaweka mioyoni mwao rekodi kamili ya maisha yetu ili kuihifadhi. Hii pia ndiyo sababu tunaweza kusema kwa wale wanaoamini haya, kwamba Mungu:

> …akatufufua pamoja, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu, — Waefeso 2:6

Rekodi ya maisha yetu ambayo imewekwa katika moyo wa Kristo pia inatokana na sisi. Anaturuhusu kuandika kumbukumbu katika moyo Wake na hivyo tunaandikwa katika viganja vya mikono Yake. Kwa hiyo ni kweli kwamba Mungu ana rekodi kamili ya maisha yetu, lakini haijaandikwa kwa madhumuni ambayo tunafikiri katika suala la ufuatiliaji, hukumu na adhabu. Imerekodiwa kwa sababu mtu anapompenda mtu mwingine, huwa anamwangalia na kumjali na kumfikiria.

> Ee BWANA, Mungu wangu, umefanya kwa wingi Miujiza yako na mawazo yako kwetu; Hakuna awezaye kufananishwa nawe; Kama ningependa kuyatangaza na kuyahubiri, Ni mengi sana hayahesabiki. — Zaburi 40:5

Hii ndiyo sababu Kristo aliweza kusoma mioyo ya watu waliokuja mbele zake pamoja na mwanamke aliyekamatwa katika uzinzi. Aliweza kusoma kumbukumbu zao ndani ya mioyo yao na pia kuwafahamisha, na walipokuja mbele yake hawakuweza kuficha au kufuta kumbukumbu kutoka kwenye kumbukumbu zao. Kile Kristo alichoandika ardhini kilikuwa ni marudio tu ya yale aliyokuwa ameyaandika ndani ya mioyo yao kwa kidole cha Mungu na ambayo wao wenyewe walikuwa tayari wametia sahihi pamoja na kibali chao.

Ni kwa sababu hii kwamba Mungu anapofungua vitabu mbinguni, Anafikia mioyo ya wanadamu. Hana haja ya vitabu vya kimwili kama tunavyotumia leo kwa sababu sheria yake si ya kimwili bali ya kiroho; kushughulika na mambo ya moyo na akili ambayo yanadhihirika katika mwili.

Mungu hatuchunguzi kwa kusudi la kutuhukumu na kutuadhibu; Kwa upendo hutuangalia na kutufikiria kila siku na anatamani kutubariki. Hivi ndivyo kumbukumbu inavyohifadhiwa katika moyo Wake. Tunapomkosea Mungu, tunachukua kalamu hiyo ya chuma na kumchoma Kristo ubavuni na kumsulubisha upya.

> ....wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa **wamsulibisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao**, na kumfedhehi kwa dhahiri. — Waebrania 6:6

Moyo wa Kristo haugeuki kamwe kuwa chuma, hivyo kila wakati tunapoandika matendo yetu ya dhambi juu yetu wenyewe na analazimishwa kushuhudia, inamchoma kwa uchungu mwingi. Huwa hivyo kila wakati kwa sababu Yeye kamwe moyo wake hauwi mgumu ili kutenda dhambi. Hatimaye tunapokutana na Kristo uso kwa uso, rekodi tuliyoandika juu Yake itakutana nasi - yote - na kisha tutaamua wenyewe kama tutasamehewa au la. Atatuuliza, "Je, hakuna yeyote anayekuhukumu?" Jibu lako litakuwa ni lipi? Utajihukumuje wewe mwenyewe unaposimama mbele zake na kila neno ulilonena na kila wazo la siri ulilotafakari limeandikwa mbele yako katika nafsi ya Kristo? Utahukumu vipi? Maovu yetu yote tuliyoyatenda na kuyaficha, tukikabiliwa nayo, yatatushinda? Yesu hataki tushikwe na mshangao na kumezwa na aibu na hatia katika siku hiyo ya mwisho; Anataka tuachane na maumivu machungu ya nafsi zetu leo na atuponye.

Ni katika muktadha huu ambapo Muumba wetu, ambaye anasema Yeye ni upendo (1 Yohana 4:8), hatunzi kumbukumbu ya matendo yetu maovu kwa kusudi la kutuadhibu.

> Upendo huvumilia, upendo hufadhili. Hauna wivu, haujisifu, hauna kiburi. Hauwavunjii wengine heshima, hauna ubinafsi, haukasiriki upesi, **hauweki kumbukumbu ya makosa**. — 1 Wakorintho 13:4-5 ( NIV)

Kuna tofauti gani kati ya kumbukumbu za maisha yetu zilizoandikwa kwenye moyo wa Yesu na rekodi ya makosa yaliyorekodiwa? Rekodi ambayo Yesu anaiweka iko ndani Yake; ni sehemu yake mwenyewe kwa sababu viumbe vyote vinashikamana katika Yeye. (Wakolosai 1:17). Rekodi ya makosa ni kitu kilicho nje yetu ambacho hakihisi maumivu, huzuni, au hasara. Hakiumizi moyo na kwa hivyo kinaweza kujikita katika adhabu isiyohisiwa inayohusisha kifo. Baba yetu na Mwanawe hawatunzi rekodi isiyohisiwa ya makosa yetu, lakini moyo wa Kristo una kumbukumbu iliyoandikwa katika Utu Wake.

Kanuni hiyo imeonyeshwa katika maono ya Ufunuo 5 kuhusu kitabu kilichofungwa ambacho hakuna mtu angeliweza kukifungua.

> Nao waimba wimbo mpya wakisema, "**Wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu** na kuzifungua muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa, ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu; nao wanamiliki juu ya nchi." Ufunuo wa — Yohana 5:9-10

Kristo anastahili kukifungua kitabu cha historia yetu ya kibinadamu kwa sababu alichinjwa kwa ajili yetu na ametembea pamoja nasi katika ubinadamu wetu unaoteseka.

Wale wanaoabudu mungu anayetengeneza orodha na kuzichunguza mara mbilimbili ili kuona kama tumekuwa watukutu au wazuri wanaabudu mungu wa ufuatiliaji, hukumu na kifo. Huyu si Mungu wa Yesu Kristo asiyeweka rekodi kama hiyo dhidi yetu. Tutakapokutana na Muumba wetu na kuja mbele za Yeye ambaye amebeba kumbukumbu zote za maisha yetu katika moyo Wake, tutaulizwa "Je, hakuna yeyote anayekulaani wewe kwa hili?" Utajibuje na utahukumu nini?

SURA YA 13

# Mawazo Yangu Si Mawazo Yenu

Katika sura ya 11, tuliangalia jinsi ambavyo uongo wa Shetani wa kwamba tuna maisha mbali na Mungu ulivyobadilisha uelewa wetu wote wa sheria. Katika sura ya 2 tulianza kuchunguza uwezekano wa kwamba haki ya Mungu ni tofauti na uelewa wetu wa haki. Kabla hatujaendelea kuchunguza kwa kina hukumu kama inavyofundishwa katika Maandiko, acheni tuchunguze kwa undani zaidi maana ya uongo wa Shetani kuhusu kutokufa na matokeo yake katika mitazamo yetu juu ya hukumu.

1. Shetani alidai kwamba hakika hatutakufa na kwa kula tunda la mti uliokatazwa kwamba tutakuwa kama Mungu. Mwanzo 3:5
2. Hili lilibadilisha mitazamo ya wanadamu kuhusu sheria. Ikiwa hatumtegemei Mungu kwa ajili ya uzima, basi sheria yake imewekwa juu yetu bila sababu halali.
3. Kwa hiyo, nia ya kimwili inapigana na sheria ya Mungu na inakataa kutii. Warumi 8:7
4. Kutenganishwa kwa ubinadamu kutoka kwa Mungu kungewafanya waangamie, kwa kuwa ni Mungu pekee aliye na uzima. Lakini Shetani anawaalika wanadamu kuwamwona Mungu kama msababisha kifo. Ikiwa mwanadamu anaona sheria ya Mungu kama agizo lisilo na maana, basi ni jambo la kimantiki kuyaona matokeo ya ukiukaji wa sheria hiyo kama mambo yaliyowekwa. Tunaona hili likifanyika katika maisha ya Kaini. Mungu anamwambia Kaini

matokeo ya asili ya matendo yake na Kaini anamtupia Mungu lawama kwa hali ya uhalisia wake mpya. Mwanzo 4:11-14

5. Kisha Shetani anaambatanisha kuwekwa kwa kifo kama adhabu ya kuvunja sheria ya Mungu. Anamdhihirisha Mwenyezi Mungu kuwa ni mwonevu katika kutoa adhabu. Tunajua hili kwa sababu kifo kinaonyeshwa kama adui wa Mungu na mwanadamu na kitu ambacho kiko katika utawala wa Shetani. Waebrania 2:14, 1 Wakorintho 15:26
6. Shetani anawasilisha kifo kwa mwanadamu kama haki ya Mungu kwa kosa la mwanadamu, akionyesha utawala wa Shetani kuwa ni wa Mungu na kumfanya Mungu kuwa mwanzilishi wa kifo. Zaburi 50:21; Zaburi 94:20
7. Kama tulivyoonyesha katika sura ya 3, basi rehema inaeleweka kuwa kama gharama inayolipwa ili kuchelewesha au kuondoa adhabu. Katika mfumo wa Shetani, rehema haimaanishi kamwe kumsamehe mtu bila pesa au bila malipo (Isaya 55:1). Mfumo huu unahitaji kwamba "haki ya Mungu" lazima itulizwe kwa dhabihu; inadai malipo ya aina fulani.
8. Uanzishwaji wa kifo kwa wanadamu kama adhabu kutoka kwa Mungu huufanya muda kuwa kitu cha thamani sana. Kipindi cha matazamio kimetolewa kwetu ili kuchagua kama tutaamini kwamba Mungu ni mwema, tuache kujitenga naye, na kumruhusu atuonyeshe dhambi zetu ili tupate kuponywa. Lakini tunaelewa kipindi hiki cha rehema katika mfumo wetu wa haki kuwa tumepewa sisi ili kumtuliza Mungu kwa matendo mema au ushahidi wa toba kwa kuukubali Msalaba kabla ya hukumu ya mwisho. Hii ina maana kwamba mara zote tunakimbia kutoka kwenye utambuzi na uponyaji unaotolewa, na kwa hivyo maisha yanakitwa katika kuitazama saa inayo-yoyoma ambapo tunakosa amani kabisa. Kuna hisia ya kudumu ya kuishiwa na wakati na hisia ya maangamizi tunapokimbia kuielekea hukumu, ambayo sasa ina maana ya adhabu ya waovu na uthibitisho wa wema.
9. Utaratibu huu wote ni mgeni kwenye mawazo ya Mungu. Kanuni zake za rehema, haki na adhabu ni tofauti kabisa na zetu. Dhana hizi tukufu zimepotoshwa katika akili zetu na uongo wa maisha ya asili

> ambayo hutufanya tuhisi bila kujua hatumhitaji Mungu na kwamba Yeye ni mtu anayetudhibiti kwa ukali.

Athari ya uongo huu wa kuwa na uzima asilia mbali na Mungu unaelezewa vyema na kisa cha kile kinachoonekana kuwa meli mbili zilizokuwa zikielekeana usiku. Redio ya meli moja ilisikika ikiwaambia meli nyingine kugeuza mkondo wao kutoka kwenye njia ya meli yao. Sauti inarudi kwenye redio kwamba hapana, unapaswa kugeuza mkondo wako ili kuepuka mgongano. Nahodha wa meli anamtishia mtu wa upande mwingine aliekuwa akiwasiliana naye kugeuza mkondo wao au kukabiliana na matokeo. Sauti inajibu, "huu ni mnara wa taa, wito wako."

Wanadamu walipokubali uongo kwamba tunaweza kuwa na kutokufa na kuwa kama Mungu, tulibadilisha uhusiano wetu na Mungu na tukamwazia kuwa kama sisi. Nuru hiyo kubwa kutoka kwenye mnara wa taa ambayo ilitumwa kwa upendo ili kutulinda kutokana na uharibifu ilifasiriwa kuwa ya dhamira ya uadui, na jamii ya kibinadamu ilijitayarisha kwa vita dhidi ya mnara huo. Wakati meli ilipotambua utambulisho wa kweli wa chanzo kingine cha mwanga, dhana nzima ilibadilika na mwanga ukaeleweka mara moja katika muktadha wake ufaao.

> Hukumu ya Mungu imekusudiwa kuleta uponyaji na urejeshaji, sio adhabu na kifo.

> Katika mateso yao yote yeye aliteswa, na malaika wa uso wake akawaokoa; kwa mapenzi yake, na huruma zake, aliwakomboa mwenyewe; akawainua, akawachukua siku zote za kale. Lakini wakaasi, wakamhuzunisha Roho yake Mtakatifu; kwa hiyo akawageukia, akawa adui, akapigana nao. — Isaya 63:9-10 (KJV)

Hivi ndivyo ilivyo katika hukumu. Tunamfikiria Mungu kuwa kama sisi. Tunamwazia kuwa mtu anayehukumu, kulaani na kuadhibu kama sisi. Lakini mawazo yake si mawazo yetu.

Hata hivyo, ili tuone hali yetu halisi, Mungu huturuhusu kukabiliana na hukumu ambayo tunafikiri Mungu anaitumia. Ikiwa Mungu hakuwa na hukumu kama tunavyoielewa, basi tusingemwona kuwa Mungu mwenye haki.

Kwa sababu ya uongo wa Shetani kuhusu uzima, tumerithi namna ya kufikiri juu ya uzima, kifo na adhabu inayompelekea Mungu sasa ahitaji kutuonyesha kwamba sivyo anavyofikiri, wakati huo huo akituvuta kwake. Anapaswa kuja karibu nasi kwa kujiruhusu aonekane kama sisi, ili tusiende mbali naye tukiamini kwamba yeye si mwenye haki na aliye mwema machoni petu.

Hukumu ya Mungu imekusudiwa kuleta uponyaji na urejeshaji, sio adhabu na kifo.

> Yesu akasema, **Mimi nimekuja ulimwenguni humu kwa hukumu**, ili wao wasioona waone, nao wanaoona wawe vipofu. — Yohana 9:39 (KJV)

Matokeo ya hukumu ya Yesu ni kwamba vipofu waanze kuona. Huu ni mfumo wa hukumu ya uponyaji. Wakati huo huo Yesu anasema kwamba hukumu yake itawafanya wale wanaofikiri wanaweza kuona kuwa vipofu, maana yake wanatambua kwamba wamekuwa vipofu (Ufunuo 3:17). Lakini kwa nini Yesu anawataka wakiri kwamba wao ni vipofu? Ni ili wapate kuponywa. Yesu alieleza sehemu ya msingi ya utume Wake kama kuwapa vipofu kupata kuona tena.

> Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema; amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na **vipofu kupata kuona tena**, kuwaacha huru waliosetwa, — Luka 4:18 (KJV)

Ni wale tu wanaotambua upofu wao wanaoweza kuponywa. Kanuni hii ya urejeshwaji imewasilishwa katika Agano la Kale katika visa mbalimbali.

> Na wakati BWANA **alipowainulia waamuzi, ndipo BWANA alikuwa pamoja na mwamuzi huyo, akawaokoa na mikono ya adui zao** siku zote za mwamuzi huyo; maana BWANA alighairi kwa ajili ya kuugua kwao kwa sababu ya watu wale waliowaonea na kuwasumbua. — Waamuzi 2:18

Ingawa kazi ya waamuzi haikuwa kamilifu, bado tunaweza kuona kusudi lilikuwa kukombolewa kutoka kwenye mateso. Kitabu cha Isaya pia kinaeleza mada hii ya ukombozi kupitia hukumu.

> “nami nitarejeza upya waamuzi wako kama walivyokuwa hapo kwanza, na washauri wako kama hapo mwanzo; baada ya hayo utaitwa, Mji wa haki, mji mwaminifu.” Sayuni itakombolewa kwa hukumu, na waongofu wake kwa haki. — Isaya 1:26-27

> Haki yangu i karibu, wokovu wangu umekuwa wazi, na mikono yangu itawahukumu kabila za watu; visiwa vitaningoja, navyo vitautumainia mkono wangu. — Isaya 51:5

Biblia inadhihirisha kwamba mawazo ya Mungu ya hukumu ni kwa ajili ya ukombozi, uponyaji na urejeshaji, si hukumu inayopelekea kifo. Lakini hii inaweza kutokea tu ikiwa tunakubali utambuzi wa Mungu wa tatizo letu badala ya utambuzi wetu wenyewe. Kisha tunaweza kuomba uponyaji na kuamini kuwa tutabadilika.

Ili kueleza jinsi Mungu anavyotuponya katika hukumu tunahitaji kuzingatia somo la Patakatifu, kwa maana hili ndilo somo muhimu ambalo linaweka kwa undani mchakato ambao kwa huo Mungu anatuokoa.

SURA YA 14

# Njia yako Ee Mungu i katika Patakatifu

Mambo tuliyozungumzia katika sura iliyotangulia yaliweka pengo kubwa kati ya Mungu na mwanadamu. Kupitia ushawishi wa Shetani, jamii ya wanadamu iligeuzwa na kuelekezwa kwenye njia yenye giza. Je, Mungu angewezaje kutukomboa na kurekebisha upya fikra zetu za uongo? Mawazo yetu yanawezaje tena kuwa mawazo ya Mungu ili tuweze kuelewa ukweli wa tabia Yake?

> Yesu akamwambia, **Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima;** mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi. — Yohana 14:6

Yesu ndiye njia ya kwenda kwa Baba, ukweli wa Baba na uzima wa Baba. Ni kwa njia ya Kristo tunawezeshwa kumrudia Mungu. Neno njia katika Kigiriki katika mstari hapo juu ni G3598 hodos, likimaanisha njia. Neno hili hili linatumika katika Agano la Kale la Kiyunani katika mstari huu:

> **Ee Mungu, njia yako** i katika patakatifu [Hekalu]; ni nani aliye Mungu mkuu kama Mungu wetu? — Zaburi 77:13

Ili Mungu aje karibu nasi na kukaa nasi, alijenga Patakatifu.


> Nao na wanifanyie patakatifu; ili nipate kukaa kati yao. — Kutoka 25:8

Lengo la kutembea katika njia hii ya Patakatifu ni kufanya mioyo yetu ya mawe iwe laini tena na kuwa mioyo ya nyama.

> Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama. — Ezekieli 36:26

Ishara ya Patakatifu [hekalu] inatuwekea hatua za kufuata ili tuweze kurudishwa kikamilifu kwa Mungu na kupatanishwa naye.

Hebu tuangalie mpangilio wa mfumo huu wa Patakatifu.




Mwenye dhambi huingia Patakatifu kupitia mlango wa ua. Chumba kiitwacho Patakatifu pa Patakatifu ni mahali ambapo uwepo wa Mungu ulikaa katika mfumo mzima wa hekalu.

Kuna vitu vingi katika hekalu na huduma zake ambazo tungeweza kujikita kwavyo,[24] lakini tunataka tu kuangalia mambo machache katika mwendelezo wa kutoka kwenye ua hadi Patakatifu Pa Patakatifu.

Kwanza, tunaona kwamba samani zote katika ua zimefunikwa na shaba. Samani za Mahali Patakatifu zimetengenezwa kwa dhahabu au zimefunikwa kwa dhahabu.[25] Kubadilika kwa madini kunaonyesha badiliko la ubora. Huwakilisha mabadiliko ya tabia yanayofanyika ndani ya mtu anapoendelea katika ujuzi wa Mungu. Kipengele cha shaba kinavutia kwa sababu ni muunganiko wa madini ya aina mbili, shaba na bati. Ni chuma ambacho kimetengenezwa na mwanadamu. Hakikuumbwa na Mungu.

> Sila naye akamzaa Tubal-kaini, mfua kila chombo cha kukatia, cha shaba na cha chuma; na umbu lake Tubal-kaini alikuwa Naama. — Mwanzo 4:22

Mungu anazungumza juu ya shaba nyeupe/shaba kwa njia hasi kama kitu cha kusafishwa kama takataka.

> Mwanadamu, nyumba ya Israeli imekuwa taka za fedha kwangu; wote *wamekuwa* **shaba, na bati, na chuma, na risasi**, kati ya tanuu; wamekuwa taka za fedha. — Ezekieli 22:18

Madhabahu ya dhabihu ni mahali ambapo dhabihu za wanyama zilitolewa. Inawakilisha kifo cha Kristo Msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. Uhakika wa kwamba ishara ya dhabihu ya Kristo iko juu ya madhabahu ya *shaba* unaonyesha kwamba Mungu anakubali *mawazo ya mwanadamu* kuhusu kile kinachohitajika ili upatanisho utendeke.

Mwanadamu alipoelekeza sababu ya kifo chake mwenyewe kwa Mungu kama adhabu ya Mungu kwa ajili ya dhambi ya mwanadamu, Mungu ilimbidi kutoa mbadala wa mwanadamu; malipo yalihitajika kabla mwanadamu hajakubali rehema ya Mungu na kuamini kwamba Mungu aliridhika kwamba heshima yake iliendelea kutunzwa. Katika kutoa dhabihu hii, Mungu anafichua kile mwanadamu anachofikiri na kile ambacho

---

[24] Please read Life Matters chapter 15 for more on this. Available at fatheroflove.info


[25] For more on this see chapter 8 of the book Cross Examined and Cross Encountered available at fatheroflove.info

mwanadamu anahitaji ili aamini kwamba Mungu ni wa neema kwake. Hoja hii kwa upande wa mwanadamu inaweza kuwa inafahamika, au hata kitofahamika, lakini bado iko pale; ni urithi wa akili zetu zilizoanguka. Kila sehemu ya Hekalu ni kumfikia mwanadamu ili kuzungumza naye mahali ambapo mawazo yake yalipo na kumpatanisha na Baba.

Kanuni mbili kuu ambazo mwanadamu alihitaji kupatanishwa nazo zilikuwa ni kuhumu ya adhabu na kifo.

> Na karama hiyo si kama ilivyokuwa kwa mtu mmoja aliyetenda dhambi; **kwa maana hukumu ilileta adhabu kwa mtu mmoja; Kwa maana ikiwa kwa kosa la mtu mmoja mauti ilitawala kwa sababu ya mmoja;** zaidi sana wao wapokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki, watatawala katika uzima kwa yule mmoja, Yesu Kristo. — Warumi 5:16-17 (KJV).

Anayehukumu hukumu ya adhabu na ambaye kosa lake lilisababisha kifo kutawala ni Adamu. Adamu alifikiri kwamba Mungu alimhukumu na mwenye shauku ya kumwua. Kwa hiyo, haya ndiyo maeneo mawili ya Hekalu ambayo lazima yafunuliwe kwa wanadamu. Hekalu ni mstatili unaounda miraba miwili. Katikati ya mraba wa kwanza kuna madhabahu ya dhabihu. Katikati ya mraba wa pili kuna sanduku la agano.



Sadaka zilitolewa kwenye madhabahu ya sadaka kila siku. Hukumu ya siku ya upatanisho ilifanyika mara moja tu kwa mwaka.

> Lakini siku ya kumi ya mwezi huo wa saba ni siku ya upatanisho; itakuwa kusanyiko takatifu kwenu, nanyi mtazitesa nafsi zenu; nanyi mtasongeza sadaka kwa BWANA kwa njia ya moto. Nanyi msifanye kazi yo yote siku hiyo; kwa kuwa ni siku ya upatanisho, ili kufanya upatanisho kwa ajili yenu mbele za BWANA, Mungu wenu. Kwa kuwa mtu awaye yote asiyejitesa mwenyewe siku iyo hiyo, atakatiliwa mbali na watu wake. Na mtu ye yote afanyaye kazi ya namna yo yote siku hiyo, mtu huyo nitamwangamiza atoke katika watu wake. — Mambo ya Walawi 23:27-30

Maelezo haya yaliyotolewa katika Mambo ya Walawi ni onyesho la jinsi wanadamu wanavyoelewa jinsi Mungu anavyopaswa kufanya kazi katika hukumu. Adamu ndiye aliyeleta hukumu, adhabu na mauti ulimwenguni. Njia ya Hekalu ni kutufunulia jinsi fikra zetu halisi zilivyo na kisha kulinganisha kile tunachokifikiri na maisha ya Yesu na kutambua kwamba mawazo yetu ni hayako sahihi. Hivi ndivyo upatanisho unavyofanyika. Ni mchakato wa kudhihirisha kwamba mfumo wetu wa maadili wenye dhambi uliorithiwa ni mbaya, na kisha tunatubu na kusamehewa. Hili linakamilisha mchakato wa upatanisho.

Dini nyingi huamini kwamba kwa sababu Mungu huamuru dhabihu na anaonekana kama hakimu katika Patakatifu pa Patakatifu Siku ya Upatanisho, hivyo ndivyo Yeye alivyo. Lakini huu ni uongo. Mungu anafanana na Yesu na mambo haya yaliyoandikwa katika sheria huakisi jinsi tulivyo. Mungu anayaonyesha kwetu ili tuweze kutubu na kuachana nayo.

Mungu anakutana nasi kwenye madhabahu ya shaba, madhabahu iliyotengenezwa kwa mchanganyiko wa madini yenye thamani ya chini iliyoundwa na mtoto wa Kaini. Baba yetu hakutamani kamwe dhabihu, lakini alizitoa ili kutuonyesha jinsi tulivyo katika asili. Tuliamini kwamba Mungu alihitaji kutulizwa kabla hajatusamehe, na tusingeamini kwamba tumesamehewa hadi damu imwagike. Hili ni wazo la kutisha, la kipagani; lakini hatukutambua. Alikuza hali yetu ya dhambi katika dhabihu hizi, wakati

huo huo kupitia shaba hii, wazo lililoundwa na mwanadamu lilitusadikisha kwamba tunaweza kusamehewa.

Mungu hahukumu au kumwadhibu mtu yeyote (Yohana 5:22; 8:15), lakini anaturuhusu kumwelewa kwa njia hii ili atuonyeshe kile tunachokifikiri kwamba Mungu anahitajika kukifanya ili kukomesha pambano hili. Kwa kawaida tunafikiri kwamba Mungu lazima atupatie muda wa kutubu, na kisha hatimaye kuhukumu kila mtu na kuua wale ambao hawatii na kuwalipa wale wanaotii.

Ikiwa tutaweza kukumbuka kwamba hekalu ni njia ya kuwaleta wanadamu kwa Mungu, basi tutakubali kwamba njia ya mchakato huu haiwakilishi Mungu ni nani, bali kile ambacho Mungu yuko tayari kukifanya ili kutufikia tulipo.

Hekalu lina ua wa shaba, huku likiwa na Patakatifu na Patakatifu pa Patakatifu palipotengenezwa kwa dhahabu na fedha. Mungu hawakilishwi na ua; huu ni uwakilishi wa wanadamu. Hili linathibitishwa na ukweli kwamba Mungu anawaambia watu wake kwa wakati fulani katika mchakato huu kuuacha ua wa nje wakati wa kupima au kujifunza mfumo huu.

> Nikapewa mwanzi kama fimbo; na mmoja akaniambia, Inuka, ukalipime hekalu la Mungu, na madhabahu, na hao wasujuduo humo. **Na behewa iliyo nje ya hekalu [Ua wa nje] uiache nje wala usiipime, kwa maana Mataifa wamepewa hiyo**, nao wataukanyaga mji mtakatifu miezi arobaini na miwili. — Ufunuo wa Yohana 11:1-2

Mahali Patakatifu hapawakilishi kikamilifu Mungu ni nani kwa sababu Mungu daima ni Mtakatifu Zaidi. Je, Mungu anawezaje kuwa Mtakatifu mahali pamoja na Mtakatifu Zaidi mahali pengine? Mahali Patakatifu hufunua mwendelezo wa mawazo ya watu kuuelekea ukweli. Sio ufunuo kamili wa jinsi tabia ya Mungu ilivyo. Hata Patakatifu pa Patakatifu sio kielelezo kamili cha tabia ya Mungu kwa sababu Mungu hakuwahi kutamani dhabihu na Hakuhitaji kamwe sadaka za kuteketezwa (Zaburi 40:6, Hosea 6:6). Haya yote ni katika kujaribu kukutana na kukidhi matakwa ya wanadamu katika mahali walipokuwa kulingana na mawazo yao. Ni

mchakato wa kutuonyesha jinsi tulivyo na kisha kutualika kulinganisha mifumo hii na jinsi Kristo alivyo na kutubu pale tunapoona utofauti.

Nilipokuwa kijana mdogo katika utineja wangu, nilifanya mambo ambayo yalinifanya nijisikie mwenye hatia sana, na nilitambua kwa kiasi fulani hali yangu ya kuwa mgonjwa wa dhambi na nilihitaji msaada. Kilikuwa ni kifo cha Yesu Msalabani kilichonifanya niamini kwamba Mungu alinisamehe dhambi zangu. Hili ni muhimu kwa wokovu. Mara nilipoamini kwamba dhambi zangu zimesamehewa na nikaanza kumfahamu zaidi Mungu jinsi alivyo kupitia kusoma habari za Yesu, mambo mengi maishani mwangu yalianza kubadilika.

Miaka michache baadaye nilianza kukua katika ufahamu wangu, nilianza kuwahukumu na kuwashutumu wengine kwa kutofuata yaliyo sawa. Ningefanya hivi kwa siri zaidi kuliko ambavyo ningefanya kwa uwazi. Niliwahukumu watu kwa sababu nilimwona Mungu akiwahukumu watu kwa kufanya mambo mabaya. Aliniruhusu nimwone kwa njia hii ili roho yangu ya hukumu ifunuliwe. Aliniruhusu kumuona kupitia Siku ya Upatanisho kama Hakimu wa kutisha na Mtakatifu ambaye alikuwa tayari kuwaangamiza wenye dhambi ambao hawakunyenyekea na kutii.

Kisha kwa wakati ufaao, Alinionyesha kile ambacho Mwanawe alikisema kumhusu katika Yohana 5:22 na jinsi Yesu Mwenyewe alivyotenda katika Yohana 8:15. Niliposoma maandiko hayo na kuyalinganisha na mimi mwenyewe, nililia kwa siku nyingi. Nilitubu na kumwomba Mungu anisamehe. Ghafla nilijiona kama mtu wa kuhukumu sana na hiki ndicho nilichokuwa nakihitaji. *Ufunuo wa hukumu ndio hasa ubinadamu unaouhitaji kuutambua jinsi tulivyo kiasilia watu wa kuhukumu na kushutumu.*

Ufunuo wa hukumu ndio hasa ubinadamu unaouhitaji kuutambua jinsi tulivyo kiasilia watu wa kuhukumu na kushutumu.

Hivi ndivyo Mungu alivyoshughulika na wanafunzi katika Mathayo 15:22-28. Alitenda kwa njia iliyoruhusu chuki yao dhidi ya mwanamke Mkanaani ifunuliwe. Hatimaye Yesu alipomponya bintiye mwanamke huyo, wanafunzi walikuwa na chaguo la kufanya. Ilibidi wajione kama watu wenye misimamo ya kidini na kutubu, au waache kumwamini Yesu.

Hii ndiyo sababu watu wengi hawatamkubali Mungu wa kweli na Mwanawe. Hawataacha tamaa ya kuhukumu na kushutumu na watanukuu Maandiko mengi kuthibitisha kwamba Mungu anahukumu na kushutumu. Maandiko haya yote yapo ili kutujaribu na kudhihirisha kile kilicho ndani yetu. Yanafanya kazi kwa njia ile ile kama inavyoonekana kana kwamba Yesu alimwita yule mwanamke Mkanaani mbwa. Tunahitaji kuchunguza vifungu hivi kwa makini zaidi.

Sasa tuangalie uelewa wa jumla wa hukumu na kufunguliwa kwa vitabu mbinguni kwa namna vinavyohusiana na Siku ya Upatanisho tuliyoizungumzia hapo awali.

SURA YA 15

# Vitabu Vikafunguliwa na Hukumu ikawekwa

Mlolongo wa historia uliowekwa katika Danieli 7 na 8 unatupa wakati maalum sana ambapo matukio ya hukumu yanatukia. Mtume Paulo alizungumza na Feliki kuhusu wakati ujao wa hukumu uliokuwa katika siku zijazo:

> Na Paulo alipokuwa akitoa hoja zake katika habari ya haki, na kuwa na kiasi, **na hukumu itakayokuja**, Feliki akafanya hofu akajibu, Sasa enenda zako, nami nikipata nafasi nitakuita. — Matendo ya Mitume 24:25

Matukio tuliyopewa katika Danieli 7 yanatusaidia kujua ni lini hukumu hii itatokea. Danieli anaona katika maono hayawani wanne wakitoka katika bahari. Wa kwanza anafanana na simba, wa pili dubu, wa tatu chui na wa nne ni mnyama asiye na jina. Baada ya kuinuka kwa wanyama hawa wanne kuna tukio la hukumu linalotukia, na kisha ufalme wa Kristo unakuja na watu wa Mungu watamiliki ufalme huu.

> Wanyama hao wakubwa walio wanne ni wafalme wanne watakaotokea duniani. — Danieli 7:17

Hawa wanyama wanne wanawakilisha wafalme wanne au, kama inavyofafanuliwa mbele kidogo, falme nne.

> Akanena hivi, Huyo mnyama wa nne **atakuwa ni ufalme wa nne juu ya dunia,** utakaokuwa mbali na falme zile zote, nao utakula dunia yote, na kuikanyaga, na kuivunja vipande vipande. — Danieli 7:23

Kutoka kwenye ufalme huu wa nne kunainuka falme 10, na baada ya hili kunainuka ufalme mwingine ulio tofauti kiasilia na nyingine na falme tatu zinangushwa ili kuuwezesha ufalme huu kutokea.

> Na habari za zile pembe kumi, katika ufalme huo wataondoka wafalme kumi; na mwingine ataondoka baada ya hao; **naye atakuwa mbali na hao wa kwanza; naye atawashusha wafalme watatu.** — Danieli 7:24

Pembe hii ndogo inazungumza maneno makuu dhidi ya Aliye Juu Zaidi na kubadilisha nyakati maalum za Mungu na sheria yake na kuwatesa watakatifu wa Mungu kwa muda wa nyakati tatu na nusu.

> Naye atanena maneno kinyume chake Aliye juu, naye atawadhoofisha watakatifu wake Aliye juu; naye ataazimu kubadili majira na sheria; nao watatiwa mikononi mwake kwa wakati, na nyakati mbili, na nusu wakati. — Danieli 7:25

Kama tulivyoonyesha hapo awali, kuna tukio la hukumu ambalo hufanyika na kisha ufalme wa Kristo unakuja na utaendelea milele.

> Lakini hukumu itawekwa, nao watamwondolea mamlaka yake, kuipoteza na kuiangamiza, hata milele. Na ufalme, na mamlaka, na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu zote, watapewa watu wa watakatifu wake Aliye juu; ufalme wake ni ufalme wa milele, na wote wenye mamlaka watamtumikia na kumtii. — Danieli 7:26-27

Tukiangalia mlolongo wa historia tangu wakati wa Danieli hadi sasa, tunaona kweli kwamba kumekuwa na falme nne za dunia na kufuatiwa na mgawanyiko wa mamlaka 10 za Ulaya, ukifuatiwa na Upapa ambao ulitawala mambo ya ulimwengu kwa zaidi ya miaka 1000.

Milki nne za ulimwengu zinawakilishwa na Babeli, Umedi-Uajemi, Ugiriki na Rumi.




Mlolongo huu wa falme nne zinazofuatwa na upanukaji wake hadi 10 unalingana na maono katika Danieli 2. Danieli alimwambia mfalme wa Babeli kwamba mfalme alikuwa kichwa cha dhahabu na kwamba kungekuwa na mfululizo wa falme tatu za ulimwengu baada ya ufalme wake. Tunaweza kufupisha habari za pembe ndogo katika Danieli 7 kama ifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | **Akainuka kutoka kwa mnyama wa nne.** *Danieli 7:7,8* | 1 | **Mapapa walichukua nafasi ya Kaisari.** |
| 2 | **Miongoni mwa pembe 10.** *Danieli 7:24* | 2 | **Upapa ulikua na nguvu miongoni mwa mataifa ya Ulaya.** |
| 3 | **Tofauti na pembe nyingine.** *Danieli 7:24* | 3 | **Upapa ni nguvu ya kidini na kisiasa.** |
| 4 | **Anaonekana kuwa mwenye nguvu zaidi kuliko pembe zingine.** *Danieli 7:20* | 4 | **Angetumia mamlaka zaidi kuliko wafalme.** |
| 5 | **Kung'olewa falme 3.** *Danieli 7:8,20,24* | 5 | **Kuondolewa kwa Heruli, Vandali na Ostrogothi.** |
| 6 | **Kunena maneno makuu kinyume chake Aliye juu.** *Danieli 7:24* | 6 | **Alidai kuwa Mungu duniani na ana uwezo wa kusamehe dhambi.** |
| 7 | **Kuwadhoofisha watakatifu wake Aliye juu.** *Danieli 7:25* | 7 | **Kati ya watu milioni 50 na 150 waliouawa na Upapa.** |
| 8 | **Aliazimu kubadili nyakati na sheria.** *Danieli 7:25* | 8 | **Kuibadilisha Sabato kuwa Jumapili, iliondoa amri ya pili.** |
| 9 | **Alitawala kwa wakati, nyakati mbili na nusu wakati.** *Danieli 7:25* | 9 | **Utawala wa Upapa ulikuwa kutoka 538 BK hadi 1798 BK.** |

Utambulisho wa pembe ndogo kama Upapa ulioibuka baada ya milki nne za ulimwengu unathibitishwa na Wasomi wengi wa Biblia kwa karne nyingi.

| Jina | Tarehe | Pembe ndogo | Mtu wa kuasi | Mwanamke wa ufunuo 17 | Mpinga Kristo |
|---|---|---|---|---|---|
| Waldensia | Karne ya 12 | | Upapa | Kanisa la Rumi | |
| Eberhard II (Salzburg) | Miaka ya 1246 | Upapa | | | |
| John Milicz | Miaka ya 1367 | | Upapa | Upapa | Upapa |
| John Wycliff | Miaka ya 1379 | Mapapa | Upapa | Upapa | Mapapa |
| John Huss | Miaka ya 1412 | | Upapa | Upapa | Papa |
| Girolamo Savonarola | Miaka ya 1497 | | Upapa | Upapa | |
| Martin Luther | 1522 | Upapa | Upapa | Upapa | Upapa |
| Philipp Melanchthon | 1543 | Upapa | | | Upapa |
| John Knox | 1547 | Upapa | Upapa | Upapa | Upapa |
| William Tyndale | 1550 | | Upapa | Upapa | Upapa |
| John Hooper | 1550 | | Upapa | Upapa | Upapa |
| Nicholas Ridley | 1554 | | | Upapa | Upapa |
| Thomas Cranmer | 1582 | Upapa | Upapa | Upapa | Upapa |
| James I of England | 1600 | Upapa | Upapa | Upapa | Upapa |
| Sir Isaac Newton | 1727 | Upapa | Upapa | Upapa | Upapa |
| John Wesley | 1764 | | Upapa | Upapa | Upapa |

Madhumuni ya utambulisho huu sio kulaani kikundi au shirika lolote; kuinuka kwa mamlaka hii ni onyesho la asili ya mwanadamu na kunaonyesha jinsi sisi sote tulivyo. Kuwahukumu viongozi wa Upapa ni kujidhihirisha kuwa na nia na roho ya aina ileile kama yao. Kusudi letu ni kutambua harakati za kinabii katika historia ya mwanadamu ili kujifunza kutoka kwao.

Danieli 7:25 inatuambia kwamba pembe ndogo ingetawala kwa wakati, nyakati mbili na nusu wakati. Rejea hii ya wakati katika Ufunuo 12 inalinganishwa na siku 1260.

> Mwanamke yule akapewa mabawa mawili ya tai yule mkubwa, ili aruke, aende zake nyikani hata mahali pake, hapo alishwapo kwa **wakati na nyakati na nusu ya wakati,** mbali na nyoka huyo. — Ufunuo wa Yohana 12:14 (KJV).

> Yule mwanamke akakimbilia nyikani, ambapo ana mahali palipotengenezwa na Mungu, ili wamlishe huko muda wa **siku elfu na mia mbili na sitini**. — Ufunuo wa Yohana 12:6

Kipindi hiki cha siku 1260 kinaleta maana pale kanuni ya Kiebrania ya siku kwa mwaka inapotumika.

> Kwa hesabu ya zile siku mlizoipeleleza nchi, **siku arobaini**, kwa kila siku mtachukua hatia yenu mwaka mmoja, ***ndiyo*** **miaka arobaini**, nanyi mtajua kukataa kwangu. — Hesabu 14:34

> Tena utakapozitimiza hizo, utalala kwa ubavu wako wa kuume, nawe utauchukua uovu wa nyumba ya Yuda; siku arobaini, **siku moja kwa mwaka mmoja, nimekuagizia.** — Ezekieli 4:6

Wakati wa utawala wa Upapa ulikuwa kutokea 538AD hadi 1798 AD, wakati Wafaransa walipomchukua Papa mateka, na kumaliza nguvu ya muda wa Upapa. Ilikuwa muda mfupi baada ya muda huu ambapo hukumu ilikuwa ianze. Ili kupata muda hususani zaidi, tunafungua Danieli sura ya 8 na kulinganisha mfuatano wa historia hapo na ule wa Danieli 2 na Danieli 7.

Maono ya Danieli 8 yanatupatia mgongano kati ya kondoo dume na mbuzi. Mbuzi mwenye pembe mashuhuri anamponda kondoo-dume, na kuchukua nafasi yake kwa nguvu. Pembe ya awali ya mbuzi inavunjika na pembe nne kuchukua mahali pake, na kisha kutoka kwenye mojawapo ya zile pembe nne pembe ndogo inatokea.

Hatuna shaka kwamba kondoo na mbuzi ni nani kwa sababu malaika Gabrieli anamwambia Danieli:

> **Yule kondoo mume uliyemwona**, mwenye pembe mbili, hao ni wafalme wa **Umedi na Uajemi**. Na **beberu ni ufalme wa Ugiriki (Uyunani).** Pembe kubwa iliyo katikati ya macho yake ndiye mfalme wa kwanza [akiwa Alexanda Mkuu]. — Danieli 8:20-21

Baada ya Alexanda Mkuu kufa, Ugiriki iligawanyika na kuwa mataifa manne, yakitawaliwa na majenerali wake wanne (pembe zinawakilisha watawala, au mamlaka). Tunajua kwamba pembe ndogo iliyotoka katika moja ya pembe za mbuzi ilikuja kuwa kubwa kuliko Ugiriki yenyewe, ambayo ilikuwa na nguvu zaidi kuliko Umedi na Uajemi, kwa sababu inasema:




Kuna mamlaka moja tu iliyofuata baada ya Ugiriki na ilikuwa kubwa kuliko Ugiriki - Rumi. Rumi ilitoka katika mojawapo ya mataifa manne yaliyofuata Ugiriki kwa kuwa iliiteka Makedonia kwanza, na kupanuka kutokea huko.

Pembe hii ndogo ilijitukuza dhidi ya Mkuu wa Jeshi, ambaye ni Masihi Yesu Kristo. Rumi ilimsulubisha Kristo na kutimiza unabii huu. Pembe hii ilitupa ukweli chini na kufanya mambo mengi ya kutisha. Danieli anashangazwa na yale ambayo pembe hiyo ndogo inayasema. Kisha Danieli anasikia mazungumzo kati ya viumbe wawili watakatifu kuhusu muda ambao mchakato huu wa kukanyaga watu wa Mungu na Patakatifu ungeendelea. Jibu lililotolewa lilikuwa kama ifuatavyo:

> Akamwambia, "Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakaswa." — Danieli 8:14

Tunapolinganisha Danieli 7 na Danieli 8 tunapata uhusiano wa kuvutia sana kati ya hukumu inayofanyika katika Danieli 7 na kutakaswa kwa Patakatifu katika Danieli 8.

| Danieli 7 | Tukio | Danieli 8 |
| --- | --- | --- |
| Simba | Babeli | - |
| Dubu | Umedi na Uajem | Kondoo |
| Chu | Uyunani | Mbuzi |
| Mnyama | Rumi | Pembe Ndogo |
| Mandhali ya Hukumu | **Hukumu** | **Kutakaswa kwa Hekalu** |
| Ufalme wa Kristo | Ujio wa pili | Kuvunjwa bila kazi ya mikono ya Mwanadamu |

Je, kuna ulinganifu gani kati ya kutakaswa kwa Patakatifu na hukumu? Utakaso wa Patakatifu pa Wayahudi kila mwaka ulifanyika wakati wa sikukuu ya Siku ya Upatanisho.

> Amri hii itakuwa amri ya milele kwenu; katika mwezi wa saba, siku ya kumi ya mwezi, mtajitaabisha roho zenu, msifanye kazi ya namna yo yote, mzalia na mgeni akaaye kati yenu. Kwa maana siku hiyo upatanisho utafanywa kwa ajili yenu, ili kuwatakasa; nanyi mtatakaswa na dhambi zenu zote mbele za BWANA. — Mambo ya Walawi 16:29-30

> Lakini siku ya kumi ya mwezi huo wa saba ni siku ya upatanisho; itakuwa kusanyiko takatifu kwenu, nanyi mtazitesa nafsi zenu; nanyi mtasongeza sadaka kwa BWANA kwa njia ya moto. — Mambo ya Walawi 23:27

Watu waliamriwa "kuzitesa nafsi zao", (yaani wajichunguze kwa kina ili kuona kama kulikuwa na dhambi yoyote ambayo haijaungamwa, au kitu chochote ambacho kingewatenganisha na Mungu.) Siku ya Upatanisho ilikuwa pia

siku ya hukumu kwa watu. Haikuwa tu huduma kwa ajili ya mtu binafsi, (dhabihu za kila siku katika mwaka zilishughulikia hilo), bali ilikuwa ni kwa ajili ya kuondolewa kwa mwisho kwa dhambi mwishoni mwa mwaka. Kwa njia ya damu alipokea msamaha kutoka kwenye dhabihu muda wa mwaka mzima, na hatia yake ilikuwa imehamishwa kwa njia ya mfano kutoka kwake hadi Patakatifu. Siku ya Upatanisho dhambi zote zilizokuwa katika Patakatifu zilishughulikiwa. Dhambi yoyote ambayo haijaungamwa katika Siku ya Upatanisho ingemfanya mwenye dhambi kuwa na hatia, na angebeba adhabu ya dhambi yake mwenyewe. Mwenye dhambi alikuwa ametakaswa kila siku kwa mwaka mzima, lakini Patakatifu palikuwa bado kwa njia ya mfano kubeba dhambi za watu. Sasa, katika Siku ya Upatanisho, Patakatifu penyewe palipaswa kutakaswa.

Kuna maelezo mengi zaidi ambayo tunaweza kuyatoa, lakini jambo kuu hapa ni kwamba utakaso wa Patakatifu ni kazi ya hukumu iliyotokea siku ya 10 ya mwezi wa saba wa Kiyahudi iitwayo Siku ya Upatanisho au Yom Kippur.

Kutokana na hili tunaweza kuanza kubainisha ni lini wakati huu wa hukumu ungeanza, kwa sababu mazungumzo kati ya hao viumbe wawili watakatifu yalionyesha kwamba ingechukua siku 2300. Danieli alizimia baada ya kusikia kwamba maono hayo yangekuwa ya siku nyingi, kabla Gabrieli hajamweleza Danieli mwisho wa zile siku 2300. Mwitikio wa Danieli kwa taarifa hii unaonyesha kwamba alielewa kwamba ilikuwa ni muda mrefu zaidi ya siku halisi 2300 au miaka 6.3 tu, muda mfupi sana ambao Danieli angeshangilia kuusikia. Mwisho wa Danieli 8 unamalizia kwa Danieli kutoelewa unabii wa miaka 2300, muda mrefu usiowazika ambao ulimwacha Danieli "mgonjwa siku nyingi."

Katika sura inayofuata, Danieli anaanza kusali kwa bidii. Wakati wa maombi haya ni miaka kadhaa baada ya maono katika Danieli 8. Danieli anaomba sala nzuri sana na kumwomba Bwana amsamehe yeye na watu wake. Kisha Gabrieli anamwendea Danieli ili kumpa ufahamu wa maono ambayo alikuwa ameona hapo awali lakini hakuelewa.

> …naam, nilipokuwa nikinena katika kuomba, mtu yule, Gabrieli, niliyemwona katika njozi hapo kwanza, akirushwa upesi, alinigusa

> panapo wakati wa dhabihu ya jioni. Akaniagiza, akaongea nami, akasema, Ee Danieli, **nimetokea sasa, ili nikupe akili upate kufahamu.** Mwanzo wa maombi yako ilitolewa amri, nami nimekuja kukupasha habari; maana wewe unapendwa sana; **basi itafakari habari hii, na kuyafahamu maono haya.** — Danieli 9:21-23

Gabriel anatanguliza unabii wa wakati mpya wa majuma 70 uliogawanywa katika sehemu 3. Majuma 7 kukamilisha hekalu. Majuma 62 zaidi hadi Masihi aje na kisha juma 1 la mwisho. Majuma 70 kwa mara nyingine tena yanatumia kanuni ya siku kwa mwaka. Jambo la muhimu katika unabii huu ni kwamba tumepewa muda wa kuanzia.

> Basi ujue na kufahamu, ya **kuwa tangu kuwekwa amri ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu hata zamani zake masihi aliye mkuu**; *kutakuwa* na majuma saba; na katika majuma sitini na mawili utajengwa tena pamoja na njia kuu zake na handaki, naam, katika nyakati za taabu. — Danieli 9:25


Amri ya kurejesha na kujenga upya Yerusalemu ilikuja katika amri tatu kutoka kwa wafalme watatu wa Uajemi, na hii imeandikwa katika kitabu cha Ezra.

> Nao wazee wa Wayahudi wakajenga, wakafanikiwa, kwa msaada wa kuhubiri kwao Hagai nabii, na Zekaria mwana wa Ido. Wakajenga, wakaimaliza kazi yao, kwa maagizo ya Mungu wa Israeli, **na kwa amri ya Koreshi, na Dario, na Artashasta mfalme wa Uajemi.** — Ezra 6:14

Amri mbili za kwanza zilihusisha tu ujenzi wa hekalu, lakini amri ya Artashasta ilihusisha kurejesha Yerusalemu yote na kuwapa uhuru kamili wa kujitawala wenyewe kulingana na sheria ya Mungu. Amri hii ilitolewa mnamo 457 KK. Tunapoweka habari hizi zote pamoja, tunaweza kuzionyesha kama inavyoonyeshwa kwenye ukurasa wa mwisho wa sura hii.

Habari hii ni ya kiufundi kidogo, lakini lengo la mchakato huu ni kuonyesha kutoka kwenye unabii wa Danieli kwamba kuna wakati uliowekwa wa mchakato wa hukumu kabla ya kuja kwa Kristo. Mandhari ya hukumu ya

Danieli 7 yanapohusishwa na unabii wa Danieli 8 na 9 huanza mwaka wa 1844. Hapo ndipo vitabu vinapofunguliwa na hukumu kuwekwa. 1844 huanza kile ambacho kingechukuliwa kuwa nyakati za kweli za mwisho, ambapo hakuna tena unabii wa wakati - mambo yanafungwa. Cha kuvutia zaidi, huu ndio wakati ambao Mapinduzi ya Viwanda huanza, na tunaweza kuona kwamba mambo mengi yamebadilika katika miaka 150 iliyopita kuliko miaka 1800 kabla ya 1844. Hajawahi kamwe mwanadamu kuwa na uwezo wa kuangamiza kabisa ulimwengu anaoishi.




Wakati huu baada ya 1844 ndio unaorejelewa katika maandishi haya yafuatayo:

> Lakini wewe, Ee Danieli, yafunge maneno haya, ukakitie muhuri kitabu, hata wakati wa mwisho; **wengi wataenda mbio huko na huko, na maarifa yataongezeka**. — Danieli 12:4

Wakati huu pia unatangazwa na Ujumbe wa Malaika wa Kwanza wa Ufunuo 14.

> Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa, akasema kwa sauti kuu, "**Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu**


> **yake imekuja**. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji.” — Ufunuo wa Yohana 14:6-7

Swali kuu linalopaswa kuibuliwa katika kujibu haya yote ni: kwa nini Mungu anaonyeshwa akiwa anaendesha eneo la mahakama akiwa na vitabu na kutoa hukumu kwa watu wakati Yesu anasema kwamba Baba Yake wala Yeye mwenyewe hamhukumu yeyote? Yesu anatuuliza swali:

> Akamwambia, Mtu wewe, ni nani aliyeniweka mimi kuwa mwamuzi au mgawanyi juu yenu? — Luka 12:14

# Muda wa Hukumu

Kulingana na Danieli 8:14 na 9:24-27



SURA YA 16

# Umeuacha Upendo Wako wa Kwanza

Usiku kabla ya Yesu kufa, tunapata mazungumzo ya kuvutia yakifanyika miongoni mwa wanafunzi.

> **Yakatokea mashindano kati yao, kwamba ni nani anayehesabiwa kuwa mkubwa.** Akawaambia, "Wafalme wa Mataifa huwatawala, na **wenye mamlaka juu yao huitwa Wenye fadhili;** lakini kwenu *ninyi sivyo*; bali aliye mkubwa kwenu na awe kama aliye mdogo; na mwenye kuongoza kama yule atumikaye." — Luka 22:24-26

Hebu fikiria huzuni ya Kristo alipokuwa akiwasikiliza wanafunzi wake wakibishana kuhusu ni nani kati yao anayepaswa kuonwa kuwa mkuu zaidi. Hili linaonyesha kwamba wanafunzi wote walikuwa wakitoa hukumu juu ya kila mmoja wao kuhusu ni nani anayepaswa kuhudumu katika nyadhifa za juu zaidi. Wamepofushwa kabisa na mateso ambayo Yesu tayari anaanza kuyahisi, na kutojua kwa makusudi kile ambacho kilikuwa karibu kufunuliwa.

Baadaye usiku huo Yesu anapojaribu kwa bidii kumwamsha Petro kutoka kwenye hatari yake, tena Petro anajilinganisha na wengine, hivyo kupitisha hukumu juu yao.

> Petro akajibu, "Hata kama wote wataanguka kwa ajili yako, mimi sitaanguka." — Mathayo 26:33 ( NIV)

Ikiwa wafuasi wa karibu zaidi wa Yesu bado walikuwa wamejawa na roho hii ya kuwahukumu wengine kuwa wenye hali ya chini kuliko wao wenyewe, inakuwa dhahiri kwamba suala hili la kuhukumu wengine limejikita sana katika moyo wa mwanadamu.

Baada ya kusulubishwa na kufufuka kwa Kristo wanafunzi walibadilishwa kabisa. Walijinyenyekeza mbele ya Mungu na kila mmoja na mwenzake na kupokea kumwagwa kwa Roho siku ya Pentekoste.

> Hata ilipotimia siku ya Pentekoste **walikuwako wote mahali pamoja**. Ghafla, sauti ikatoka mbinguni, kama sauti ya upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi." — Matendo 2:1-2 (KJV).

Tunasoma maneno ya Petro baada ya wakati huu.

> lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia, si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo. Wala si kama wajifanyao mabwana juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya vielelezo kwa lile kundi. — 1 Petro 5:2-3

Jaribu la kutumia mamlaka juu ya wengine katika mchakato wa hukumu linaweza kutupata kwa urahisi, hasa wakati kanisa linapopitia changamoto ya mafundisho ya uongo. Kanisa la Efeso lilikabiliwa na changamoto kubwa juu ya suala la mafundisho, na tunaona maneno ya Yesu kuhusu hali hii.

> Nayajua matendo yako, na taabu yako, na subira yako, na ya kuwa huwezi kustahimili wabaya; **tena umewajaribu wale wajiitao mitume, nao sio, ukawaona kuwa waongo;** — Ufunuo 2:2 KJV)

Neno kuwajaribu lina maana ya kupima na kuchunguza. Viongozi wa kanisa la Efeso waliwajibu wale waliofundisha makosa kwa roho ya uchunguzi na hukumu. Viongozi hao walifanikiwa kuuzuia uzushi uliokuwa ukitaka kuingia kanisani, lakini walifanya hivyo kwa gharama kubwa.

> Lakini nina neno juu yako, ya kwamba **umeuacha upendo wako wa kwanza**. Basi, kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu,

> ukayafanye matendo ya kwanza. Lakini, usipofanya hivyo, naja kwako, nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu. — Ufunuo wa Yohana 2:4-5

Katika kutafuta kulitakasa kanisa dhidi ya makosa, viongozi walipoteza upendo wao wa kwanza. Jinsi ilivyo rahisi kuanza kuonya dhidi ya watu wanaoshikilia mawazo tunayojua kuwa ya uongo. Ni kweli kwamba tunahitaji kusema ukweli na kuutofautisha na makosa, lakini tunapoanza kuwatenga watu tunaweza kuanza kupoteza upendo wetu kwao. Tunaanza kutoka kwenye upendo wa kwanza wa kuhubiri injili hadi kujikita kwenye kujitetea mara kwa mara dhidi ya uzushi. Tunaona mwelekeo huu katika kanisa la awali pamoja na wingi wa vitabu vinavyoitwa "Dhidi ya ______". Baadhi ya mifano ni pamoja na *Dhidi ya Wapagani, Dhidi ya Manichaeans, Dhidi ya Marcion, Dhidi ya Sabellians, Dhidi ya Aunomius, Dhidi ya Vigilantius, nk*.

Kupotea kwa upendo wa agape katika kanisa la Efeso lilikuwa pigo baya sana kwa kanisa. Jumbe kwa yale makanisa saba hazikuandikwa kwa makanisa ya mahali hapo tu wakati huo, bali pia zilikuwa unabii wa kanisa katika vipindi vya nyakati vilivyofuatana tangu enzi ya Mitume hadi siku hizi. Tunajua hili kwa sababu kulikuwa na zaidi ya makanisa saba huko Asia. Fragia, Pamfilia, Galatia, Ponto na Kapadokia yalikuwa pia ni makanisa huko Asia. Makanisa saba yalichaguliwa kwa sababu yaliwakilisha kanisa la Kikristo katika nyakati zote tangu wakati wa Kristo.

> Heri asomaye na wao wayasikiao maneno ya unabii huu, na kuyashika yaliyoandikwa humo; kwa maana wakati u karibu. — Ufunuo wa Yohana 1:3

Yohana anarejelea kitabu kizima kama unabii na si tu kuanzia kwenye mihuri saba na kuendelea. Neno saba lenyewe ni ishara katika Biblia ya utimilifu au ukamilifu. Hapa kuna mfano mmoja:

> Na siku ya saba Mungu alimaliza (kukamilisha/kumaliza) kazi yake yote aliyoifanya, akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya. — Mwanzo 2:2

Kwa hiyo, makanisa saba yanawakilisha historia kamili au iliyokamilika ya kanisa duniani tangu Kristo alipokuja mara ya kwanza hadi ajapo mara ya pili. Ukiongeza katika hili mihuri saba inawakilisha mchakato kamili wa kutia muhuri kanisa la Mungu katika kipindi hicho hicho. Tazama mwendelezo ufuatao wa mawazo katika makanisa.

| Kanisa | Maana | Mwendelezo wa Hukumu |
|---|---|---|
| 1 Efeso *(31-100 BK)* | Kutamanika | **Na umewajaribu wale wanaosema kuwa** ni Mitume na sio, na kuwaona ni waongo. Ufunuo 2:2 |
| 2 Smirna *(100-313)* | Manukato mazuri Wakati wa mateso | Usiogope mambo yatakayokupata. Hakika **Ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe,** Ufunuo 2:10 |
| 3 Pergamo *(313-538)* | Ndoa Halisi | Nayajua matendo yako, na ukaapo, ndipo penye **kiti cha Shetani**: Ufunuo 2:13 |
| 4 Thiatira *(538-1519)* | Kuvunjilia mbali | Naye ashindaye, na kuyashika matendo yangu hata mwisho, **nitampa mamlaka juu ya mataifa, naye atawachunga kwa fimbo ya chuma; kama vyombo vya mfinyanzi vitavunjwa vipande vipande**; kama mimi nilivyopokea kwa Baba yangu. Ufunuo 2:26-27 |
| 5 Sardi *(1519-1798)* | Mambo Yaliyosalia | Yeye ashindaye atavikwa mavazi meupe; **wala sitalifuta jina lake katika kitabu cha uzima**, bali nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu, na mbele ya malaika zake. Ufunuo 3:5 |

| | | |
|---|---|---|
| **6** Filadelphia *(1798-1844)* | Upendo wa kindugu | Tazama, nakupa watu wa sinagogi la Shetani, wasemao kwamba ni Wayahudi, nao sio, bali wasema uongo; tazama, **nitawafanya waje kusujudu mbele ya miguu yako**, na kujua ya kuwa mimi nimekupenda wewe." Ufunuo 3:9 |
| **7** Laodikia *(1844-Sasa)* | Hukumu ya watu | Kwa sababu wasema, Mimi ni tajiri, nimekuwa tajiri, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe ni mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi - Ufunuo 3:17 |

Inashangaza sana kwamba katika kanisa la Efeso viongozi walikuwa wakiwachunguza na kuwahukumu wengine na roho hii ilionyeshwa tena kwa kanisa katika enzi iliyofuata ambapo kanisa lilijaribiwa na kuhukumiwa na ulimwengu. Neno lile lile la Kiyunani linatumika kuhusiana na makanisa haya yote mawili. Je, roho ya kuwahukumu wengine ilikuwa imetoa mwanya katika kanisa ambao uliwaruhusu kukabiliana na yale waliyokuwa wameanza kuwatendea wengine? (Ona Mathayo 7:1)

Kutokana na mateso ya kanisa wakati wa enzi ya Smirna, kanisa lilikuwa tayari kuafikiana na kupewa kiti kwenye meza ya Rumi. Pergamo inamaanisha ndoa halisi, na kanisa na serikali kuunganishwa pamoja wakati wa enzi hii na kuanza kuketi kwenye kiti cha hukumu cha Shetani. Hii ilifungua njia kwa Shetani kuanzisha kiti chake cha hukumu ndani ya kanisa katika enzi ya tatu ya historia ya kanisa la Kikristo.

Pamoja na kiti cha hukumu cha Shetani kikiwa kimeanzishwa, kanisa wakati wa enzi za giza liliikumbatia roho ya hukumu kiasi kwamba Kristo anazungumza nao kama amepewa mamlaka juu ya mataifa, kuwatawala kwa chuma na kuwaponda wale wanaopinga mamlaka yao. Watu wengi wa kweli wa Mungu walishutumiwa na kuhukumiwa kifo wakati huu. Roho ya kuhukumu, kushutumu na kuua ilikuwa imelitawala kanisa la Kikristo kabisa katika enzi hii.

Huu ndio muktadha wa Danieli 7 na maneno makuu ambayo pembe ndogo inayazungumza.

> Nikaziangalia sana pembe zake, na tazama, pembe nyingine ikazuka kati yao, nayo ilikuwa ndogo, ambayo mbele yake pembe tatu katika zile za kwanza zikang'olewa kabisa; na tazama, katika pembe hiyo mlikuwa na macho kama macho ya mwanadamu, na kinywa kilichokuwa kikinena maneno makuu. — Danieli 7:8

> Nikatazama, na pembe iyo hiyo ilifanya vita na watakatifu, ikawashinda; hata akaja huyo mzee wa siku, nao watakatifu wake Aliye juu wakapewa hukumu; na majira yakawadia watakatifu waumiliki ufalme. — Danieli 7:21-22

Muktadha wa hukumu kuanzia 1844 ni jibu kwa mashtaka yaliyowekwa dhidi ya watu wa Mungu na nguvu ya ile pembe ndogo iliyotawala kutoka kwenye kiti cha Shetani. Hukumu ya Mungu kwa hakika ni uthibitisho wa watu wake dhidi ya shutuma zinazoletwa na Shetani kupitia viongozi wa kanisa. Viongozi wa Kiyahudi walikuwa wamemhukumu mwanamke aliyekamatwa katika uzinzi na kumleta kwa Yesu ili kuchunguza kesi hiyo, na badala yake Yesu aligeuzia hukumu juu yao. Vivyo hivyo, baada ya kanisa kuwahukumu watu wengi sana kifo, Mzee wa Siku anarudisha hukumu juu ya kanisa. Ni akina nani walioona rehema mbele ya Yesu miaka elfu mbili iliyopita, na ni akina nani walioachwa wakifikiri wakiwa wamehukumiwa? Ni nani anayeona rehema katika hukumu ya Mzee wa Siku katika mwisho wa nyakati, na ni nani anayejiona kuwa amehukumiwa?

> Hukumu ya Mungu ni kuwatetea watu wake kutokana na mashtaka waliyowekewa na Shetani kupitia viongozi wa kanisa.

Kwa wale walio na imani ya Yesu na kuona wema wa Baba kupitia macho ya Mwanawe, hukumu ya Mungu haihusu Mungu kuwahukumu watu wa Mungu bali ni kuwatetea kutokana na mashtaka waliyowekewa na Shetani kupitia viongozi wa kanisa. Mungu anaruhusu hukumu hiyo itendeke kwa sababu inafichua yaliyo mioyoni mwa watu wa Mungu wanaposhtakiwa na Shetani kupitia mawakala wake. Je, watu wa Mungu wanamwamini Mungu

kupitia mchakato huu wa hukumu, au wanakatisha tumaini lao kwa Mungu kuwaongoza katika majaribu makali?

Baada ya karne nyingi za mateso, watu wa Mungu wanalia ili kulipiza kisasi juu ya adui zao kwa sababu ya yale waliyotendewa. Hili limetajwa katika muhuri wa 5 unaofanana na kanisa la 5 la makanisa saba.

> ....Nikaona chini ya madhabahu roho zao waliouawa kwa ajili ya neno la Mungu,… wakalia kwa sauti kuu, wakisema, Ee Bwana, mtakatifu na wa kweli hata lini usitake kuhukumu na kulipiza kisasi damu yetu juu yao wakaao juu ya nchi? — Ufunuo 6:9-10 (KJV)

Kanisa liliteseka sana na mamilioni walikufa. Bado roho ya kisasi ilibaki kati ya watu wa Mungu, na shauku kwa ajili ya Mungu kuwaangamiza adui zao. Tukitazama nyuma kwenye historia hii tunafahamu zaidi tabia ya moyo wa mwanadamu. Watetezi wa kwanza katika kanisa wa kutumia nguvu kudhibiti mawazo ya binadamu, kama Augustine, hakika hawakuweza kufikiria jinsi mchakato waliouanzisha ambavyo ungekuwa wa giza na wa kutisha. Tulihitaji historia hii ili kujifunza kutokana na kuona jinsi asili yetu ya kimwili na ya kinyama na isiyo na huruma inavyodhihirishwa.

Mungu hangetuambia tu kwamba hivi ndivyo tulivyokuwa, kwa maana hatungemwamini na hatungemwelewa, kama mtoto ambaye hawaamini wazazi wake na anahitaji kugusa kitu cha moto kabla ya kukubali kwamba kitamuunguza. Hii ndiyo sababu Mungu aliruhusu mbegu ya dhambi kukua: ili ulimwengu wote upate kuona maendeleo yake na kuelewa matunda yake, na kujua kwamba hakuna jambo chanya katika kufanya dhambi na hakuna uhalali wa madai ya Shetani dhidi ya sheria na serikali ya Mungu. Hivyo ndivyo Mungu "atakomesha kabisa; taabu haitainuka mara ya pili." (Nahumu 1:9)

Kanisa la Filadelfia liliitwa kanisa la upendo wa kindugu. Lilikuwa ni kanisa dogo na dhaifu lililofuata ukweli, lakini ndani yake kulikuwa na upendo mwingi. Maneno ya Yesu kwao – "Nitawafanya waje kusujudu mbele ya miguu yako," - yanazungumzia shauku yao ya kutambuliwa na kuthaminiwa. Unapokuwa mdogo, mnyonge na mwenye kukandamizwa, jaribu la

kutambuliwa huongezeka. Yesu anawatia moyo wale walio katika Filadelfia katika lugha wanayoelewa. Maadui zao watanyenyekea mbele yao na mabaya waliyoyapata yatarekebishwa. Ni lugha ya hukumu.

Watu katika kipindi cha kanisa la Filadelfia, ambalo lilifika hadi 1844, hawakuelewa kile kilichokuwa mioyoni mwao. Walielewa kusafishwa kwa Patakatifu katika tarehe hiyo kumaanisha Yesu angerudi na kuhukumu ulimwengu - hatimaye Mungu angewalipizia kisasi kama walio sahihi na waovu kama wasio sahihi, na wale waliowatesa na kuwakataa wangeadhibiwa. Pale ambapo haya hayakutokea katika Siku ya Upatanisho ya 1844, kundi hili kubwa la watu, lililoitwa Waadventista, walikatishwa tamaa sana; tukio hili lilijulikana kama "Kukatishwa tamaa." Kwa jinsi walivyotambua kwamba Mungu angelitenda wakati huo katika mwaka wa 1844, Mungu alitaka watafakari juu ya tabia yao ya kuhukumu, lakini cha kusikitisha, wengine walikatisha imani na bado wengine wakabawa na kasoro hii ya tabia iliyokuwa ndani kabisa ya moyo wa mwanadamu na kubaki bila kuponywa. Iliachwa kwa kanisa la mwisho kwa mbegu hii kudhihirishwa kikamilifu na kushughulikiwa katika ubinadamu.

Kanisa la mwisho ni Laodikia, ambalo linamaanisha kuhukumu watu - ni kanisa la hukumu. Urithi wa kibinadamu wa kuhukumu na kulaani unafikia kilele katika kanisa hili. Mungu anatuma ujumbe kwa ulimwengu wakati huu akitangaza kwamba hukumu imeanza. Mungu anaonyeshwa akipanda kiti cha hukumu ili kupata kumbukumbu za maisha za wale wote wanaodai kumwamini Kristo.

Watu wa Mungu wanaonaje hukumu hii? Inategemea jinsi wanavyoelewa tabia ya Mungu. Ikiwa wanaona Mungu kama mwendesha mashtaka anayepitia rekodi ili kufuta wale ambao hawakufikia viwango, basi kwa kawaida watachukua tabia kama hii wakati wa kushughulika na wanadamu wenzao. Kanisa hili linajihukumu lenyewe kuwa "tajiri na limeongezeka kwa mali" na linajiona kuwa bora kuliko wengine.

Kutokana na roho hii ya hukumu, ni lazima Bwana atufunulie yale yaliyo mioyoni mwetu kwa kuturuhusu kudhihirisha kwake tabia ya Hakimu ambayo itawahukumu na kuwaangamiza wale wanaoikataa kweli kama vile waaminifu wanavyoielewa. Wakati huo huo wale wanaojua tabia ya kweli ya

Mungu wataamini kwamba Mungu ndiye mtetezi wao dhidi ya shutuma za Shetani. Mashtaka haya ama yanafanywa moja kwa moja dhidi yao kwa kuwaambia wao ni wadhambi wasio na tumaini na hawatashinda kamwe, au yanatolewa kupitia kwa wale walio katika kanisa ambao wanaona nuru mpya juu ya tabia ya Mungu kama tishio.

Matukio ya hukumu kutoka 1844 ni kwa ajili ya watakatifu wa Mungu kujiona wenyewe na kile hasa kilicho katika mioyo yao. Inafichua kwamba hili ndilo tunalotamani kiasili na kwamba huu ndio mchakato tunaofikiri unahitajika ili kumaliza pambano kuu.

Ukweli ni kwamba kuanzia 1844, ni tabia ya Mungu ambayo inahukumiwa hasa. Maneno ya Ufunuo 14:7 yanaweza kusomwa kwa njia mbili:

> … wakisema kwa sauti kuu, "Mcheni Mungu na kumtukuza, **kwa maana saa ya hukumu yake imekuja;** na kumwabudu yeye aliyezifanya mbingu na nchi, na bahari na chemchemi za maji." — Ufunuo 14:7

Saa ya hukumu yake imekuja! Nani anafanya hukumu? Mungu au sisi? Yesu anatuambia kwamba Mungu hamhukumu mtu ye yote, hivyo basi ni sisi tunaohukumu, na tunapomhukumu Mungu kuwa yuko hivi au vile ndivyo tutakavyoona hukumu yake kuwa juu yetu wenyewe.

> Vipi ikiwa wengine hawakuamini? Je! kutokuamini kwao kutaibatilisha imani ya Mungu? Mungu na awe kweli, na kila mtu ni mwongo; kama ilivyoandikwa, **ili upate kuhesabiwa haki katika maneno yako, na kushinda uhukumiwapo.** — Warumi 3:3-4 (KJV)

Je, unamhukumu Mungu namna gani? Je, Mungu anahukumu, anashutumu na kuwaua watu? Au je, anafanana na Yesu ambaye ni mwenye rehema, mwenye neema, anayewapenda adui zake na kuwatendea mema wale wanaomchukia? Kama uhukumuvyo…

SURA YA 17

# Mto Unaong'aa au Mwali wa Moto?

Danieli 7 hutimiza jukumu muhimu sana katika kumwona Mungu kama Hakimu anayewahukumu na kuwaangamiza wale wanaofanya uovu. Maono katika sura hii yanaelezea mfuatano wa falme zinazotawala ulimwengu na kuwashinda wapinzani wao. Kisha tunatambulishwa nguvu ya pembe ndogo inayoibuka kutokea Rumi ambayo tuliielezea katika sura mbili zilizopita.

> Nikaziangalia sana pembe zake, na tazama, pembe nyingine ikazuka kati yao, nayo ilikuwa ndogo, ambayo mbele yake pembe tatu katika zile za kwanza zikang'olewa kabisa; na tazama, katika pembe hiyo mlikuwa na macho kama macho ya mwanadamu, **na kinywa kilichokuwa kikinena maneno makuu.** — Danieli 7:8

Ni yapi baadhi ya mambo makuu ambayo pembe ndogo iliyasema?

> Papa ana hadhi kuu na ameinuliwa sana kiasi kwamba yeye si mwanadamu tu, bali kana kwamba ni Mungu, na mwakilishi wa Mungu. …(imetafsiriwa kutoka kwa Lucius Ferraris, "Papa II," Prompta Bibliotheca, Vol. VI, pp. 25–29).

> Petro na waandamizi wake wana uwezo wa kuweka sheria zenye kanuni na zinazokataza, uwezo vivyo hivyo kutoa maongozi kutoka kwa sheria hizi, na, inapohitajika kuzibatilisha. **Ni wao**

> **ambao huhukumu makosa dhidi ya sheria, kuweka na kutoa adhabu. Mamlaka hii ya kuhukumu itajumuisha hata uwezo wa kusamehe dhambi.** Kwa maana dhambi ni uvunjaji wa sheria za ufalme usio wa kawaida, na iko chini ya ufahamu wa waamuzi wake waliowekwa. The Catholic Encyclopedia, Vol XII, art, "Pope," ukurasa wa 265.

Mapapa walidai kuwa Mungu duniani na walidai uwezo wa kuwahukumu na kuwashutumu wale waliokiuka sheria zao. Katika kipindi cha zama za giza, Upapa, kupitia mamlaka yake ya uchunguzi, ulichukua ufuatiliaji na hukumu ambayo ilisababisha hukumu ya vifo vya mamilioni ya watu katika nchi nyingi alizozitawala.

Mtazamo wa kanisa la Kirumi juu ya Mungu ulikuwa wa hukumu kwa wale ambao hawakufuata kanuni ya imani kama walivyoifafanua. Mwishoni mwa kipindi hiki cha ukuu wake ambapo "aliwatesa watakatifu wake Aliye Juu Zaidi," ( Danieli 7:25 ) maono yanabadilika na kuwa na mtazamo wa mbinguni.

> Nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa, na mmoja aliye mzee wa siku ameketi; mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa chake kama sufu safi; kiti chake cha enzi kilikuwa miali ya moto, na gurudumu zake moto uwakao. **Mto kama wa moto** ukatoka ukapita mbele zake; maelfu elfu wakamtumikia, na elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele zake; hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa. — Danieli 7:9-10

Tunaona taswira ya eneo la mahakama na vitabu vya kumbukumbu vinafunguliwa kwa ajili ya uchunguzi na malaika wote wa mbinguni wamekusanyika kushuhudia tukio hili. Maono hayo hayarekodi hata neno moja la Mzee wa Siku. Yanahamia tu kwenye tukio linalofuata.

> Nikatazama wakati huo; kwa sababu ya sauti ya yale maneno makubwa iliyoyasema ile pembe; nalitazama hata mnyama yule akauawa, mwili wake ukaharibiwa, akatolewa ateketezwe kwa moto. Na kwa habari za wale wanyama wengine,

> walinyang'anywa mamlaka yao; walakini maisha yao yalidumishwa kwa wakati na majira. — Danieli 7:11-12

Inaonekana kana kwamba Mungu amekwisha hukumu na kuadhibu matendo ya pembe ndogo, na kisha kuiharibu na kuiteketeza kwa moto.

Kwa kuwa Baba hasemi chochote, tunaalikwa kutambua tabia ya Baba hapa. Ni sawa na jinsi Yesu alivyowashughulikia wanafunzi wake.

> Na tazama, mwanamke Mkananayo wa mipaka ile akatokea, akampazia sauti akisema, Unirehemu, Bwana, Mwana wa Daudi; binti yangu amepagawa sana na pepo. Wala **yeye hakumjibu neno.** Nao wanafunzi wake wakamwendea, wakamwomba, wakisema, Mwache aende zake; kwa maana anapiga kelele nyuma yetu. — Mathayo 15:22-23

Yesu aliponyamaza kimya kumjibu yule mwanamke Mkanaani, wanafunzi walitafsiri ukimya huo kuwa hukumu dhidi ya mwanamke huyo. Tukio hili lilitabiriwa kwa maneno haya:

> Umekaa na kumsengenya ndugu yako, Na mwana wa mama yako umemsingizia. Ndivyo ulivyofanya, **nami nikanyamaza; Ukadhani ya kuwa Mimi ni kama wewe.** Walakini nitakukemea; Nitayapanga hayo mbele ya macho yako. — Zaburi 50:20-21

Yesu alikaa kimya ili tabia ya kweli ya wanafunzi idhihirishwe. Hiki ndicho kinachotokea katika Danieli 7. Baba yuko kimya na kisha mfululizo wa matukio unatokea. Tunaona kwamba ni kwa sababu ya maneno ya pembe ndogo kwamba mnyama hatimaye anachukuliwa na kuharibiwa.

> Nikatazama wakati huo; **kwa sababu ya sauti ya yale maneno makubwa iliyoyasema ile pembe;** nalitazama hata mnyama yule akauawa, mwili wake ukaharibiwa, akatolewa ateketezwe kwa moto. — Danieli 7:11

Pembe hii ndogo katika Danieli 7 inafananishwa na mwanamke anayepanda mnyama katika Ufunuo 17. Mwanamke anawakilisha kanisa (Yeremia 6:2), na mnyama anayempanda anawakilisha mamlaka ya serikali ya ulimwengu.

Pembe kumi ni wafalme kumi wanaotawala mwishoni mwa historia ya dunia. Mwanamke anaangamizwa vipi na ni nani anayemwangamiza?

> Na zile pembe kumi ulizoziona, na huyo mnyama, hao watamchukia yule kahaba, nao watamfanya kuwa mkiwa na uchi, watamla nyama yake, watamteketeza kabisa kwa moto. Ufunuo wa — Yohana 17:16

Tunaona pembe ndogo na mwanamke aliyempanda mnyama huyo wakiteketezwa kwa moto. Ni wafalme wa dunia wanaomwangamiza mwanamke, akiwakilisha nguvu sawa na ile pembe ndogo. Hii ina maana kwamba Mungu haiangamizi pembe ndogo. Pembe ndogo inajiangamiza yenyewe kwa maneno yake ya fahari.

> BWANA amejidhihirisha na kutekeleza hukumu; Amemnasa mdhalimu kwa kazi ya mikono yake. — Zaburi 9:16

> “Kwa sababu hiyo nimemwaga ghadhabu yangu juu yao; nimewateketeza kwa moto wa hasira yangu; nami nimeileta njia yao wenyewe juu ya vichwa vyao,” asema Bwana MUNGU. Ezekieli 22:31

Mungu anatuambia jinsi hasira yake inavyofanya kazi. Maamuzi yale yale ambayo watu binafsi, makanisa, na mataifa huyachukua yanaruhusiwa kuwarudia wale hasa wanaofanya maamuzi haya kwa wema au kwa uovu. Mungu haingilii kati kutumia nguvu, lakini badala yake anaruhusu matukio kufuata mkondo wake wa asili hadi kile ambacho mtu anakipanda, kinavunwa katika mavuno yake mwenyewe.

> Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele. — Wagalatia 6:7-8

Kama vile Mafarisayo walivyomleta mwanamke kwa Kristo kwa ajili ya hukumu na hasemi chochote ila anaandika juu ya ardhi, vivyo hivyo Mzee wa Siku katika hukumu hasemi chochote ila anaandika kimya kimya juu ya

mavumbi ya mioyo ya watu ukweli wa kile wanakichofanya ili wapate kutubu au hatimaye kuasi hadi kujiangamiza wenyewe.

Tunapotazama mandhari ya chumba cha enzi, tunamwazia Mungu akiwa amesimama akiwahukumu watenda maovu. Kwa hiyo tunaona moto utokao kwake kama mwali wa moto uliotumwa kuwa onyo kwa watenda maovu ambao wanakaribia kuulipia uhalifu wao kwa nguvu itokayo katika kiti cha enzi cha Mungu.

> Mto wa moto ukatoka na ukapita mbele yake. — Danieli 7:10

Maneno "mto wa moto" yanaweza pia kutafsiriwa kama mto unaong'aa. Wazo hili linatuunganisha na matukio mengine ya mandhari ya chumba cha enzi.

> Mbele ya kile kiti cha enzi palikuwa na **bahari ya kioo, kama bilauri.** — Ufunuo 4:6

> Kisha akanionyesha mto **wa maji ya uzima, wenye kung'aa kama bilauri**, ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu, na cha Mwana-Kondoo, — Ufunuo wa Yohana 22:1

Mto unaotiririka kutoka kwenye kiti cha enzi cha Mungu ndio mto unaong'aa wa uzima. Popote unapopita mto huu kuna uhai.

> Na itakuwa kwamba kila kiumbe chenye uhai kiendacho, popote mito iendako, kitaishi. — Ezekieli 47:9

Ukimya wa Baba katika eneo hili la chumba cha enzi unatualika kuhukumu jinsi anavyoshughulikia hali hiyo. Tunapotazama tukio hili, "saa ya hukumu yake imekuja."

(Ufunuo 14:7). Sisi ndio tunaoamua tabia yake kwa wakati huo. Je, tunamwona Baba kupitia maneno ya Mwanawe (Yohana 5:22), au tunamwona Baba kupitia asili tuliyopewa kutoka kwa Adamu; asili inayohukumu na kutoa adhabu ya kifo? (Warumi 5:16).

Tunakumbuka kama tulivyosema katika sura ya mwisho kwamba roho ya hukumu ilikuja ndani ya kanisa muda mfupi baada ya utume wa Kristo hapa

duniani. Shetani hatimaye alianzisha kiti chake cha hukumu katika kanisa na akaanza kuwahukumu na kuwashutumu waaminifu.

Matendo ya Aliye Juu Zaidi katika hukumu ni kuwatetea watu wa Mungu dhidi ya mashtaka yaliyotolewa dhidi yao na ile pembe ndogo.

> Nikatazama, na pembe iyo hiyo ilifanya vita na watakatifu, ikawashinda; **hata akaja huyo mzee wa siku, nao watakatifu wake Aliye juu wakapewa hukumu**; na majira yakawadia watakatifu waumiliki ufalme. — Danieli 7:21-22

Hukumu hiyo inaijaribu mioyo ya watu wa Mungu. Wazo la Mungu kuketi kama Hakimu linaweza kusababisha shauku ya asili ya wanadamu kuhukumu na kushutumu kuelekezwa kwa Mungu katika hukumu. Tunataka kuwahukumu na kuwaangamiza adui zetu, kwa hiyo tunadhihirisha kwamba Mungu anataka kuwahukumu na kuwaangamiza adui zake. Lakini Mungu hayuko hivi. Mungu hamshtaki mtu yeyote bali huwatetea tu watoto Wake waaminifu dhidi ya mashtaka ya Shetani.

Mungu hamshtaki mtu yeyote bali huwatetea tu watoto Wake waaminifu dhidi ya mashtaka ya Shetani.

Shetani anawashitaki mchana na usiku. Ananong'oneza tuhuma zake akilini mwao. Watakatifu wanamlilia Mungu ili waokolewe kutokana na shutuma hizi. Watu wa Mungu ama wanamlilia Mungu ili awape neema na nguvu, au wanaanza kuwahukumu na kuwashutumu wengine kama wanavyowazia Mungu atafanya kwa niaba yao. Utafanyaje katika hukumu hii?

Kwa sababu ile pembe ndogo ilihukumu na kuwashutumu wengine, maneno na matendo yake yenyewe yaliipelekea yenyewe kuhukumiwa na kushutumiwa na hatimaye kuangamizwa. Mungu hadhihakiwi. Ikiwa watu watapanda mbegu za hukumu na za kushutumu, basi hili ndilo watakalokumbana nalo. Tufuate maneno ya Yesu na tusimhukumu mtu. Kisha hatutahukumiwa (Mathayo 7:1). Uchaguzi ni wetu wa sehemu gani tutasimama katika hukumu hii.

Kama unavyohukumu…

SURA YA 18

# Lugha ya Majeshi Maovu

Kabla tu ya kufa Yesu alitamka maneno haya ya kuhuzunisha moyo:

> Eloi, Eloi, lama sabakthani? (maana yake, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?"). — Mathayo 27:46 ( NIV)

Maneno ambayo Yesu aliyasema hayakuwa ya Kiebrania bali ya Kiaramu. Hili limewafanya wengi kuamini kwamba Yesu alizungumza zaidi katika Kiaramu. Hiki kilikuwa kipengele maarufu cha filamu ya The Passion iliyoongozwa na Mel Gibson.

Kuna uthibitisho mwingi wa kuunga mkono kwamba Kiebrania kilizungumzwa sana wakati wa Kristo. Tunaona hili kutokana na ishara iliyotundikwa juu ya kichwa cha Yesu wakati wa kusulubishwa kwake pamoja na jinsi Paulo alivyohutubia baadhi ya wasikilizaji wake.

> Naye Pilato akaandika anwani, akaiweka juu ya msalaba, imeandikwa, YESU MNAZARETI, MFALME WA WAYAHUDI. Basi anwani hiyo waliisoma wengi katika Wayahudi; maana mahali pale aliposulibiwa Yesu palikuwa karibu na mji; **nayo iliandikwa kwa Kiebrania, na Kirumi, na Kiyunani.** — Yohana 19:19-20 (KJV).

> …Basi, alipompa ruhusa, Paulo akasimama madarajani, akawapungia mkono wale wenyeji; na ilipokuwa kimya kabisa, **akanena nao kwa lugha ya Kiebrania,** akisema,...Matendo ya Mitume 21:40

Yesu alipozungumza na Paulo njiani kuelekea Dameski, alizungumza naye kwa Kiebrania:

> Tukaanguka nchi sote, **nikasikia sauti ikisema nami kwa lugha ya kiebrania,** Sauli! Sauli! Mbona waniudhi? Ni vigumu kwako kuupiga mateke mchokoo. — Matendo ya Mitume 26:14

Maelezo ya maeneo kama Gabatha na Golgotha pia yako "katika lugha ya Kiebrania" (Yohana 5:2; 19:13, 17; Ufunuo 9:11; 16:16).

Kama hatua ya kuvutia, tafsiri kadhaa za kisasa zimebadilisha neno la Kigiriki kwa Kiebrania na kulitafsiri kuwa Kiaramu.

> **Sote tukaanguka chini, nami nikasikia sauti ikiniambia kwa Kiaramu,** 'Sauli, Sauli, kwa nini unanitesa? Ni vigumu kwako kuipiga teke michokoo.' — Matendo 26:14 (NIV)

Wasomi wa Lugha ya Biblia wanasawazisha badiliko hili la neno kwa msingi kwamba waliamua kwamba lugha ya Kiebrania ilikuwa tayari imeondolewa katika matumizi ya jumla na neno lugha ya Kiebrania linamaanisha tu lugha ya kawaida ambayo ilikuwa Kiaramu. Hata hivyo hii inabadilisha maana ya neno lenyewe na kukanusha marejeo ya wazi ya Kiebrania katika maandishi. Kiebrania na Kiaramu zilikuwa lugha mbili tofauti, na kunukuu Maandiko kulipaswa kufanywa kwa Kiebrania kwa sababu hapakuwa na Torati ya Kiaramu.

Hali hii inakuwa ya kuvutia zaidi unapotazama jinsi Wayahudi walivyofikiria kuhusu Kiaramu.

> Tofauti ya wazi ilifanywa, kati ya Wayahudi wenyewe, kati ya Kiebrania na Kiaramu. Sio tu kwamba Kiebrania kilikuwa chaguo la kisomi na fasihi, lakini pia kilizingatiwa kama lugha ya kawaida ya maisha ya kila siku. "Katika nchi ya Israeli," Mishnah ilisema, "kwa

nini lugha ya Kiaramu? Ama Lugha Takatifu (Kiebrania, sic) au lugha ya Kiyunani". Kiaramu hakikuwa na "fahari", na "hakikuamuru uaminifu", kama Safrai na Stern wanavyoona, wakati Kiebrania kilikuwa na vyote viwili. Hata katika nyakati za baadaye za Talmud, ilikatazwa kuitoa hati ya Kiaramu inayowaka kutoka kwenye moto siku ya Sabato, ilhali iliruhusiwa kwa hati yenye maandishi ya Kiebrania. Kuondoka kwenye ibada ya masinagogi wakati wa usomaji wa Biblia ya Kiebrania kulikatazwa, lakini si kwa usomaji wa Kiaramu. Hata kukariri Maandiko katika Kiaramu hakukutosha, ilhali kuyasikia tu katika Kiebrania, bila kuelewa neno lolote, kulikuwa "kutekeleza wajibu [wa mtu]"!

Kwa watu wa Kiyahudi, ilikuwa ni Kiebrania ambacho kilikuwa "Lugha Takatifu", ilhali Kiaramu kilionekana kuwa "lugha ya Nguvu majeshi Maovu" [Kutoka Zohar]. Sio kwamba hii ya pili ilikataliwa kabisa, lakini kwamba ilichukuliwa kama lugha ya pili baada ya Kiebrania – "lugha halisi ya mababa" na lugha ya hotuba za kawaida. Hivyo Talmud ya Yerusalemu inatangaza kwamba:

> "Lugha nne ni za thamani: Kigiriki kwa ajili ya nyimbo, Kirumi kwa ajili ya vita, Kiaramu kwa ajili ya nyimbo za maombolezo, na Kiebrania kwa ajili ya kuzungumza".

Hiyo ndio ilikuwa nafasi ya Kiaramu - katika "nyimbo za maombolezo". Lakini Kiebrania kilikuwa ni msingi wa mazungumzo ya kila siku ("kwa ajili ya mazungumzo") na ibada. Hivyo kwa mababa wa Kiyahudi kutozungumza na mwanawe "kwa Kiebrania", tangu alipokuwa mtoto mchanga, na kumfundisha sheria, ilikuwa ni "kana kwamba alikuwa amemzika". Kuhusu Kiaramu, kinyume chake, marabi walionya:

> "Yeyote anayefanya maombi binafsi [katika maombi] kwa Kiaramu, malaika wahudumu hawamsikilizi, kwani malaika hawaelewi Kiaramu".

Hili, hata hivyo halikuwa la kisheria, lakini inaonyesha tu undani wa hisia dhidi ya Kiaramu miongoni mwa wasomi wa Kiyahudi.

> Hakika, Talmud inasimulia tukio la hapo awali ambapo Gamalieli - Gamalieli yule yule ambaye Paulo alisoma chini yake (Matendo 22:3), na ambaye neno lake la busara kuhusu Wakristo limeandikwa katika Matendo 5:34-40 - alikuwa ameketi juu ya ngazi za hekalu ambalo bado lilikuwa halijakamilika. Mtu fulani alimwonyesha nakala ya tafsiri ya Kiaramu ya Ayubu, ya kwanza na wakati huo ndiyo "Targum" pekee. Alichukizwa sana na hilo, hata akamwambia mjenzi "aizike chini ya kifusi". Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa jaribio la kwanza katika sehemu ya Maandiko ya Kiaramu, katika Yudea ya wakati wa Yehoshua [Yesu]![26]

Ikiwa Kiaramu kilitumiwa na Wayahudi kuwasilisha wimbo wa maombolezo au maombolezo kwa ajili ya wafu, na ikizingatiwa kwamba Kiaramu kilikuwa "lugha ya majeshi maovu," basi twaona kwamba matumizi yake yanaweza kumaanisha ushawishi wa uwepo usiotakikana.

Yesu alipokuwa anakufa Msalabani, alibeba uzito wa dhambi za ulimwengu. Alikuwa amezungukwa na watu waovu wakimdhihaki na wakati huo wote Shetani anazidi kumsonga kwa mawazo kwamba Baba yake amemwacha. Maneno yenyewe ya Yesu katika Kiaramu yanaonyesha kwamba katika giza anakandamizwa na ushawishi wa kigeni ambao ni lugha ya maombolezo na kifo.

Katika muktadha huu, uandishi wa Danieli 7 katika Kiaramu kinyume na Kiebrania cha Danieli 8 ni muhimu sana.

Katika Danieli 7, Mungu anachukuliwa kupitia mtazamo ya ushawishi wa kigeni. Lugha ya hukumu na kifo inatumika kama kioo cha kutazama kazi ya Mungu katika hukumu.

Hukumu inapoelezwa katika Danieli 8 hakuna mandari yaa mahakama. Inasema tu:

> Naye akaniambia, "Kwa siku elfu mbili na mia tatu; **ndipo patakatifu patakapotakaswa."** — Danieli 8:14

[26] http://danielbenyaacovysrael.blogspot.com/2013/06/did-yehoshua-spoke-hebrew-or-aramaic.html

> Naye akaniambia, hata jioni-asubuhi elfu mbili na mia tatu, **ndipo patakatifu patakapotangazwa kuwa ni patakatifu.** — Danieli 8:14 (YLT)

> Mwingine akajibu, "Itachukua jioni na asubuhi 2,300; **ndipo Hekalu litakaporekebishwa tena."** — Danieli 8:14 (NLT)

Ndani ya Patakatifu pa Patakatifu pa Hekalu hakuna vitabu vya kumbukumbu nje ya Amri 10 na kitabu cha torati. Hakuna ishara za chumba cha mahakama katika nafasi hii. Danieli 2-7 imetolewa kwa Kiaramu kwa sababu sura hizi zinajumuisha unabii unaohusu hasa masuala ya kisiasa na hivyo kuzingatiwa kuwa na manufaa kwa Mataifa (Kiaramu kilikuwa lingua franca ya wakati huo). Katika Danieli 7 mtazamo huu wa Mungu kama Hakimu katika chumba cha mahakama kulingana na mtazamo wa mwanadamu kwake umetolewa kwa Kiaramu ili kusisitiza jambo kwamba huu ni mtazamo mgeni mbinguni, unaotolewa kwa wale walio na utaji mioyoni mwao (2 Wakorintho 3:15). ), kwa maana Baba hamhukumu na kumshutumu mtu ye yote.

Kiaramu ni mchanganyiko wa Wakaldayo na Kiebrania. Kinachanganya lugha ya Yerusalemu na lugha ya Babeli na hili ni muhimu sana. Mandhari ya hukumu ya Danieli 7 inachanganya mchakato wa hukumu ya Mungu na mchakato wa hukumu ya Babeli.

Katika lugha ya Kiebrania ya Danieli 8, kinachofafanuliwa ni urejeshwaji tu wa mambo ambayo yalikuwa nje ya utaratibu. Adamu alipomhukumu na kumshutumu Mungu kwa kufikiri kwamba Mungu alitaka kumuua mke wake, aliweka hekalu la moyo yake nje ya utaratibu. Halikuwa katika hali sahihi.

Kwa namna ileile kifo cha Yesu kilifungua kwa wanadamu imani kwamba Mungu anaweza kusamehe dhambi zetu kupitia mchakato wa dhabihu ambao haukuwakilisha tabia ya Mungu, hivyo pia kupitia mchakato unaoonekana kuwa ni hukumu ya adhabu, ubinadamu unakuja kuelewa kwamba dhambi itashughulikiwa kwa usahihi. Katika imani hii, basi mwanadamu anaalikwa kutofautisha mawazo yake ya hukumu na maneno ya Yesu ambayo yanatuambia kwamba Mungu hamhukumu mtu yeyote.

Ukimya wa Mungu katika Danieli 7 ukiunganishwa na lugha ya Kiaramu ulimfunika Baba katika giza ambalo Adamu aliwazia Mungu kuwa. Uthibitisho mwingine wa hili ni kwamba wakati Yesu yuko Msalabani, wakati utengano kamili na Baba yake unapotokea, anapobeba uzito kamili wa dhambi, Aliita "Mungu Wangu" badala ya "Baba Yangu". Hasemi "Baba Yangu, Baba Yangu, mbona umeniacha?" Katika injili zote nne, Yesu mara kwa mara anamrejelea Mungu kama Baba Yake. Hapa ndipo mahali pekee ambapo Yesu anamtaja kuwa Mungu Wangu, isipokuwa pale anapotaka Mariamu aelewe kwamba Baba yake ni Mungu Wake, ambaye pia ni Baba yake na Mungu wake Mariamu (Yohana 20:17). Mtu aliye na imani ya Yesu anamwona Mungu kuwa Baba yake, lakini mtu ambaye hataacha kuwahukumu wengine, katika siku hiyo ya mwisho, hatamwona Mungu kama Baba yake, bali atamuona kuwa Hakimu kwake.

Tunapotazama mandhari ya hukumu katika sura hii, tunajiona tumefunuliwa jinsi tutakavyoshughulika na watenda maovu. Tunamwazia Baba kuwa kama sisi kwa sababu ananyamaza mbele ya mawazo yetu ya uongo. Hata hivyo, katika nuru ya maisha ya Mwanawe duniani, Yeye hutukemea mbele ya macho yetu. Kila muujiza ambao Yesu aliufanya ni kemeo kwetu. Kila kofi usoni mwake alilolivumilia kwa subira ni kilio kwamba Baba yetu hafikirii kama tunavyofikiri na hahukumu kama tunavyohukumu.

Je, lugha na maneno ya Yesu yalikuwa muhimu alipokuwa karibu kufa? Je, aliashiria uwepo wa kitu kigeni?

Kama uhukumuvyo…

SURA YA 19

# Muktadha wa Hukumu kabla ya Marejeo

Kama tulivyochunguza hapo awali, kuna kipindi cha hukumu kinachofanyika kabla ya Ujio wa Pili wa Kristo. Mfuatano wa matukio katika Danieli 7 unadhihirisha hili waziwazi. Swali la kujibu ni hili; Nini asili ya hukumu hii wakati tunajua kwamba Mungu hahukumu wala hashutumu?

> Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba. — 2 Petro 3:9

Baba yetu hataki hata mmoja wa watoto Wake apotee. Anataka wote waokolewe. Tunapotazama katika Danieli 7 tunaona kwamba ni kupitia mchakato wa hukumu kwamba Kristo anaweza kumiliki ufalme wake.

> Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbingu akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye. Naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele, ambayo hayatapita kamwe, na ufalme wake ni ufalme usioweza kuangamizwa. — Danieli 7:13-14

Ufalme ambao Kristo anapokea ni ule ambao watu wote, mataifa na lugha watamtumikia kwa furaha. Utawala wa Kristo ni wa upendo wa kina na

mapenzi ya watu wake kwake. Utawala wake si wa nguvu bali wa uhuru na upendo wa wazi.

Shetani anadai umiliki wa kila mtu katika sayari hii. Kila mtu atendaye dhambi, anadai kuwa ni wake. Kabla tu ya Kristo kurudi kudai watoto Wake, Shetani mshitaki yuko chini ili kupinga watoto wa Mungu wanaomwamini kufufuliwa na kukombolewa.

> Nikasikia sauti kuu mbinguni, ikisema, Sasa kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake; **kwa maana ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu**, mchana na usiku. Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa. — Ufunuo wa Yohana 12:10-11

Biblia inatupatia kielelezo cha jinsi hukumu ya wafu inavyotokea. Kielelezo hiki kinapatikana katika maisha ya Musa.

> Lakini Mikaeli, malaika mkuu, alipokuwa akishindana na Ibilisi, na kuhojiana juu ya mwili wa Musa, hakuthubutu kuleta mashitaka ya kumtukana, **bali alisema, Bwana na akukemee.**" — Yuda 1:9 (KJV)

Muda fulani baada ya Musa kufa, alichukuliwa mbinguni. Huu ulikuwa ufufuo wa kwanza kuwahi kutokea kutoka kwa wafu. Biblia inafundisha kwamba mtu anapokufa, anarudi mavumbini na kungoja kaburini hadi ufufuo wa mwisho.

> kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa; **lakini wafu hawajui neno lo lote,** wala hawana ijara tena; maana kumbukumbu lao limesahauliwa. — Mhubiri 9:5

> Kwa hiyo mwanadamu hulala chini na hainuki. Mpaka mbingu zitakapokuwa hazipo tena, hawataamka wala kuamshwa kutoka katika usingizi wao. Laiti ungenificha kaburini, na kunificha mpaka ghadhabu yako ipite, na ungeniwekea wakati uliowekwa, na kunikumbuka! Je! mtu akifa ataishi tena? Siku zote za utumishi

> wangu mgumu nitangoja, mpaka mabadiliko yangu yaje. Utaita, nami nitakuitikia; Utatamani kazi ya mikono yako. — Ayubu 14:12-15

Kinyume na vile watu wengi ambavyo huamini, nafsi haifi.

> **Je! mwanadamu anayeweza kufa** atakuwa na haki zaidi kuliko Mungu? Je! mtu atakuwa safi kuliko Muumba wake? — Ayubu 4:17 (KJV)

Ikiwa mwanadamu tayari alikuwa na hali ya kutoweza kufa, kwa nini Biblia inatuambia tutafute kutokufa?

> wale ambao kwa saburi katika kutenda mema **wanatafuta utukufu na heshima na kutokuharibika [kutokufa],** watapata uzima wa milele — Warumi 2:7 (KJV)

Mungu peke yake ndiye asiyeweza kufa.

> …ambako yeye kwa majira yake atakudhihirisha, yeye aliyehimidiwa, Mwenye uweza peke yake, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana; **ambaye yeye peke yake hapatikani na mauti,** amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa; wala hakuna mwanadamu aliyemwona, wala awezaye kumwona. Heshima na uweza una yeye hata milele. Amina. — 1 Timotheo 6:15-16

Kuna mengi zaidi ambayo tungependa kuyashiriki katika mada hii, lakini jambo muhimu hapa ni kwamba hadi leo kumekuwa na idadi ndogo tu ya watu waliofufuliwa kutoka kwa wafu na kwenda mbinguni. Watoto wengine wa Mungu waliokombolewa watafufuliwa katika Ujio wa Pili.

> Lakini, ndugu, hatutaki msijue **habari zao waliolala mauti**, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini. Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye. Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. **Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na**

**mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani;** na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele. — 1 Wathesalonike 4:13-17

Kwa Musa ambaye alipelekwa mbinguni lilikuwa ni suala la kipekee. Henoko na Eliya pia walichukuliwa mbinguni, lakini hawakufa kwanza kama Musa.[27] Kristo aliposhuka kutoka mbinguni ili kumfufua Musa kutoka kwa wafu, Shetani alikuja kubishana na Kristo kama ilikuwa ni halali kwake kufufuliwa.

Kama tulivyozungumzia katika sura ya 12, rekodi ya maisha ya Musa ilikuwa imeandikwa ndani ya moyo wake na pia kuandikwa ndani ya moyo wa Kristo. Malaika waliopewa jukumu la kutulinda pia hurekodi matukio yetu ya maisha kwa sababu hutufuata katika maisha yetu na kushuhudia mambo yote tunayoyafanya.

Malaika wa BWANA hufanya kituo, Akiwazungukia wamchao na kuwaokoa. — Zaburi 34:7

Shetani anapotafuta kupinga madai ya Kristo juu ya maisha ya Musa, ni rekodi ya maisha ya Musa ambayo inazungumza kwa niaba yake katika wakati huo wa hukumu. Kristo alijua kila jambo la mwisho la maisha ya Musa kwa sababu kupitia Roho wa Mungu, Kristo alishuhudia kila tukio ndani yake.

Ee BWANA, umenichunguza na kunijua. **Wewe wajua** kuketi kwangu na kuondoka kwangu; **Umelifahamu** wazo langu tokea mbali. **Umepepeta** kwenda kwangu na kulala kwangu, Umeelewa na njia zangu zote. **Maana hamna neno ulimini mwangu Usilolijua kabisa, BWANA**. — Zaburi 139:1-4

Historia ya Musa ilionyesha waziwazi imani yake kwa Mwokozi wake. Ilionyesha kwamba alitumainia wema wa Kristo peke yake. Musa alikuwa amejihukumu mwenyewe kuhusiana na hili kabla ya kufa, na liliandikwa

[27] [27] See Genesis 5:23,24; 2 Kings 2:11.

ndani ya moyo wake na kuandikwa ndani ya moyo wa Kristo kama kumbukumbu ya kudumu.

> …mkutano mkuu na kanisa la wazaliwa wa kwanza **walioandikwa mbinguni**, na Mungu mwamuzi wa watu wote, na roho za watu wenye haki waliokamilika, — Waebrania 12:23

Kristo alinyamazisha shutuma za Shetani dhidi ya Musa na kusema "Bwana akukemee." Yote ambayo Kristo alipaswa kufanya ni kufunua kumbukumbu ya maisha ya Musa. Musa alikuwa ameiamua kesi yake mwenyewe na kuiweka mikononi mwa Mwokozi wake, kwa hiyo Shetani alipokuja kudai Musa, Kristo alisimama kumtetea na kwa hiyo alikuwa na uwezo wa kumfufua Musa kutoka katika usingizi wa kifo.

Huu ndio mfano wa wote watakaofufuliwa katika ufufuo wa kwanza wa wenye haki. Kabla Kristo hajaja kuwafufua watoto wake waliolala kutoka kwa wafu, Shetani atakuja kupinga haki ya Kristo ya kuwafufua. Rekodi ya watakatifu waliolala walioandikwa ndani ya moyo wa Kristo iko wazi, na rekodi zitathibitisha kama walikuwa wamejiona kuwa wanastahili uzima wa milele au la.

> Msihukumu, msije mkahukumiwa ninyi. **Kwa kuwa hukumu ile mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa;** na kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakachopimiwa. — Mathayo 7:1-2

> Kisha Paulo na Barnaba wakazungumza kwa ujasiri na kusema, "Ilikuwa lazima sisi kwanza tuwahubiri ninyi neno la Mungu ninyi Wayahudi. Lakini kwa kuwa mmelikataa na **kujiona hamstahili uzima wa milele**, sisi tutawatolea watu wa mataifa mengine." — Matendo 13:46 ( NLT )

Wale wanaojua kuwa wao ni wenye dhambi na kutumainia wema wa neema ya Mungu watakoma kuwahukumu wengine na kutulia tu katika neema na huruma ya Mungu. Wanapofikia mwisho wa maisha yao duniani na kuhakiki rekodi ya maisha yao, wanaona kushindwa na udhaifu wao mwingi. Wanajaribiwa kuwa na shaka ikiwa kuna kitu chochote kizuri katika maisha yao. Wanaachana na imani yoyote iwezekanayo kwamba wanastahili uzima wa milele kutokana na sifa zao njema na kutumainia tu rehema na

neema ya Mungu. Hili linaandikwa katika rekodi ya maisha yao, na rekodi hii itatolewa wakati Shetani atakapopinga haki ya Kristo ya kuwafufua kwa sababu wameandikwa katika mikono ya Kristo.

Kwa hiyo tangu 1844, Kristo amekuwa akitayarisha orodha ya wale watakaofufuliwa katika Ujio wa Pili. Shetani amekuwa akipinga kila moja ya madai ya mwisho ambayo Kristo anayafanya juu ya roho za wanadamu. Kuna wengine ambao Kristo anatamani kuwaokoa lakini Shetani anapopinga madai hayo, kumbukumbu iliyoachwa inadhihirisha kwamba hawakushikilia sana imani yao katika Kristo. Kwa hao, madai ya Shetani yanaimarishwa na anawezeshwa kuizuia nafsi hiyo isifufuliwe kwenye Ujio wa Pili. Inakuwa jambo la kuvunja moyo sana kwa Kristo kukubali dai la Shetani juu ya mtu kwa sababu rekodi ya maisha yao inaonyesha kwamba waliacha imani yao.

Kama tulivyogundua katika kisa cha mwana mpotevu na vile vile katika hukumu katika Danieli 7; Mungu hasemi neno dhidi ya mtu yeyote katika kesi. Kila mtu ameacha rekodi yake mwenyewe na rekodi hizi zinazungumza zenyewe. Kristo anakumbuka kila kesi kwa maana anamjua kila mtu kwa undani na kila kitu kuhusu historia yao, na kwa hiyo Anaweza kusimama kutetea watoto wa Mungu wakati Shetani anapinga kesi yao. Shetani ndiye mwendesha mashtaka na Kristo ndiye mtetezi. Mungu na Mwanawe hubatilisha uamuzi wa Shetani dhidi ya watu wa Mungu na hukumu inatolewa kwa niaba yao.

> Nikatazama, na pembe iyo hiyo ilifanya vita na watakatifu, ikawashinda; hata akaja huyo mzee wa siku, **nao watakatifu wake Aliye juu wakapewa hukumu;** na majira yakawadia watakatifu waumiliki ufalme. — Danieli 7:21-22

Ni wale tu ambao wamedai kuwa wafuasi wa Kristo wanaokuja katika hukumu hii. Wale wasiomkiri Kristo, au wasioonyesha ushahidi wa kazi ya Roho wa Kristo maishani mwao, wanatangaza kwamba hawataki mwili wa mbinguni uliojazwa na kuishi kupitia Roho wa Kristo; roho yao inakataa kutii utaratibu wa kijamii wa mbinguni ambao kanuni yake kuu ni upendo usiohukumu. Shetani anadai umiliki wa watu hao ambapo Kristo anaukubali

kulingana na kanuni za uhuru wa kuchagua, ingawa ni kinyume na shauku ya Kristo ya kumfufua kila mtu.

> Amwaminiye yeye hahukumiwi; **asiyeamini amekwisha kuhukumiwa;** kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu. — Yohana 3:18

Wale wasiomwamini Mwana wa Mungu hawana njia ya kuepuka roho yao ya kuhukumu. Wanapokabiliwa na dhambi zao, wanajihukumu wenyewe na kutamani kufa.

Na wafalme wa dunia, na wakuu, na majemadari, na matajiri, na wenye nguvu, na kila mtumwa, na mwungwana, wakajificha katika pango na chini ya miamba ya milima,

> wakiiambia milima na miamba, **Tuangukieni, tusitirini, mbele za uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na hasira ya Mwana-Kondoo**. Kwa maana siku iliyo kuu, ya hasira yao, imekuja; naye ni nani awezaye kusimama? — Ufunuo wa Yohana 6:15-17

Wakati Kristo atakaporudi na kulia kwa sauti ya Malaika Mkuu, "njoo nje," masikio ya watakatifu waliolala yataingiwa na sauti ya ushindi na wanaamka kutoka makaburini mwao na kutoka kuingia katika uzima wa milele.

Wafu waovu ambao hawakuamini masikio yao yamefungwa ili wasisikie. Katika maisha yao yote walikuwa wametenda dhambi na kuwa mbali na maombi ya Roho wa Mungu na hivyo sauti ya Kristo ni ngeni kwao. Hawaitikii wito, ingawa wito ulikuwa wa kila mtu kutoka.

> Amin, amin, nawaambia, Saa inakuja, na sasa ipo, wafu watakapoisikia sauti ya Mwana wa Mungu, **na wale waisikiao watakuwa hai**. — Yohana 5:25

Wafu waovu wanapinga mwito huu na kwa hiyo wanakaa katika mavumbi ya dunia hadi mwisho wa miaka 1000 wakati ambapo watafufuliwa.

Katika Ujio wa Mara ya Pili Kristo haigusi dunia katika umbo Lake la kimungu lililotukuzwa kikamilifu. Kama Angefanya hivi, basi wote wangetoka ardhini

kama inavyothibitishwa na ufufuo wa waovu baada ya miaka 1000 kuisha na Kristo anaigusa dunia. Kristo huwaita watakatifu wake waliolala kutokea angani ili wale tu waliokufa katika imani watoke.

> Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu**, ili tumlaki Bwana hewani;** na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele. — 1 Wathesalonike 4:17

> Naye atawatuma malaika zake pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule wake toka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu. Mathayo 24:31

Mwishoni mwa miaka 1000, Kristo atakaporudi duniani pamoja na jiji la mbinguni, wale waliokataa rehema ya Kristo watafufuliwa.

> Tazama, siku moja ya BWANA inakuja, ambayo mateka yatagawanyika kati yako. **Kwa maana nitawakusanya mataifa yote walete vita juu ya Yerusalemu;** na huo mji utapigwa, nazo nyumba zitatekwa, nao wanawake watatendwa jeuri; na nusu ya watu wa mji watatoka kwenda utumwani; **ila mabaki ya watu wa mji hawatakatiliwa mbali.** Hapo ndipo atakapotokea BWANA, naye atapigana na mataifa hayo, kama vile alipopigana zamani siku ya vita. **Na siku hiyo miguu yake itasimama juu ya mlima wa Mizeituni, unaoelekea Yerusalemu upande wa mashariki, nao mlima wa Mizeituni utapasuka katikati yake, upande wa mashariki na upande wa magharibi; litakuwako huko bonde kubwa sana;** na nusu ya mlima ule utaondoka kwenda upande wa kaskazini, na nusu yake itaondoka kwenda upande wa kusini. — Zekaria 14:1-4

> Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita, wala hapana bahari tena. **Nami nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe.** — Ufunuo wa Yohana 21:1-2

Bila Roho wa Kristo kuzungumza na dhamiri zao, waovu wanafunua hisia zao za kweli kwa Mungu na wenye haki na kutamani kuwaangamiza wale walio katika mji huo.

> Na hiyo miaka elfu itakapokwisha, Shetani atafunguliwa, atoke kifungoni mwake; naye atatoka kuwadanganya mataifa walio katika pembe nne za nchi, Gogu na Magogu, kuwakusanya kwa vita, ambao hesabu yao ni kama mchanga wa bahari. **Wakapanda juu ya upana wa nchi, wakaizingira kambi ya watakatifu, na mji huo uliopendwa**. Moto ukashuka kutoka mbinguni, ukawala. — Ufunuo wa Yohana 20:7-9

Kwa utafiti wa kina kuhusu jinsi moto unavyoshuka kutoka kwa Mungu na kuwaangamiza waovu, Tazama kijitabu "Consuming Fire" kinachopatikana kwenye fatheroflove.info.

Kwa ufupi, ni uzito wa hatia anayobeba mtenda dhambi ndiyo inayomwangamiza mwishowe. Mbele za Mungu na Mwana-Kondoo ambapo wanakabili rekodi yao yote ya maisha, wanajihukumu wenyewe kabisa na kuangamizwa na hatia yao wenyewe. Uchungu huu wa kiroho wa akili na Ubongo ni mchungu zaidi kuliko mateso ya kimwili.

Kwa ufupi, ni uzito wa hatia anayobeba mtenda dhambi ndiyo inayomwangamiza mwishowe. Mbele za Mungu na Mwana-Kondoo ambapo wanakabili rekodi yao yote ya maisha, wanajihukumu wenyewe kabisa na kuangamizwa na hatia yao wenyewe.

Ninyi mtachukua mimba ya makapi, mtazaa majani makavu; pumzi yenu ni moto utakaowateketeza wenyewe.

> Nanyi mtachukua mimba ya makapi, mtazaa majani makavu; **Pumzi yenu ni moto utakaowateketeza wenyewe.** Nao mataifa watakuwa kama kuchoma chokaa, kama miiba iliyokatika, iteketezwayo motoni. — Isaya 33:11-12

Kwa muhtasari, tunagundua maana ya hukumu iliyofafanuliwa katika Danieli 7. Mandhari ya mahakama inaundwa kwa sababu Shetani hataki kupoteza yeyote kati ya wale waliopita kaburini. Kama vile mlinzi wa Kirumi aliyetumwa kulilinda kaburi la Yesu ili kuzuia dhana yoyote ya wazo la

kwamba Kristo angeweza kufufuka, vivyo hivyo Shetani anazingira makaburi ya wafu wenye haki na kutafuta kuzuia wao kukiepuka kifo.

Kristo anamkemea Shetani huku rekodi/kumbukumbu zikidhihirisha wazi imani ya Mkristo ambaye Shetani anataka kudai kuwa milki yake.

Wale wanaoutazama uso wa Baba yetu wa mbinguni kwa imani, kupitia kioo cha tabia ya Yesu, wanaona kwamba Mungu hamhukumu au kumshutumu mtu yeyote. Shetani ndiye mshitaki na ndiye anayetafuta hukumu yetu. Shetani hutafuta kuweka tabia zake mwenyewe kwa Mungu ili kutufanya tufikiri kwamba Mungu anatuhukumu na kutushutumu. Mungu alimtuma Mwanawe kudhihirisha tabia yake, na si kuuhukumu ulimwengu, (Yohana 3:17). Katika hukumu Mungu anakaa kimya na kutuacha tuhukumu namna tunavyofikiri ataishughulikia hali hiyo. Kwa hivyo, tunaona ukweli kamili wa maneno ya Kristo:

> Kwa kuwa hukumu ile mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa;...
> — Mathayo 7:2

SURA YA 20

# Wakati wa Taabu ya Yakobo

Katika sura iliyopita tumeelezea mchakato wa hukumu wa wale wanaokufa kabla ya kuja kwa Kristo na kufufuliwa kutoka kwa wafu ili kukutana na Kristo hewani. Ni nini kinachotokea kwa wale wafuasi waaminifu wa Kristo ambao watasalia "hai" wakati wa kuja kwa Kristo? Je, hukumu inashughulikaje nao? Maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo.

> Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani. — 1 Wakorintho 10:11

Visa vya Biblia vitatusaidia sisi tunaoishi katika siku za mwisho kuelewa kile kinachotokea kwa watu wa Mungu wanapokabili mchakato wa hukumu, kama ilivyoelezwa katika Danieli 7, kabla ya kuja kwa Kristo.

Tulichunguza kisa cha mwanamke aliyefumaniwa katika uzinzi katika sura ya 10 na mchakato wa hukumu alioupitia akiwa hai. Aliletwa kwa Kristo na wale waliodai kuwa wafuasi wa Mungu. Kama viongozi wa Kiyahudi, kuna Wakristo wengi wanaowaambia watu ulimwenguni kwamba Mungu atawachoma motoni kwa ajili ya dhambi zao. Maneno na matendo yao yana uwezo wa kuwatupa wale wanaowashtaki miguuni pa Kristo. Ingawa wengi

hujibu kwa hasira na jeuri kwa washtaki wao, wengine hutii mashitaka yanayotolewa dhidi yao na kutafuta msamaha wa dhambi zao.

Kwa hiyo, katika siku za mwisho, makanisa ya Kikristo yana jukumu lao katika kuukabili ulimwengu na dhambi zake na kuwaambia watu juu ya hukumu inayowangoja. Ingawa makanisa yana mitazamo isiyofaa kabisa juu ya Mungu, bado yanashiriki sehemu yao katika kuamsha usadikisho juu ya dhambi.

Tunapokaribia siku za mwisho, Biblia inatuambia kutakuwa na wakati wa taabu kuu ambao haujawahi kutokea. Matukio ya hivi majuzi yanayohusiana na UVIKO-19 na ghasia za hapa na pale, pamoja na athari za kuongezeka kwa uharibifu wa mazingira, zinaweza hata kuonyesha kuwa tuko kwenye ukingo wa wakati huu wa shida.

> Wakati huo Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako; **na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo;** na wakati huo watu wako wataokolewa; kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile. — Danieli 12:1

Watu watakapoanza kuona dunia inayumba na majanga yakianza kuathiri sana dunia na mataifa ya ulimwengu, wengi wataanza kujiuliza ikiwa ni dhambi zao wenyewe ndizo zimeleta mambo haya duniani. Kutakuwa na tabaka mbili za watu wa dini zitakazojitokeza wakati matatizo haya yanapoanza.

> Na mmoja wa wale wahalifu waliotungikwa alimtukana, akisema, Je! Wewe si Kristo? Jiokoe nafsi yako na sisi. Lakini yule wa pili akamjibu akamkemea, akisema, Wewe humwogopi hata Mungu, nawe u katika hukumu iyo hiyo? Nayo ni haki kwetu sisi, kwa kuwa tunapokea malipo tuliyostahili kwa matendo yetu; bali huyu hakutenda lo lote lisilofaa. Kisha akasema, Ee Yesu, nikumbuke utakapoingia katika ufalme wako. — Luka 23:39-42

Watu hawa wote wawili walisulubishwa pamoja na Yesu. Mmoja wao alikubali kwamba janga hili lilikuwa linamwangukia kwa sababu ya dhambi

yake mwenyewe. Yule mwingine alimkemea Yesu kwa hasira na kudai kwamba ikiwa Kristo alikuwa vile ambavyo Yeye alidai kuwa basi angewaokoa wote. Mmoja alitubu kwa huzuni na matumaini; mwingine alibaki na hasira, dharau, na akakataa kutubu.

Paulo anasema siku za mwisho zitakuwa kama uzoefu wa mwanamke ambaye anakaribia kuzaa.

> Maana ninyi wenyewe mnajua yakini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku. Wakati wasemapo, Kuna amani na salama, ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafula, **kama vile utungu umjiavyo mwenye mimba**, wala hakika hawataokolewa. — 1 Wathesalonike 5:2-3

Kwa kutumia mlinganisho huohuo, Yeremia aliandika maneno haya:

> Maana BWANA asema hivi, Tumesikia sauti ya tetemeko, na ya hofu, wala si ya amani. Ulizeni sasa, mkaone kwamba mwanamume aona utungu wa uzazi; mbona, basi, ninaona kila **mtu anaweka mikono yake viunoni, kama mwanamke aliye na utungu**, na nyuso zote zimegeuka rangi. Ole! Maana siku ile ni kuu, hata hapana inayofanana nayo, **maana ni wakati wa taabu yake Yakobo**; lakini ataokolewa nayo. — Yeremia 30:5-7

Kufadhaika kwa jamii ya kibinadamu hatimaye kutazidi katika ghadhabu ya kutisha ya uharibifu. Wengi watapoteza maisha katika kipindi hiki cha machafuko ya kutisha.

> Hutaogopa hofu ya usiku, Wala mshale urukao mchana, Wala tauni ipitayo gizani, Wala uele uharibuo adhuhuri, **Ijapo watu elfu waanguka ubavuni pako. Naam, kumi elfu mkono wako wa kuume!** Hata hivyo hautakukaribia wewe. — Zaburi 91:5-7

Wakati ulimwengu unapoanza kubadilika, watu watakuwa wakitafuta kitu au mtu wa kulaumiwa kwa ajili ya uovu wote unaotokea. Viongozi wa kidini wa ulimwengu watatoa amri kuhusu ibada.

Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa Mwana-Kondoo, akanena kama joka.

> Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake. Naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza, ambaye jeraha lake la mauti lilipona. Naye afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu. Naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya mbele ya huyo mnyama, akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi. Akapewa kutia pumzi katika ile sanamu ya mnyama, hata ile sanamu ya mnyama inene, na kuwafanya hao wote wasioisujudu sanamu ya mnyama wauawe. ]Naye awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao; tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake. — Ufunuo wa Yohana 13:11-17

Ni nje ya upeo wa kitabu hiki kwenda kwa undani kuhusu unabii huu. Kwa uchambuzi wa kina tafadhali soma kitabu cha "Great Controversy" kinachopatikana *fatheroflove.info*

Jambo kuu tunalotaka kulizingatia hapa ni kwamba shinikizo litatumika kwa ulimwengu wote kushikamana na aina moja ya dini. Wale ambao hawatatii alama hii ya mamlaka watatishiwa kifo kwa kukataa kutii.

Ni wakati huu ambapo watu wa Mungu wanakabiliwa na wakati mbaya wa taabu. Sawa na mwanamke aliyekamatwa katika uzinzi, wengi wataburutwa mbele ya mahakama kwa kukataa kutii sheria za kidini zilizotungwa.

Huu ndio wakati ambao Biblia inaurejelea kama Taabu ya Yakobo. Kisa kinachorejelewa hapa ni pale Yakobo alipokuwa ameondoka na wake zake na watoto wake kutoka kwa baba mkwe wake ambaye alimlaghai. Yakobo alikuwa anarudi nyumbani katika nchi ya familia yake. Shida ilikuwa kwamba

kaka yake alikuwa anakuja kukutana naye ili kumaliza makovu ya zamani ambayo yalitokana na Yakobo kumdanganya baba yake na kuiba haki ya mzaliwa wa kwanza ya kaka yake. Haki ya mzaliwa wa kwanza ni urithi wa kiroho unaotolewa kubariki familia katika utajiri wa kiroho na kimwili. Esau, ndugu ya Yakobo alitaka utajiri wa kimwili lakini hakujali mambo ya kiroho. Yakobo sasa alikuwa anakabiliwa na kifo kutoka kwa kaka yake. Alipokuwa akielekea nyumbani, akimkimbia baba mkwe na sasa akimkabili kaka yake mwenye hasira, anapokea taarifa.

> Wale wajumbe wakarudi kwa Yakobo wakisema, Tulifika kwa **ndugu yako, Esau, naye anakuja kukulaki, na watu mia nne pamoja naye.** Ndipo Yakobo akaogopa sana, na kufadhaika sana, akawagawanya watu waliopo pamoja naye, na kondoo, na ng'ombe, na ngamia, wawe matuo mawili. — Mwanzo 32:6-7

Yakobo anafanya yote awezayo kibinadamu ili kujitayarisha kwa ajili ya mgogoro huo, kisha anaomba kwa Mungu amsaidie katika hali hii mbaya.

> Yakobo akasema, "Ee Mungu wa baba yangu Ibrahimu, na Mungu wa baba yangu Isaka, BWANA, uliyeniambia, Rudi uende mpaka nchi yako, na kwa jamaa zako, nami nitakutendea mema; mimi sistahili hata kidogo hizo rehema zote na kweli yote uliyomfanyia mtumwa wako; maana nalivuka mto huo wa Yordani na fimbo yangu tu, na sasa nimekuwa matuo mawili. Uniokoe sasa na mkono wa ndugu yangu, mkono wa Esau, maana mimi namwogopa, asije akanipiga, na mama pamoja na wana." — Mwanzo 32:9-11

Yakobo anaomba kwa huzuni na machozi kwa Mungu ili amsaidie. Anaposali, ghafla anashambuliwa na mtu anayeonekana kuwa mvamizi.

> Yakobo akakaa peke yake; na mtu mmoja akashindana naye mweleka hata alfajiri. — Mwanzo 32:24

Anapigana usiku kucha na mtu huyu asiyemjua. Hatimaye, kulipopambazuka, mvamizi huyu akamgusa Yakobo na nyonga yake ikateguka. Alijua mara moja kwamba hakuwa akishindana mweleka na mwanadamu bali na mtu wa Kimungu.

Naye alipoona ya kuwa hamshindi, alimgusa panapo uvungu wa paja lake; ukateguka uvungu wa paja la Yakobo alipokuwa akishindana naye.

> Akasema, Niache, niende, maana kunapambazuka. Akasema, Sikuachi, usiponibariki. Akamwuliza, Jina lako n'nani? Akasema, Yakobo. Akamwambia, Jina lako hutaitwa tena Yakobo, ila Israeli, maana umeshindana na Mungu, na watu, nawe umeshinda. Yakobo akamwuliza, akasema, Niambie, tafadhali, jina lako? Akasema, Kwa nini waniuliza jina langu? Akambariki huko. Yakobo akapaita mahali pale, Penueli, maana alisema, Nimeonana na Mungu uso kwa uso, na nafsi yangu imeokoka. — Mwanzo 32:25-30

Tukio hili la ajabu linaelezewa katika Yeremia 30:7 kuwa litatokea tena kwa watu wa Mungu kabla tu ya kuja kwa Kristo mara ya pili.

Yakobo anapofikiria maisha yake, anakumbuka mambo yote mabaya ambayo ameyafanya. Anaanza kuhisi kwamba yuko katika mazingira haya kwa sababu ya kushindwa kwake mara nyingi. Anajaribiwa kuhisi kwamba Mungu amemwacha.

Mwana wa Mungu anakuja kumsaidia, lakini Yakobo, kama mwana wa Adamu, anaogopa kwamba mgeni huyu anataka kumdhuru. Anashindana na Malaika maalum kwa ajili ya maisha yake bila kujua kuwa Malaika huyu hakuja kumdhuru bali kumuokoa. Mwana wa Mungu anaruhusu pambano hili kuendelea kuamua kama Yakobo atajitoa kabisa kwa Mungu na kutumaini msamaha wake, au kukata tamaa katika hali ya kushindwa.

Wakati huu, Shetani anamjaribu Yakobo kwamba dhambi zake ni kubwa sana kwa Mungu kumsamehe. Shetani anaendesha kesi yake dhidi ya Yakobo na kumjaza mashaka. Anahisi kwamba amechelewa sana. Lakini anashindana na mashaka yake hata anapopambana na mvamizi huyu. Pambano moja linawasilishwa na lingine. Kisa hiki hiki kinasimuliwa kwa njia nyingine katika maisha ya Yoshua Kuhani Mkuu.

> Kisha akanionyesha Yoshua, kuhani mkuu, amesimama mbele ya **Malaika wa BWANA**, na **Shetani** amesimama mkono wake wa kuume ili kushindana naye. BWANA akamwambia Shetani, **BWANA na akukemee Ewe Shetani;** naam, BWANA,

> aliyechagua Yerusalemu, na akukemee; je! Hiki si kinga kilichotolewa motoni? Basi, Yoshua alikuwa amevaa nguo chafu sana, naye alikuwa akisimama mbele ya malaika. Naye huyo akajibu, akawaambia wale waliosimama mbele yake, akisema, Mvueni nguo hizi zenye uchafu. Kisha akamwambia yeye, Tazama, nimekuondolea uovu wako, nami nitakuvika mavazi ya thamani nyingi. — Zekaria 3:1-4

Tunaona mfululizo wa matukio kama hayo yakionyeshwa hapa pia wakati Shetani alipobishana na Kristo kuhusu mwili wa Musa, wakati huu tu mtu anayehusika yuko hai. Hii si hukumu ya wafu bali ya walio hai. Malaika wa Bwana anamkemea Shetani kwa niaba ya Yoshua kama vile alivyomkemea kwa Musa.

> Lakini **Mikaeli, malaika mkuu**, aliposhindana na **Ibilisi**, na kuhojiana naye kwa ajili ya mwili wa Musa, hakuthubutu kumshitaki kwa kumlaumu, bali alisema, **Bwana na akukemee.** — Yuda 1:9

Yale yaliyompata Musa baada ya kifo chake, yalimtokea Yakobo, Yoshua Kuhani Mkuu na mwanamke aliyekamatwa katika uzinzi wakiwa hai. Shetani anatafuta kumfanya mwenye dhambi akate tamaa kwa sababu ya dhambi zake. Shutuma zinazojeruhi za shetani huhisiwa kana kwamba Mungu Mwenyewe ndiye anamhukumu mwenye dhambi. Sauti ya upole ya Mungu ikitoa tumaini kwa mwenye dhambi huhisiwa kana kwamba imezimishwa na sauti ya mshitaki. Kama Yesu Msalabani, sauti ya Mungu inaonekana kuwa kimya kwa muda mfupi.

> Mungu wangu, Mungu wangu, Mbona umeniacha? Mbona U mbali na wokovu wangu, Na maneno ya kuugua kwangu? Ee Mungu wangu, nalia mchana lakini hujibu Na wakati wa usiku lakini sipati raha. — Zaburi 22:1-2

Ni wakati ambapo mwenye dhambi anahisi kulemewa kabisa ndipo anakumbuka ukweli unaosema:

> Lakini sheria iliingia ili kosa lile liwe kubwa sana; na dhambi ilipozidi, neema ilikuwa nyingi zaidi; — Warumi 5:20

Watu wa Mungu wanamshinda Shetani na mashtaka yake. Wanachagua kuamini kwamba Mungu ni kama Yesu kabisa. Wanaamini kwamba hatawaacha na kuwakatilia mbali kwa ajili ya dhambi zao. Wanaelewa ahadi ya uzima wa milele licha ya ukweli kwamba maisha yao yote yameharibiwa na dhambi na ubinafsi. Jina lao limebadilishwa kutoka kuwa Yakobo, ambalo linamaanisha mnyang'anyi, hadi Israeli, ambalo lina maana ya *mshindi*.

Rekodi nzima ya maisha yetu inawasilishwa kwetu na tunahisi kutokuwa na msaada. Wakati huo tutamgeukia Kristo na kumshikilia na kusema "Naamini hutaniacha.

Shetani anajaribu kutusadikisha kwamba Mungu atatuacha mwishowe. Imani yetu itabaki imara licha ya kuhisi kulemewa kabisa na mashtaka ya Shetani dhidi yetu. Anatutazamisha maisha yetu ya zamani katika rangi nyeusi zaidi na tunajaribiwa kukata tamaa. Rekodi nzima ya maisha yetu inawasilishwa kwetu na tunahisi kutokuwa na msaada. Wakati huo tutamgeukia Kristo na kumshikilia na kusema "Naamini hutaniacha. Ninaomba baraka zako na ninaamini utanipa."

Huu ndio ushindi wa imani ambao Kristo alikuwa nao pale Kalvari, na anatupa ushindi huu, imani ya Yesu (Ufunuo 14:12).

Utaratibu huu wa hukumu ni jaribu kali kwa watu wa Mungu. Tunapotafakari haya, tunajaribiwa kuhisi woga sana au kutafakari kama hili litatokea kweli. Swali ambalo lazima liulizwe ni: "kwa nini watu wa Mungu wanapaswa kupitia mchakato huu mkubwa wa majaribio?" Je, hakuna njia rahisi zaidi kuliko hii?

SURA YA 21

# Hukumu ilikuja kwa kosa la mtu mmoja

Tulijadili katika sura ya 4 chimbuko la Hukumu ya adhabu katika jamii ya wanadamu. Sababu ya Adamu na Hawa kukimbia kutoka kwenye uwepo wa Mungu katika bustani ni kwa sababu ya hukumu ya adhabu ya Adamu kwa Mungu.

> Kisha wakasikia sauti ya BWANA Mungu, akitembea bustanini wakati wa jua kupunga; **Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, BWANA Mungu asiwaone**. — Mwanzo 3:8

> …awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa **hofu ya mauti** walikuwa katika hali ya utumwa. — Waebrania 2:15

Hofu ya kifo ilianzia kwa Adamu kwa sababu alifikiri kwamba Mungu alitaka kumwadhibu mke wake Hawa kwa kifo. Kwa uasi na hasira, alichukua tunda na kuamua kuikabili hatma yake pamoja naye. Ndani ya moyo wa Adamu kulikuwa na hukumu na shutuma dhidi ya Mungu na Mwanawe. Uongo kwamba Mungu alitaka kuwaua ulibadilika kuwa hofu wakati Yule ambaye Adamu alimwogopa na kumchukia sasa alipokuwa akimkaribia (Malaki 3:5).

Kwa hakika, Mwana wa Mungu alikuwa akimjia Adamu kwa upendo, huruma na rehema. Adamu aliwazia kwamba anakuja na hukumu na adhabu ili kumuua. Ili Mwana wa Mungu aweze kumkaribia Adamu, ilimbidi kuufunika uungu Wake kamili. Uwepo kamili wa upendo wa Mungu

unapokutana na mtenda dhambi aliyejawa na hatia, anayemchukia Mungu, hofu huwa nyingi na mdhambi hufa.

Fungu lifuatalo ni namna ambavyo mdhambi anavyopata uzoefu wa kuja mbele za Mungu akiwa na hofu na hukumu ya Mungu moyoni mwake.

> …katika mwali wa moto, akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii habari njema ya Bwana wetu Yesu Kristo; **ambao watapata haki na uharibifu wa milele kutoka kwenye uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake.** — 2 Wathesalonike 1:8-9 (YLT)

Hivi ndivyo inavyoonekana kutoka kwenye mtazamo wa Mungu:

> Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka! Angalieni, nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa. — Mathayo 23:37-38

Ni wazo la kufadhaisha kujua kwamba asili yetu ya kibinadamu tuliyopokea kutoka kwa Adamu ina mwelekeo wa kumchukia Mungu, daima hudhani kwamba Mungu anataka kutuua kwa ajili ya dhambi zetu au kutuacha kwa kutokuwa wema vya kutosha.

> Wakamnung'unikia Mungu na Musa, wakasema, **Mbona mmetupandisha kutoka Misri ili tufe jangwani?** Hakuna mkate! Hakuna maji! Na tunachukia chakula hiki kibaya! — Hesabu 21:5 (NIV)

> Nia inayotawaliwa na mwili **ni uadui kwa Mungu;** haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kufanya hivyo. — Warumi 8:7 (NIV)

> Kwa hiyo, kama kwa kosa la mmoja [Adamu] hukumu ilikuja juu ya watu wote na kuleta adhabu; — Warumi 5:18 (KJV)

Kosa la Adamu lilikuwa kuamini kitu kuhusu tabia ya Mungu ambacho kilikuwa cha uongo. Aliamini kimakosa kwamba Mungu alitaka kumuua mke

wake. Aliwazia kwa uongo kwamba Mungu alidai kifo kwa ajili ya kosa. Kupitia kosa hili kulikuja roho ya hukumu na shutuma kwa Mungu na Mwanawe. Tumerithi uadui huu dhidi ya Mungu ambao unadhihirika dhidi ya Kristo Mwanawe. Mungu alitufunulia hii chuki iliyozama ndani yetu alipomtoa Mwana wa Mungu kuishi kama mwanadamu kati yetu, na kukataliwa na kuuawa nasi.

Kama tulivyojadili katika sura ya 5, Adamu, katika kujilinda, aliielekeza hukumu yake mwenyewe kwa Mungu kama ambaye alidai kifo. Huu ndio mchakato:

1. Adamu anaamini kwamba kifo (adhabu ya kifo) ni matokeo ya uvunjaji wa sheria.
2. Adamu anavunja sheria.
3. Adamu anahisi hatia.
4. Adamu anahisi kwamba sasa lazima afe.
5. Adamu anatafuta kuhamisha lawama na hivyo kuhamishia hukumu ya kifo kwa Mwana wa Mungu.

Kila wakati Mwana wa Mungu anapokuja katika uwepo wetu, mlolongo huu unaamshwa. Hivi ndivyo hukumu ya mtu mmoja inavyowafikia watu wote. Kila mtu ana asili ndani yao inayomlilia Mwana wa Mungu. Kilichotokea miaka 2000 iliyopita kinatuonyesha kile tunachoweza kukifanya tunapopewa uhuru wa kushughulika na Mwana wa Mungu jinsi tunavyotaka.

Ili kuondoa amri hii ya kifo ambayo inakaa ndani yetu kwa asili, Kristo alipaswa kuchukua asili hii juu Yake na kisha kuiondoa kwa kifo na ufufuo wake.

> Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo. Kwa maana yeye ndiye amani yetu, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kiambaza cha kati *kilichotutenga*. **Naye akiisha kuuondoa ule uadui kwa mwili wake; ndiyo sheria ya amri zilizo katika maagizo; ili afanye hao wawili kuwa mtu mpya mmoja ndani ya nafsi yake;** akafanya amani. Akawapatanisha wote wawili na Mungu katika mwili mmoja, kwa njia ya msalaba,

akiisha kuufisha ule uadui kwa huo msalaba. — Waefeso 2:13-16 (KJV)

Adamu alikuwa amejenga kiambaza cha ukuta kati yake na Kristo kupitia hukumu aliyoitoa kuhusu Mwana wa Mungu. Kristo alijitwalia asili ya Adamu na kukibomoa kiambaza cha ukuta ule wa kati ili aweze kuja mbele zetu bila sisi kujiangamiza wenyewe kwa kuogopa adhabu ambayo tunafikiri itatuangukia.

Wafasiri wengi wanasema kwamba aya hii inazungumza juu ya kubomoa ukuta kati ya Myahudi na Mmataifa, na hili ni matumizi ya pili katika fungu hili. Walakini, uadui wote kati ya wanadamu ni dhihirisho tu la uadui ambao wanadamu wanauhisi dhidi ya Mungu.

Unapochukua neno maagizo katika Kiyunani na kulipekua Agano la Kale la Kiyunani ili kuona mahali linapotumika, tunagundua kwamba hili halina uhusiano wowote na sheria ya Musa bali ni maagizo ya wanadamu, haswa maagizo ya kifo yaliyowekwa na wanadamu. Hapa chini kuna aya za pekee katika Agano la Kale la Kiyunani zinazotumia neno hili [G1378] kwa ajili ya maagizo.

- Ezra 6:8 - Amri ya Kiajemi ya kujenga hekalu.
- Ezekieli 20:26 kuanzia mstari wa 25 – Mungu aliwaacha wafuate sheria ambazo hazikuwa nzuri. Mungu aliwatia unajisi kwa amri zao wenyewe.
- Danieli 2:13 - Amri ya kifo ya kuwaangamiza wenye hekima.
- Danieli 3:10, 29 - Amri ya kifo kwenye uwanda wa Dura na mfalme wa Babeli.
- Danieli 4:6 - Amri ya kuwaleta wenye hekima wote.
- Danieli 6:8, 10, 12, 13, 15, 26 - kutia muhuri amri ya kifo ya kutomwabudu Mungu ila mfalme.

Ikiwa tutaongeza matumizi ya hili neno katika Agano Jipya:

- Luka 2:1 - Amri ya Kaisari.
- Matendo 16:4 - Amri ya Mitume kuweka mipaka ya kile kinachofundishwa kutoka kwenye Sheria ya Musa kutokana na msimamo wa kupita kiasi wa baadhi ya Wayahudi juu ya swali hili.

- Matendo 17:7 - Amri ya Kaisari.
- Waefeso 2:15 - Kristo amekomesha sheria za amri (za kibinadamu) zilizomo katika maagizo.
- Wakolosai 2:14 - Kufuta kabisa amri za kibinadamu zilizokuwa dhidi yetu.

Matumizi ya neno hili kwa ajili ya maagizo yanadhihirisha kwamba halina uhusiano wowote na sheria ambazo Musa aliziandika katika Agano la Kale. Badala yake, linazungumzia sheria na matakwa ya wanadamu.

Amri ya kwanza ya kibinadamu ilikuwa kwamba Mwana wa Mungu afe kwa ajili ya matukio yaliyotokea katika bustani ya Edeni. Adamu alipitisha hukumu hii kwa watoto wake wote na hivyo hukumu hii inakuja juu ya watu wote katika hali yao ya asili. Asili ya mwanadamu inajaribu kuficha chuki hii na kudai kumpenda Mungu, sawa na raia wa taifa la kiimla ambao wanaogopa kuuawa ikiwa hawatamheshimu mkuu wa nchi (Mfano: Korea Kaskazini).

Wale wanaotembea katika njia ya wokovu, wakikubali kwamba maisha ambayo Yesu aliyadhihirisha katika dunia hii miaka 2000 iliyopita ni ufunuo kamili wa tabia ya Mungu na kwamba Mungu anasamehe dhambi zetu bure, wanaanza kubadilishwa kutoka kwenye roho ya kuhukumu hadi roho ya upendo na msamaha.

> Nami nitawapa moyo mmoja, nami nitatia roho mpya ndani yao; nami nitauondoa moyo wa kijiwe katika miili yao, nami nitawapa moyo wa nyama; ili waende katika amri zangu, na kuyashika maagizo yangu, na kuyatenda; nao watakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao. — Ezekieli 11:19-20 (KJV)

Tabia yetu ya kweli lazima ionyeshwe kwetu ili tuweze kufunguliwa kikamilifu kutoka kwenye roho yetu ya hukumu na amri ya kifo tuliyorithi kutoka kwa baba yetu wa kwanza. Hatuwezi kuepuka hisia ya kina ya hukumu inayotokana na asili zetu tunapomkaribia Mwana wa Mungu, lakini tunaweza kufahamu kwa nini hili hutokea na kuruhusu Kristo kufanya kazi ndani yetu badala ya kumkataa na kumsulubisha upya.

Ikiwa tutaweza kushikilia ahadi za Mungu, tukisaidiwa na Roho Wake, na kustahimili hukumu yetu wenyewe ambayo tumeimimina juu ya Kristo ikiaksiwa tena kwetu - basi tutatiwa muhuri wa jina la Baba.

> Kisha nikaona, na tazama, huyo Mwana-Kondoo amesimama juu ya mlima Sayuni, na watu mia na arobaini na nne elfu pamoja naye, wenye jina lake na jina la Baba yake limeandikwa katika vipaji vya nyuso zao. — Ufunuo wa Yohana 14:1

Yesu katika kuvaa mwili wake wa kibinadamu kamwe hakuanguka katika jaribu la kufikiri kwamba Baba yake alimhukumu wala hakumhukumu Baba yake kwa ajili ya magumu aliyokuwa akiyapitia. Yesu anafahamu kabisa jinsi asili yetu ilivyo kwa namna ambavyo hatuwezi kuifahamu isipokuwa tuwe na utambuzi wake. Ikiwa tunakubali kweli kwamba sisi, kama Kaini, ni wauaji wenye chuki kwa asili, tukaifia nafsi, na kuamini katika neema yake, tutapokea kikamilifu zawadi ya bure ya maisha yake na Yeye atashinda ndani yetu.

> Na kwa sababu hakuwa na haja ya mtu kushuhudia habari za mwanadamu; kwa maana yeye mwenyewe alijua yaliyomo ndani ya mwanadamu. — Yohana 2:25 (KJV)

> Bali twanena hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliiazimu tangu milele, kwa utukufu wetu; ambayo wenye kuitawala dunia hii hawaijui hata mmoja; maana kama wangaliijua, wasingalimsulibisha Bwana wa utukufu; — 1 Wakorintho 2:7-8 (KJV)

Hivi karibuni nguvu za giza zitaachiliwa kikamilifu juu ya ulimwengu huu, lakini kwa sasa malaika wanazuia pepo za machafuko zisiharibu dunia kikamilifu ili watu wa Mungu waweze kutiwa muhuri wa tabia ya Baba (jina).

> Baada ya hayo nikaona malaika wanne wamesimama katika pembe nne za nchi, wakizizuia pepo nne za nchi, upepo usivume juu ya nchi, wala juu ya bahari, wala juu ya mti wo wote. Nikaona malaika mwingine, akipanda kutoka maawio ya jua, mwenye muhuri ya Mungu aliye hai; akawapigia kelele kwa sauti kuu wale malaika wanne waliopewa kuidhuru nchi na bahari, akisema,

> Msiidhuru nchi, wala bahari, wala miti, hata tutakapokwisha kuwatia muhuri watumwa wa Mungu wetu juu ya vipaji vya nyuso zao. — Ufunuo wa Yohana 7:1-3 (KJV)

Kutiwa muhuri kwa watu wa Mungu ni kuondolewa kwa asili ya amri ya kifo cha hukumu tuliyorithi kutoka kwa Adamu. Watu wa Mungu watatiwa muhuri katika tabia ambayo itakoma kumhukumu na kumshutumu mtu yeyote bali kutegemea kabisa wema na huruma ya Mungu.

Mfumo mpya umeamriwa na maneno ya Kristo kwamba Yeye wala Baba yake hawamhukumu mtu yeyote.

Hii ndiyo sababu watu wa Mungu lazima wapitie wakati wa taabu ya Yakobo. Mitazamo ya amri ya kifo ya miili yetu ndiyo sababu kuu ya kumzaa Kristo ndani yetu (au kuwa kama Kristo katika tabia) ni kama uchungu mkali sana wa kuzaa.

> Kwa maana nimesikia sauti, kama sauti ya mwanamke wakati wa utungu wake, na sauti yake aumwaye, kama mwanamke azaaye mtoto wake wa kwanza, sauti ya binti Sayuni, atwetaye kupata pumzi, na kunyosha mikono yake, akisema, Ole wangu, sasa! Kwa maana roho yangu inazimia mbele ya wauaji. — Yeremia 4:31 ( YLT )

Mfumo ambao tumeweka baadhi ya aya hizi utakuwa mpya kwa wale wanaofahamu mafundisho ya Biblia ya kutiwa muhuri na matukio ya mwisho ya historia ya dunia. Mfumo mpya umeamriwa na maneno ya Kristo kwamba Yeye wala Baba yake hawamhukumu mtu yeyote.

Utahukumu vipi?

SURA YA 22

# Kiti cha Hukumu cha Kristo

Mwishoni mwa sura ya 3 tuliuliza swali kama tunaielewa kweli haki ya Mungu ni nini. Tumeshughulikia mambo mengi ili kuonyesha kwamba Mungu hamhukumu au kumshutumu mtu yeyote. Tunajikumbusha kauli tuliyoitoa katika sura ya 3.

> Inaaminika karibu kila mahali kwamba enzi kuu ya Mungu, na kwa hiyo viongozi wote wa jumuiya wanaotawala miongoni mwa watu, hutegemeza haki juu ya uwezo wa kushika upanga. Uadilifu ni kuhukumu matendo kuwa mema au mabaya na hivyo kuwalipa wema na kuwaadhibu wabaya.

Mtazamo huu wa Mungu unaona rehema ikifanya kazi kama kanuni inayopingana na haki. Mitazamo yetu ya kibinadamu ya kanuni hizi mbili ni kwamba haziwezi kufanya kazi kwa wakati mmoja. Ikiwa rehema inatolewa, basi haki lazima idai matakwa yake. Haki ikitendeka basi rehema itakuwa imepuuzwa.

Ikiwa kanuni ya nguvu (iwe ya kimwili au ya kiakili) na tishio la kifo huondolewa kutoka kwenye mtazamo wetu wa haki ya Mungu, uhusiano kati ya rehema na haki hubadilika kabisa.

> Haki na Adili ndio msingi wa kiti chako cha enzi; rehema na kweli zatangulia mbele za uso wako. — Zaburi 89:14 (NKJV)

> Haki na hukumu ndio makao ya kiti chako cha enzi: fadhili na kweli zitakutangulia. — Zaburi 89:14 (KJV)

Mstari huu katika Zaburi ni muhimu sana kwa sababu unazungumzia uhusiano kati ya haki na rehema. Nimenukuu matoleo mawili kwa sababu moja hutumia nuktamkato kuunganisha vishazi viwili huku la pili likitumia nuktapacha. Hivyo, kuna tofauti gani?

> Nuktamkato zinapaswa kuwasilisha ushahidi au sababu ya taarifa iliyotangulia; kwa mfano, sentensi hii inatumia ipasavyo nuktamkato. Nuktapacha, kwa upande mwingine, inapaswa kutumika kwa uhusiano wenye nguvu na wa moja kwa moja. Inapaswa kutoa msisitizo, mfano, au maelezo.[28]

KJV inatoa uhusiano mkubwa kati ya haki na rehema. Kimsingi inasema kwamba haki na hukumu ya Mungu inadhihirishwa kama rehema na ukweli. Matumizi ya nuktamkato katika NKJV yanapendekeza kwamba haki na rehema vinahusiana. Hii pia inaweza kuunga mkono wazo lile lile, lakini muunganiko ni mwepesi kidogo. Bila kujali hili, kanuni ya msingi ya usambamba wa Kiebrania inaonyesha kwamba wazo lile lile linarudiwa, kwa njia tofauti tu.

Ukweli unaovutia wa mstari huu ni kwamba haki ya Mungu inadhihirishwa kama rehema. Haki ni kufanya yaliyo sahihi. Kulingana na tabia ya Mungu jambo sahihi la kufanya ni kuonyesha rehema.

> **Baba wa yatima na mwamuzi wa wajane**, Mungu katika kao lake takatifu. — Zaburi 68:5 (KJV)

> BWANA, umeisikia tamaa ya wanyonge, Utaitengeneza mioyo yao, utalitega sikio lako. **Ili kumhukumu yatima naye aliyeonewa**, Binadamu aliye udongo asizidi kudhulumu. — Zaburi 10:17-18

[28] http://crosstalk.cell.com/blog/colons-vs-semicolons

> Kwa maana Wewe, Bwana, U mwema, Umekuwa tayari kusamehe, Na mwingi wa fadhili, Kwa watu wote wakuitao. — Zaburi 86:5 (KJV)

Ni jambo linalofaa kufanya kuwatunza yatima na maskini. Ni haki kuonyesha huruma na kusamehe. Hii ni haki katika ufalme wa Mungu. Kuna vifungu kadhaa vya Maandiko vinavyozungumzia juu ya Mungu kuwahukumu watu. Kile ambacho kwa kawaida tungedhani ni hukumu ya adhabu ni hukumu inayoleta uponyaji na urejeshwaji.

> Tokea Sayuni, ukamilifu wa uzuri, Mungu amemulika. Mungu wetu atakuja wala hatanyamaza, Moto utakula mbele zake, na tufani yavuma sana ikimzunguka pande zote. Ataziita mbingu zilizo juu, Na nchi pia awahukumu watu wake. Nikusanyieni wacha Mungu wangu Waliofanya agano nami kwa dhabihu. Na mbingu zitatangaza haki yake, Kwa maana Mungu ndiye aliye hakimu. — Zaburi 50:2-6

> BWANA wa majeshi amesema hivi, ya kwamba, Fanyeni hukumu za kweli, kila mtu na amwonee ndugu yake rehema na huruma; tena msimdhulumu mjane, wala yatima, wala mgeni, wala maskini; wala mtu awaye yote miongoni mwenu asiwaze mabaya juu ya ndugu yake moyoni mwake. — Zekaria 7:9-10 (KJV)

Kitendo cha hukumu ya Mungu ni kuponya na kuokoa watu wake. Anatuambia:

> Ukaniite siku ya mateso; Nitakuokoa, na wewe utanitukuza. — Zaburi 50:15

Swali la haraka linalokuja ni vipi kuhusiana na adhabu ya watenda maovu? Je! Mungu hana kizuizi kwa wale wanaotaka kufanya maovu? Zaburi ya 50 inaendelea kama ifuatavyo:

> Bali mtu asiye haki, Mungu amwambia, Una nini wewe kuitangaza sheria yangu, Na kuliweka agano langu kinywani mwako? Maana wewe umechukia maonyo, Na kuyatupa maneno yangu nyuma yako. Ulipomwona mwivi ulikuwa radhi naye, Ukashirikiana na

> wazinzi. Umekiachia kinywa chako kinene mabaya, Na ulimi wako watunga hila. Umekaa na kumsengenya ndugu yako, Na mwana wa mama yako umemsingizia. Ndivyo ulivyofanya, nami nikanyamaza; Ukadhani ya kuwa Mimi ni kama wewe. Walakini nitakukemea; Nitayapanga hayo mbele ya macho yako. — Zaburi 50:16-21

Bwana anawaambia waovu mahali ambapo kosa lao lilipo na hatari kubwa inayowakabili. Anaweka haya mbele ya macho yao. Sura hiyo inahitimisha kama ifuatavyo:

> Yafahamuni hayo, Ninyi mnaomsahau Mungu, Nisije nikawararueni, Asipatikane mwenye kuwaponya. Atoaye dhabihu za kushukuru, Ndiye anayenitukuza. Naye autengenezaye mwenendo wake, Nitamwonyesha wokovu wa Mungu. — Zaburi 50:22-23

Tafsiri nyingi za Biblia hutafsiri Zaburi 50:22 kusema kwamba Mungu atawararua waovu vipande-vipande. Tafsiri hii inaonyesha jinsi ambavyo tungetarajia Mungu atende, lakini andiko hilo halisemi hivyo tunapochunguza kwa makini.

> Fahamuni haya, nawasihi, ninyi mnaomsahau Mungu, nisije nikararua, wala hakuna mwokozi. — Zaburi 50:22 (YLT)

Neno la Kiebrania "rarua" liko katika umbo linalomaanisha tu kutengeneza au kurarua. Halina maana ya kurarua vipande vipande. Neno lile lile la Kiebrania[29] kwa ajili ya kurarua limetumika katika kitabu cha Hosea na hutuambia hasa kile ambacho Mungu anamaanisha katika kisa hiki:

> Kwa maana mimi ni kama simba kwa Efraimu, na kama mwana-simba kwa nyumba ya Yuda; nararua na kwenda, nachukua, wala hapana mwokozi. naenda-naparudi mahali pangu, hata watakapokuwa ukiwa, na kunitafuta uso wangu. Katika shida zao wananitafuta upesi! — Hosea 5:14-15 (YLT)

[29] The Hebrew word is in the Qal form. If the word was intended to mean tear in pieces it would need to be in either the Niphal or Poal form.

*Kurarua* kunafafanuliwa kama Mungu kurudi mahali pake na kuruhusu waovu kukabiliana na matokeo ya uchaguzi wao. Wacha tufuate mlolongo huu.

1. Mungu hujirarua *mwenyewe* na kwenda zake
2. Sasa hakuna mwokozi kwa waovu
3. Mungu anarudi mahali pake na kungoja
4. Mpaka waovu wawe ukiwa kutokana na kukabili matokeo ya matendo yao
5. Waovu wana nafasi kuutafuta uso wa Mungu katika dhiki zao

Ni uchungu kwa Mungu kuruhusu yeyote wa watoto wake kukabiliana na uovu wao wenyewe. Inamuuma sana kulazimika kuondoka. Anajua watoto Wake watateseka lakini kwa sababu hawatasikia, Mungu lazima awaache kulingana na uchaguzi wao wenyewe.

Katika mahali hapa pa dhiki tunaona kwamba waovu wana wakati wa kumtafuta Mungu haraka na kuponywa. Hivi ndivyo Mungu anavyomaanisha katika mstari wa mwisho wa Zaburi 50.

> Atoaye dhabihu za kushukuru, Ndiye anayenitukuza. Naye autengenezaye mwenendo wake, Nitamwonyesha wokovu wa Mungu. — Zaburi 50:23

Maneno haya yanasemwa kwa waovu. Hukumu ya Mungu kwa waovu inawaruhusu kuona matokeo ya uovu wao; ili wakabiliane na dhiki ya matendo yao katika tumaini la kwamba waovu watarudi kwa Mungu na kuponywa. Mungu ana uwezo wa kusuluhisha kwa kiasi fulani matokeo haya ili yawaangukie waovu kwa namna ifaayo zaidi ya kuwasaidia kutambua udanganyifu wa dhambi (angalia kwa mfano jinsi mapigo yalivyotokea katika nchi ya Misri kwa namna ambayo ilikuwa ni kuwaonyesha kutoweza kuokoa kwa miungu ya Misri). "Kwa maana katika yeye vitu vyote hushikana," Wakolosai 1:17. Ikiwa wakati wowote watu waovu wataona neema kwa Mungu na kutubu, Mungu ataelekeza uso Wake kwao tena na kuwarehemu. Matendo ya Mungu katika hukumu siku zote ni ya kuponya, sio kulaani na kuangamiza.

Hivi ndivyo Biblia inavyofafanua haki ya kulipiza kisasi:

> BWANA amejidhihirisha na kutekeleza hukumu; Amemnasa mdhalimu kwa kazi ya mikono yake. — Zaburi 9:16

Tena, Mungu huwatendeaje waasi wanaofanya maovu? Anawaruhusu kunaswa katika kazi ya mikono yao wenyewe. Mungu anarudi mahali pake mpaka wawe ukiwa. Kanuni hii imeandikwa katika Amri 10 zenyewe.

> ….Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; **nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao,** nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu. — Kutoka 20:5-6

Haki ya Mungu ni kuonyesha rehema na kuleta urejeshwaji, lakini rehema yake ikikataliwa, basi kwa kuheshimu uhuru wa kuchagua huwaruhusu wanadamu kupata matokeo ya asili ya uchaguzi wao wenyewe. Wanadamu wanapofadhaika kwa sababu ya maafa yanayowaangukia katika upumbavu wao, Mungu hutafuta kuwavuta warudi kwake ili kuwaponya. Ikiwa watu bado wanakataa kusikiliza, basi wataangamia katika uovu wao wenyewe. Mfumo huu wa haki ni tofauti kabisa na ule wa Kaisari (yaani mamlaka ya kibinadamu) ambaye ataleta maumivu, kufungwa na kifo kwa mkosaji. Hii ni mojawapo ya njia ambazo Mungu hurejesha njia za wanadamu juu yao; Anaruhusu haki ya Kaisari kuwepo na anaruhusu uovu wa mfumo huu wa haki kuwaadhibu wale wanaofanya uovu. Biblia inaliita hili kisasi cha Mungu.

> Kwa maana watawalao hawatishi watu kwa sababu ya matendo mema, bali kwa sababu ya matendo mabaya. Basi, wataka usimwogope mwenye mamlaka? Fanya mema, nawe utapata sifa kwake; kwa kuwa yeye ni mtumishi wa Mungu kwako kwa ajili ya mema. **Lakini ufanyapo mabaya, ogopa; kwa maana hauchukui upanga bure; kwa kuwa ni mtumishi wa Mungu, amlipizaye kisasi mtenda mabaya kwa ajili ya ghadhabu.** — Warumi 13:3-4

Kanuni za Warumi 13:3-4 ni onyesho la kanuni ya Amri 10 ya kupatiliza matendo mabaya juu yake. Kwa njia hii Kaisari anakuwa mtumishi wa Mungu kuulipiza kisasi uovu. Hii haimaanishi kwamba Kaisari anaishi

kulingana na tabia ya Mungu au anamwakilisha Mungu kwa njia yoyote ile, badala yake Mungu anaruhusu matokeo ya mfumo wa haki wa uongo wa kifo kumrudia.

Kaisari na Kristo wote wana kiti cha hukumu.

> Paulo akasema, **Mimi ninasimama hapa mbele ya kiti cha hukumu cha Kaisari**, ndipo panipasapo kuhukumiwa; sikuwakosa Wayahudi neno, kama wewe ujuavyo sana. — Matendo ya Mitume 25:10

> **Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo,** ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya. — 2 Wakorintho 5:10

Viti hivi viwili vya hukumu havifanani. Kiti cha hukumu cha Kristo kinafanya kazi kwa kanuni tofauti kabisa na ya Kaisari. Mfumo wa haki wa mbinguni hautumii nguvu au tishio la kifo ili kuunga mkono kanuni zake. Matumizi ya nguvu ni kinyume na ufalme wa Kristo.

> Yesu akajibu, Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu. Kama ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huu, watumishi wangu wangenipigania, nisije nikatiwa mikononi mwa Wayahudi. Lakini ufalme wangu sio wa hapa. — Yohana 18:36

Kanuni ya kupigana ni kanuni ya nguvu katika muktadha huu. Ufalme wa Kristo hautumii nguvu. Inamaanisha nini kusimama kwenye kiti cha hukumu cha Kristo ili kupokea mambo yanayofanywa katika mwili? Hili linaweza kuonekana kama tishio, sivyo?

> Lakini wewe je! Mbona wamhukumu ndugu yako? Au wewe je! Mbona wamdharau ndugu yako? Kwa maana sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu. — Warumi 14:10

Paulo anauliza swali, kwa nini wamhukumu ndugu yako? Kisha anaonya kwamba tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo. Je, kauli hii ni

tishio la kushawishi tabia njema? Hili haliwezekani. Haileti mantiki kabisa kwamba sisi hatupaswi kuwahukumu wengine, wakati huo huo Kristo atatuhukumu. Ikiwa hatupaswi kuwahukumu wengine, basi tunahitaji kielelezo kamili katika Kristo cha kutohukumu. Hivi ndivyo Yesu anavyotuambia. Yeye Hamhukumu mtu yeyote (Yohana 8:15).

Kusimama mbele ya Yesu, Yeye ambaye ni kiini cha upendo, msamaha na huruma, ni mateso kwa nafsi yenye ubinafsi.

Ni nini basi maana ya kusimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo?

> Wapenzi wangu, msilipize kisasi, bali ipisheni ghadhabu ya Mungu, kwa maana imeandikwa: "Kulipiza kisasi ni juu yangu; mimi nitalipa," asema Bwana. Kinyume chake: "Adui yako akiwa na njaa, mpe chakula; akiwa na kiu, mpe kitu cha kunywa. Kwa kufanya hivyo, utampalia makaa ya moto juu ya kichwa chake." — Warumi 12:19-20 ( NIV)

Kusimama mbele ya Yesu, Yeye ambaye ni kiini cha upendo, msamaha na huruma, ni mateso kwa nafsi yenye ubinafsi. Viongozi wa Kiyahudi waliposimama mbele ya Kristo alipokuwa akiandika juu ya mchanga, kuwepo kwake na kile alichokiandika kiliwasukuma kujihukumu wenyewe na kuondoka zao.

Upendo na huruma ya Mungu vina nguvu yake ya asili ya kusadikisha. Huruma ya Mungu isiyo na kikomo ina uwezo usio na kikomo wa kuitia hatiani nafsi juu ya jinsi Mungu alivyo msafi na jinsi tulivyo waovu. Kila siku Mwokozi wetu huvumilia majanga mabaya ya watu kujiua, mauaji, utumiaji wa dawa za kulevya na utoaji mimba. Kuvumilia kwake mambo haya kunaonyesha upendo mkubwa sana kiasi kwamba hatuwezi kuuelewa kikamili.

Upendo huu una nguvu kiasi kwamba mwenye dhambi anaposimama mbele ya kiti hiki cha hukumu cha Kristo bila kusamehewa dhambi zake, hatia ya ubinafsi wake itamponda. Si Mungu anayemhukumu mwenye dhambi, kwa maana hukumu haitoki kwa Mungu bali kutoka kwa Shetani na Adamu.

Pokea rehema za Mungu leo; hii ni haki ya Mungu, kukusamehe bure na kukuondolea mzigo wa hatia yako.

SURA YA 23

# Utakaso wa Hekalu na Siku ya Upatanisho

Mwanzoni mwa kalenda ya Kiyahudi ni sikukuu ya Pasaka na Mikate Isiyotiwa Chachu. Huu ni mwanzo wa mchakato wa upatanisho. Hujikita katik dhabihu na msamaha wa dhambi. Hili hupata kitovu chake katika ua na madhabahu ya dhabihu.

Siku takatifu zaidi ya mwaka kwa Wayahudi ni Yom Kippur, au kwa Kiingereza, Siku ya Upatanisho. Matukio ya siku hii huwezesha ukamilifu wa mchakato wa upatanisho. Yom Kippur hutokea katika mwezi wa saba na kazi yake kuu ni katika Patakatifu pa Patakatifu pa Hekalu. Watu wanatakiwa kufunga na kunyenyekeza nafsi zao mbele za Mungu, na kuomba kwamba mambo yote yawekwe sawa na Mungu kwa maana ni siku ya hukumu.

Tamaduni kuu inayohusishwa na siku hii inahusisha mbuzi wawili:

> Ataivaa ile kanzu takatifu ya kitani, atakuwa na zile suruali za kitani mwilini mwake, atafungwa ule mshipi wa kitani, naye atavaa ile kofia ya kitani; hayo ndiyo mavazi matakatifu, naye ataoga mwili wake majini, na kuyavaa. **Kisha atatwaa mikononi mwa mkutano wa Waisraeli mbuzi waume wawili, kwa sadaka ya dhambi;** na kondoo mume kwa sadaka ya kuteketezwa. Na Haruni atamtoa yule ng'ombe wa sadaka ya dhambi, aliye kwa ajili ya nafsi yake, na kufanya upatanisho kwa ajili ya nafsi yake mwenyewe, na kwa ajili ya nyumba yake. **Kisha atawatwaa wale**

> **mbuzi wawili na kuwaweka mbele za BWANA mlangoni pa hema ya kukutania. Na Haruni atapiga kura juu ya wale mbuzi wawili; kura moja kwa ajili ya BWANA; na kura ya pili kwa ajili ya Azazeli.** Na Haruni atamleta yule mbuzi aliyeangukiwa na kura kwa ajili ya BWANA, na kumtoa awe sadaka ya dhambi. Bali yule mbuzi aliyeangukiwa na kura kwa ajili ya Azazeli atawekwa hai mbele za BWANA ili kumfanyia upatanisho, ili kumpeleka jangwani kwa ajili ya Azazeli. — Mambo ya Walawi 16:4-10

Tulionyesha katika sura ya 14 kwamba Hekalu haliwakilishi kikamilifu tabia ya Mungu lakini badala yake linawakilisha mchakato ambao mwanadamu anapatanishwa na Mungu. Dhabihu na matoleo hukupendezwa nazo (Zaburi 40:6). Hiyo ina maana tukio hili linaonyesha mitazamo yetu ya kibinadamu ya hukumu.

Mbuzi mmoja anaitwa mbuzi wa Bwana na mwingine ni mbuzi wa Azazeli. Kwa nini mbuzi hutumiwa badala ya kondoo?

Kinachovutia ni kwamba neno la Kiebrania la mbuzi hapa linaweza kutumika kwa njia tatu tofauti:

1) Mwenye manyoya (kivumishi)
2) Mbuzi-dume (nomino)
   2a) kama mnyama wa dhabihu
   2b) **satyr, inaweza kumaanisha mbuzi mwenye pepo** kama nguruwe wa Gadara (Mathayo 8:30-32)

Mchakato ambao mbuzi wawili huchaguliwa ni kwa bahati nasibu. Aidha mbuzi anaweza kuwa mbuzi wa Bwana au mbuzi wa Azazeli. Hapa ndipo mahali pa kwanza katika Biblia ambapo kupiga kura kunatajwa. Adam Clarke, mfafanuzi mashuhuri wa Biblia wa karne ya 19, anatoa utaratibu wa jinsi bahati nasibu hiyo ilivyofanyika.

> Wayahudi wanatujulisha kwamba kulikuwa na kura mbili zilizotengenezwa kwa mbao, mawe, au aina yoyote ya chuma. Katika moja iliandikwa **לשם** Lashemu, kwa ajili ya Jina hilo, yaani., **יהוה** Yehova, ambalo Wayahudi hawataliandika wala kulitamka; na

> katika lile la pili liliandikwa **לעזאזל** Laazazeli, kwa ajili ya Mbuzi wa Azazeli; kisha wakazipiga kura mbili katika chombo kinachoitwa **קלפי** kalpey, mbuzi wakiwa wamesimama na nyuso zao kuelekea magharibi. Kisha kuhani akaja, na hao mbuzi wakasimama mbele yake, mmoja upande wa kulia na mwingine upande wa kushoto; ndipo kalpei akatikiswa, na kuhani akatia mikononi mwake yote miwili, akatoa kura katika kila mmoja; kile kilichokuwa katika mkono wake wa kulia akakiweka juu ya mbuzi aliye upande wake wa kuume, na kile katika mkono wake wa kushoto akakilaza juu ya mbuzi. mbuzi aliyekuwa upande wake wa kushoto; na kulingana na yale yaliyoandikwa kwenye kura, yule mbuzi wa Azazeli na mbuzi wa dhabihu walithibitishwa. (Tazama the Mishna, in Tract. Yoma. Comment of Leviticus 16:8).

Njia ambayo Mungu kwa kawaida aliwasilisha mapenzi yake ilikuwa kwa kutumia Urimu na Thumimu. Haya yalikuwa mawe mawili yaliyowekwa kwenye mabega ya Kuhani Mkuu. Mungu angewasilisha mapenzi yake kwa njia ya jiwe moja kuwaka au jiwe lingine kufunikwa na wingu. Hata hivyo katika Siku ya Upatanisho kupiga kura hutumiwa badala ya Urimu na Thumimu, njia ya unyenyekevu zaidi na inayoonekana kuwa haina maana. Inaweza kusemwa kwamba Bwana huchagua ni mbuzi yupi, lakini ana mwonekano wa kubahatisha kabisa.

Kanuni hii ya kuweka hatia ya taifa juu ya mtu au mnyama ilikuwa ya kawaida katika tamaduni za kipagani. Inalingana kikamilifu na jinsi mwanadamu wa asili anavyotatua hatia. Adam Clarke anatoa historia hii ya kuvutia anapotoa maoni yake kuhusu Mambo ya Walawi 16:10.

> Mataifa mengi ya kale yalikuwa na dhabihu za urithi, ambazo walihamisha kwa kutumia taratibu na sherehe fulani hatia ya jumuiya kwa ujumla, kwa namna ile ile ambayo mbuzi wa Azazeli alitumiwa na Wayahudi. Fahali mweupe aliyetolewa dhabihu na Wamisri kwa mungu wao Apis alikuwa wa namna hii; walikata kichwa cha yule fahari ambaye walikuwa wametoa dhabihu, na baada ya kuwa kimeandaliwa vizuri, "ili kwamba ikiwa kuna uovu wowote unaozunguka juu yao, au juu ya nchi ya Misri, uweze kumwagika juu ya kichwa hicho," walikiuza kwa Wagiriki au

kukitupa ndani ya mto Nile - Tazama Herod. Euterp., p. 104, edit. Gale.

> Petronius Arbiter anasema kwamba ilikuwa desturi miongoni mwa wakazi wa kale wa Marseilles, kila walipopatwa na tauni yoyote, kumchukua mmoja wa raia maskini zaidi ambaye alijitoa kwa ajili hiyo, na kumlisha mwaka mzima kwa chakula safi na bora zaidi, walimpamba kwa vervain, wakamvika mavazi matakatifu; na baada ya kuomba kwamba maovu yote ambayo mji huo uliwekwa wazi yaweze kumwangukia, basi walimlowanisha juu ya mwamba - Satiricon, kwa taratibu. Suidas, chini ya neno περιψημα, anaona kwamba ilikuwa ni desturi ya kujitolea mtu kila mwaka kufa kwa ajili ya usalama wa watu, kwa maneno haya, Περιψήμα ημων γενου, Uwe mtakasaji wetu; na baada ya kusema hivyo, kumtupa baharini kama dhabihu kwa Neptune.

Pengine ni kanuni hiyohiyo ambayo ilitumika kwa Yona alipowaambia watu waliokuwa karibu naye wamtupe nje ya meli kama dhabihu, hivyo kuchukua hatia yote na kukomesha dhoruba.

Waisraeli walikuwa wametoka Misri na walijua desturi za Wamisri za upatanisho. Kanuni hizi zinaletwa katika mfumo wa ibada ya Waisraeli ili kuwafundisha wanadamu kwamba Mungu atashughulikia tatizo la dhambi na kuondoa hatia katika taifa. Ni kanuni hiyohiyo ambayo Kayafa, Kuhani Mkuu katika wakati wa Kristo, alisihi wakati alipopendekeza kwamba taifa linapaswa kuua mtu mmoja ili kuokoa wengine.

> ….wala hamfikiri ya kwamba yafaa mtu mmoja afe kwa ajili ya watu, wala lisiangamie taifa zima. — Yohana 11:50

Pilato, katika kutafuta kuokoa maisha ya Yesu, anautolea umati wachague kama ni Yesu au Baraba atolewe kafara.

> "Lakini kwenu kuna desturi ya mimi kuwafungulia mtu mmoja wakati wa Pasaka; basi, mwapenda niwafungulie Mfalme wa Wayahudi? Basi wakapiga kelele tena kusema, Si huyu, bali Baraba. Naye yule Baraba alikuwa mnyang'anyi." — Yohana 18:39-40

Ni muhimu kwamba kubahatisha kwa nani anayeishi na nani ambaye anakufa kwa mfanano wa mbuzi wawili kunadhihirishwa katika kusulubishwa kwa Kristo. Umati wenye kigeugeu, wakichochewa na mihemko, wanamchagua Baraba aishi, na Kristo afe.

Kisa cha Yom Kippur ni Mungu akitafuta kuzungumza na wanadamu kwamba ametupatanisha na Yeye, lakini jinsi anavyowasiliana nasi ni kupitia njia zetu za kufikiri. Mawazo ya Mungu si mawazo yetu, na hivyo ili atufikie ni lazima aseme nasi kwa jinsi tunavyoelewa.[30]

Kisa cha Yom Kippur kwa kweli kinaturudisha mwanzo, kwani mambo yanaweza tu kuishia pale yalipoanzia; maana yake ni pale tu mambo ambayo yamezua mzozo yanaposhughulikiwa, ndipo mambo yanaweza kusuluhishwa.

Katika bustani, Adamu aliihamishia hatia yake kwa wengine wawili:

> Adamu akasema, "**Huyo mwanamke uliyenipa**" *awe* pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala. — Mwanzo 3:12

Kristo alikuwa Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu na hivyo anawakilishwa na mbuzi wa Bwana. Hawa alilazimika kubeba jukumu la kumwongoza mume wake katika dhambi. Akawa mbuzi wa Azazeli wa Adamu. Ulikuwa ni uzoefu wa nyikani kwake ambapo hatimaye aliangamia muda mfupi tu kabla ya miaka 1000 baadaye.

Mwishoni mwa historia ya dunia hii, viongozi wa kidini wa makanisa wataushinikiza ulimwengu kuabudu kulingana na maagizo yao. Wote lazima wapokee chapa ya mnyama ili waweze kununua na kuuza. Kama tulivyotazama katika sura ya 20, amri ya kifo itawekwa kwa wale wanaokataa kuabudu kulingana na mfumo wa ibada ya Jumapili iliyolazimishwa. Ulimwengu utaanza kupata maafa makubwa kutokana na kutunga sheria kinyume na sheria ya Mungu inayotuamuru kuitakasa Sabato ya siku ya 7.

Watu wa Mungu watalaumiwa kwa ajili ya misiba inayokuja juu ya dunia. Baadhi yao watauawa kama dhabihu kwa matumaini ya bure kwamba mtikisiko wa vitu vya asili na ubinadamu utakoma. Wakati Kristo

---

[30] [30] See chapter 16 of the book Agape available at fatheroflove.info.

atakapotokea kuwakomboa watoto wake, waovu watatambua kwamba wamedanganywa. Kisha wanatafuta kuweka hasira zao juu ya viongozi wa kidini waliowadanganya. Wanatafuta upatanisho kupitia kifo cha watu hawa wa kidini.

Hatimaye, Shetani ndiye aliyeongoza ulimwengu katika udanganyifu, na baada ya watakatifu kuchukuliwa mbinguni na waovu kuharibiwa kupitia matokeo ya uchaguzi wao wenyewe, Shetani anaachwa duniani kwa miaka 1000.

> Kisha nikaona malaika akishuka kutoka mbinguni, mwenye ufunguo wa **kuzimu**, na mnyororo mkubwa mkononi mwake. Akamshika yule joka, yule nyoka wa zamani, ambaye ni Ibilisi na Shetani, **akamfunga miaka elfu;** — Ufunuo wa Yohana 20:1-2

Minyororo ambayo Shetani na malaika zake wamefungwa nayo ni minyororo ya hali zao.

> Kwa maana ikiwa Mungu **hakuwaachilia malaika waliokosa,** bali kwa **minyororo ya kiza kinene** aliwatupa shimoni [Tartalo], akawatia katika hukumu, wakiwa wamehifadhiwa; — 2 Petro 2:4 (YLT)

Shetani hakumhurumia yeyote katika historia ya wanadamu. Aliwahukumu, kuwalaani na kuwashtaki wanadamu wote. Kwa miaka elfu moja, kama alivyohukumu, lazima aketi katika ukimya wa dunia hii iliyovunjika na kukabiliana na hukumu yake mwenyewe. Biblia inaliita shimo lisilo na mwisho au kuzimu. Kina cha kukata tamaa ambacho Shetani anakipitia ni kisichokuwa na mwisho. Atakuwa katika jela ya kutosamehe kwake. Yesu anadokeza hili katika mfano.

> Kisha Petro akamwendea akamwambia, Bwana, ndugu yangu anikose mara ngapi nami nimsamehe? Hata mara saba? Yesu akamwambia, Sikuambii hata mara saba, bali hata saba mara sabini. Kwa sababu hii ufalme wa mbinguni umefanana na mfalme mmoja aliyetaka kufanya hesabu na watumwa wake. Alipoanza kuifanya, aliletewa mtu mmoja awiwaye talanta elfu kumi. Naye alipokosa cha kulipa, bwana wake akaamuru auzwe,

> yeye na mkewe na watoto wake, na vitu vyote alivyo navyo, ikalipwe ile deni. Basi yule mtumwa akaanguka, akamsujudia akisema, Bwana, nivumilie, nami nitakulipa yote pia. Bwana wa mtumwa yule akamhurumia, akamfungua, akamsamehe ile deni. Mtumwa yule akatoka, akamwona mmoja wa wajoli wake, aliyemwia dinari mia; akamkamata, akamshika koo, akisema, Nilipe uwiwacho. Basi mjoli wake akaanguka miguuni pake, akamsihi, akisema, Nivumilie, nami nitakulipa yote pia. Lakini hakutaka, akaenda, akamtupa kifungoni, hata atakapoilipa ile deni. Basi wajoli wake walipoyaona yaliyotendeka, walisikitika sana, wakaenda wakamweleza bwana wao yote yaliyotendeka. Ndipo bwana wake akamwita, akamwambia, Ewe mtumwa mwovu, nalikusamehe wewe deni ile yote, uliponisihi; nawe, je! Haikukupasa kumrehemu mjoli wako, kama mimi nilivyokurehemu wewe? **Bwana wake akaghadhibika, akampeleka kwa watesaji, hata atakapoilipa deni ile yote.** Ndivyo na Baba yangu wa mbinguni atakavyowatenda ninyi, msiposamehe kwa mioyo yenu kila mtu ndugu yake. — Mathayo 18:21-35

Mtu aliyekuwa anadaiwa shukrani kwa bwana wake kwa kughairi deni lake aligeuka na kumhukumu mtu aliyekuwa na deni lake la kiasi kidogo. Maana ya kisa hiki ni kwamba wale ambao hawasamehe watakabiliwa na jela ya mateso ya kujihukumu na uchungu. Mungu hawatesi, lakini anawaruhusu kukabiliana na matokeo ya uchaguzi wao wenyewe. Mateso haya malaika walioanguka wanaogopa kuyakabili.

> Alipomwona Yesu alipiga kelele, akaanguka mbele yake, akasema kwa sauti kuu, Nina nini nawe, Yesu, Mwana wa Mungu aliye juu? **Nakusihi usinitese**. Kwa kuwa amemwamuru yule pepo mchafu amtoke mtu yule. Maana amepagawa naye mara nyingi, hata alilindwa kifungoni na kufungwa minyororo na pingu; akavikata vile vifungo, akakimbizwa jangwani kwa nguvu za yule pepo. Yesu akamwuliza, Jina lako nani? Akasema, Jina langu ni Jeshi; kwa sababu pepo wengi wamemwingia. **Wakamsihi asiwaamuru watoke kwenda shimoni.** Basi, hapo palikuwa na

> kundi la nguruwe wengi wakilisha mlimani; wakamsihi awape ruhusa kuwaingia wale. Akawapa ruhusa. Pepo wakamtoka mtu yule wakawaingia nguruwe, **nalo kundi lilitelemka gengeni kwa kasi, wakaingia ziwani, wakafa maji.** — Luka 8:28-33

Katika kisa hiki tunaona dhana za mateso na kuzimu zimeunganishwa. Malaika walioanguka wanatafuta kumlaumu Mwana wa Mungu kwa ajili ya mateso watakayokumbana nayo, lakini wanaelekeza woga wao wa kuhukumiwa kwa Kristo kwa sababu wamemhukumu kila mtu aliyewazunguka. Nguruwe wanaozama wanafanya kama ishara ya malaika wenyewe ambao walikataa lulu ya thamani kubwa. Malaika hawa walimkanyaga Mwana wa Mungu chini ya miguu yao na kudharau wema wake kwao.

> Msiwape mbwa kilicho kitakatifu, **wala msitupe lulu zenu mbele ya nguruwe,** wasije wakazikanyaga chini ya miguu yao, wakageuka na kuwararua. — Mathayo 7:6

Kuzidiwa kwa nguruwe baharini kunaonyesha mateso ya roho ya malaika waovu ambao watazidiwa na minyororo yao ya kutosamehe. Malaika hawa wana kauli mbiu:

Hatusamehi na hatusahau kamwe.

Maneno haya yanarudi kwa malaika walioanguka. Yote waliyofanya hawawezi kusahau, na kwa vile hawasamehi, hawana uwezo wa kuamini kuwa watasamehewa. Kwa hiyo, wanakaa gerezani kwa muda wa miaka 1000 hadi watakapokabiliana na utukufu kamili wa Mungu, wakati huo watakapolemewa na usadikisho wa dhambi zao na kuzama kama nguruwe baharini.

> Watakushusha hata shimoni; **nawe utakufa kifo chao waliouawa kati ya bahari.** — Ezekieli 28:8 (KJV)

Dunia hii itakapokwisha itakuwa ukiwa kabisa. Biblia inaeleza wakati ambapo hakuna mwanadamu duniani na kila kitu kitaharibika.

> Nikaangalia, na tazama, hapakuwa na mtu hata mmoja, na ndege wote wa angani wamekwenda zao. Nikaangalia, na tazama, shamba lililozaa sana limekuwa ukiwa, na miji yake yote ilikuwa imebomoka mbele za BWANA, na mbele za hasira yake kali. Maana BWANA asema hivi, Nchi yote itakuwa ukiwa; lakini sitaikomesha kabisa. — Yeremia 4:25-27 (KJV)

Shetani ameachwa duniani bila watu wa kuwajaribu na malaika walioanguka hawana la kufanya. Wanasukumwa katika bahari ya kukata tamaa na kusongwa na uchungu, hukumu, na mateso. Huku wanadamu wote wakiwa wamekufa au wako mbinguni, wao ndio pekee waliosalia kubeba madhara ya dhambi duniani. Mazingira ya historia yenye jeuri, upotovu, na uchafu wa mwanadamu sasa uko juu ya Shetani na malaika zake.

> Basi sasa, umelaaniwa wewe katika ardhi, iliyofumbua kinywa chake ipokee damu ya ndugu yako kwa mkono wako; — Mwanzo 4:11

Shetani sasa amelaaniwa kabisa kutoka katika dunia ambayo ilikuwa imefungua kinywa chake kupokea damu yote ambayo Shetani na malaika zake walikuwa wamewaongoza wanadamu kuimwaga.

Katika sherehe ya Siku ya Upatanisho, Kuhani Mkuu anaweka mikono miwili juu ya mbuzi aliye hai na kuungama, au, kama Kiebrania aonyeshavyo, anazitupa dhambi hizo juu ya mbuzi huyo.

> Na Haruni ataweka mikono yake miwili juu ya kichwa cha yule mbuzi aliye hai, na kuungama juu yake uovu wote wa wana wa Israeli, na makosa yao, naam, dhambi zao zote; naye ataziweka juu ya kichwa chake yule mbuzi, kisha atampeleka aende jangwani kwa mkono wa mtu aliye tayari. — Mambo ya Walawi 16:21

Je, hii ina maana gani? Je, Kristo anafanya kile ambacho Adamu alimfanyia hapo mwanzo? Je, Anamlaumu Shetani kwa kila jambo?

Yesu ametuambia kwamba yeye hahukumu wala hashutumu. Hata hivyo, tunakumbuka kile kinachotokea kwenye kiti cha hukumu cha Kristo.

> BWANA amejidhihirisha na kutekeleza hukumu; Amemnasa mdhalimu kwa kazi ya mikono yake. Zaburi 9:16

> Kwa maana hiyo siku ya BWANA i karibu juu ya mataifa yote; kama ulivyotenda, ndivyo utakavyotendwa; malipo yako yatakurudia juu ya kichwa chako mwenyewe. Obadia 1:15

> Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Wagalatia 6:7

Shetani atakutana na adhabu aliyoipanga. Kama vile Hamani aliyetengeneza mti wa kumtundika Mordekai juu yake (Esta 7:10), Shetani mwenyewe anakabiliwa na adhabu ambayo yeye mwenyewe amedai kwa wengine.

Kama vile watu waliomleta mwanamke aliyekamatwa katika uzinzi ili kumhukumu na Yesu badala yake aliandika kwenye mchanga na kuleta matendo yao wenyewe kwenye fahamuzao, vivyo hivyo Kristo ameona maisha yote ya Shetani. Kila kitu ambacho Shetani amefanya kimeandikwa juu ya Kristo. Kila dhambi ambayo wanadamu wamefanya imechorwa juu ya Yesu. "Haruni…ataungama juu yake [mbuzi] maovu yote ya wana wa Israeli…" Neno lililotumika hapa ni *kukiri*, si *kutamka laana*. Sehemu ya maana ya neno hili kukiri ni:

> (kwa mikono iliyonyooshwa); kuomboleza sana (kwa kukunja mikono)

Kama kisa cha Kaini, Kristo hakutamka adhabu juu ya Kaini aliposema au kukiri matendo ya Kaini aliyofanya na kile ambacho kingekuwa matokeo ya matendo yake. Aliyazungumza huku akitokwa na machozi na huzuni kwa yale yatakayompata.

> Basi sasa, umelaaniwa wewe katika ardhi, iliyofumbua kinywa chake ipokee damu ya ndugu yako kwa mkono wako; utakapoilima ardhi haitakupa mazao yake; utakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani. — Mwanzo 4:11-12

Kama Kaini, Shetani atakuwa mkimbizi na mzururaji duniani kwa miaka 1000, isipokuwa atakuwa akiishi katika angahewa ya miaka 6000 ya dhambi. Kristo

anakiri hili juu ya Shetani, kama alivyokiri juu ya Kaini kile ambacho kingempata kwa sababu ya uovu wake.

Kwa mtazamo wa kibinadamu tunasoma hili kama kuhamishia lawama kwenye chanzo asili cha tatizo, hivyo kuondoa hatia kwa taifa zima. Lakini haki ya Mungu haitaji aina hii ya uhamisho wa deni; ni haki ya Shetani, ambapo dhambi haiwezi kuondolewa/kuponywa/kusamehewa, ambayo inadai utaratibu huu. Kwa Mungu, kinachotokea ni mchakato wa kusema kwaheri. Ni wakati wa ukweli ambapo Shetani lazima akabiliane na matendo ambayo amefanya. Kristo hafanyi hivi katika roho ya kushutumu na kubadilisha lawama. Mawazo yake sio mawazo yetu. Kristo na Baba wamewasamehe bure waliookolewa kwa dhambi zao zote. Hawahitaji dhabihu ili dhambi zipate kusamehewa.

Kupitia ishara ya jinsi wanadamu wanavyoelewa upatanisho na kuondolewa kwa hatia, wanadamu wanaridhika kwamba Mungu anatuambia kwamba tatizo la dhambi litatatuliwa.

Kuna wengi wanaoamini kuwa mbuzi wa Azazeli ni Kristo kwa sababu dhambi zote za watu zinaungamwa juu yake. Tunakumbuka kwamba mbuzi huchaguliwa kwa bahati nasibu, mbuzi yeyote kati ya hawa angeweza kutimiza nafasi hii. Neno la Kiebrania la mbuzi lenyewe linajumuisha maana ya shetani, na vivyo hivyo neno *Azazeli*, jina la mbuzi wa Azazeli.[31] Sherehe nzima inahusu mfumo wa haki wa Shetani na inatuthibitishia kwamba dhambi itaondolewa hatimaye kutoka katika ulimwengu.

Mungu hakudai dhambi zetu zote ziwekwe juu ya Kristo ili kumaliza tatizo la dhambi. Sisi kama wanadamu tulihitaji hili kwa sababu Adamu alilidai hapo mwanzo. Ndio njia pekee tunayoelewa kuwa hatia inaweza kuondolewa.

> Na hiyo miaka elfu itakapokwisha, Shetani atafunguliwa, atoke kifungoni mwake; naye atatoka kuwadanganya mataifa walio katika pembe nne za nchi, Gogu na Magogu, kuwakusanya kwa vita, ambao hesabu yao ni kama mchanga wa bahari. Wakapanda juu ya upana wa nchi, wakaizingira kambi ya watakatifu, na mji

[31] 1906 Jewish Encyclopedia entry: http://jewishencyclopedia.com/articles/2203-azazel

> huo uliopendwa. Moto ukashuka kutoka mbinguni, ukawala. — Ufunuo wa Yohana 20:7-9

Mwishoni mwa miaka 1000 waovu watafufuliwa tena. Shetani mara moja anaanza tena kazi yake ya udanganyifu juu ya wanadamu waovu. Hivyo anaachiliwa kutoka kwenye minyororo yake ya utusitusi kwa kuwa ana kitu cha kumkengeusha. Shetani hajabadilika. Hangeweza kusamehe hivyo hawezi kuamini kwamba anaweza kusamehewa. Shetani huwashawishi waovu kujaribu kuuteka mji. Wameazimia kuwaua wakaaji wa jiji la kimbingu ambalo limeshuka kutoka mbinguni kuja duniani.

> Mungu hakudai dhambi zetu zote ziwekwe juu ya Kristo ili kumaliza tatizo la dhambi. Sisi kama wanadamu tulihitaji hili kwa sababu Adamu alilidai hapo mwanzo.

Waovu wanatafuta kuuteka mji wa Mungu, lakini utukufu wa tabia ya Mungu iliyofunuliwa katika Mwanawe unawafunika na hatia. Hofu ya kuja katika uwepo wa Mwana wa Mungu katika uungu Wake kamili husababisha hukumu yao ya mauaji irudi juu yao. Kadiri walivyokuwa na chuki zaidi kwa Kristo na waaminifu, ndivyo wanavyohisi hatia zaidi wanapoutazama utukufu wa Mungu na Mwanawe. Katika hali ya kukata tamaa ya mwisho wanageukia kila mmoja wao kwa wao na kujiangamiza wenyewe, hata wanapokandamizwa na hukumu yao ya kifo ambayo walikuwa wameipitisha dhidi ya waadilifu, hivyo wanazama kama nguruwe baharini.

> “Nami nitaita upanga, uje juu yake katika milima yangu yote, asema Bwana MUNGU; nao upanga wa kila mtu utakuwa juu ya ndugu yake.” — Ezekieli 38:21

> Tena itakuwa siku hiyo, ya kwamba mashaka makubwa yatokayo kwa BWANA yatakuwa kati yao; na kila mmoja wao atakamata mkono wa jirani yake, na mkono wake utainuliwa ili kushindana na mkono wa jirani yake. — Zekaria 14:13

> Maana silaha zote za mtu mwenye silaha wakati wa mshindo, na mavazi yaliyofingirishwa katika damu, yatakuwa tayari kuteketezwa, yatakuwa kuni za kutiwa motoni. — Isaya 9:5

> Basi, tazama, nitaleta wageni juu yako, watu wa mataifa wenye kutisha; nao watafuta panga zao juu ya uzuri wa hekima yako, nao watautia uchafu mwangaza wako. Watakushusha hata shimoni; nawe utakufa kifo chao waliouawa kati ya bahari. — Ezekieli 28:7-8

Kama Farao na majeshi yake waliozama baharini wakitafuta kuwaua watu wa Mungu, na kama nguruwe waliosonga baharini, ndivyo Shetani na waovu watakavyofikia mwisho wao.

Tunapowatazama wale mbuzi wawili, na tuone katika huu mfumo wetu wa kibinadamu wa kuwalaumu wengine kwa dhambi zetu. Hebu tutubu na kujinyenyekeza mbele za Mungu na kujifunza jambo kuu la mbuzi wawili - watu lazima walaumu mtu mwingine na kuweka hatia yao kwa mwingine. Kupitia mfano huu wa mbuzi wawili, Bwana anaakisi kwetu katika kioo moyo wa uovu wetu, akiturudisha kwa Adamu katika bustani na dhambi ya kuelekeza lawama na kutafuta mbuzi wa Azazeli ili kulipia dhambi zetu.

Tunyenyekeze nafsi zetu mbele za Mungu na tuache kuwalaumu wengine kwa matatizo yetu. Ni waume na wanawake wangapi kila siku wanaohamisha hatia zao kwa wenzi wao ili kulipia dhambi zao? Je, ni wangapi wanaokaa na kutafuta ni nani atakayelaumiwa kwa hisia zao za hatia? Siku ya Upatanisho inatuita sisi kuacha kuwatwika wengine jukumu la mateso yetu. Na tuache kuhukumu wengine na kujiachilia wenyewe katika mikono yenye upendo ya Baba yetu ambaye atafanya mambo yote yafanye kazi pamoja kwa ajili ya manufaa yetu.

> Atarejea na kutuhurumia; atayakanyaga maovu yetu; nawe utazitupa dhambi zao zote katika vilindi vya bahari. Wewe utamtimilizia Yakobo kweli yako, na Ibrahimu rehema zako, ulizowaapia baba zetu tangu siku za kale. — Mika 7:19-20

SURA YA 24

# Bila ya Mwombezi

Kama tulivyojadili katika sehemu kadhaa, mtazamo wetu wa kibinadamu wa haki unahusisha kipindi cha ufuatiliaji ambapo wale wanaoshukiwa wanapata muda wa kubadili tabia zao. Wamepewa kipindi cha rehema ili kuingia kwenye njia sahihi. Katika mfumo wetu wa mahakama tuna wanasheria ambao watamtetea mtu anayehojiwa ili kuchelewesha hukumu wakati haiwezi kuondolewa.

Iwapo mtu huyo atapatikana kuwa na hatia baada ya muda wa neema uliowekwa, basi haki ya utendaji inachukua mkondo wake na mchakato wa uteyezi hukoma. Utekelezaji wa haki unahitaji kwamba utetezi wote lazima ukome na mwenye hatia lazima aadhibiwe kwa mujibu wa sheria. Njia zote za kukata rufaa zikiisha, mtetezi au wakili hawezi tena kumtetea mtu huyo.

Kuhusiana na nafsi ya Kristo, anaishi daima ili kufanya maombezi kwa ajili yetu.

> Bali yeye, kwa kuwa akaa milele, anao ukuhani wake usioondoka. Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; **maana yu hai sikuzote ili awaombee**. — Waebrania 7:24-25

Nafsi inapotambua kwamba ina hatia ya kuvunja sheria ya Mungu, inamgeukia Kristo kama mwombezi wake na kuamini kwamba Kristo atamwombea kwa Mungu ili ampe rehema.

> Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki, — 1 Yohana 2:1

Kutokana na mitazamo yetu ya kibinadamu kuhusu haki, Kristo anachukuliwa kuwa anatuombea ili Mungu atupe rehema. Lakini Mungu daima atawapa rehema wale wanaomwomba kwa sababu Mungu ni upendo.

Ukweli ni kwamba Kristo anatuombea kulingana na mitazamo yetu ya haki. Anakutana nasi tulipo na kwa hiari anatushika mkono na kutuwasilisha kwa Baba.

Kwa sababu ya ukweli kwamba Kristo ameishi kama mwanadamu na alikuwa tayari kufa kwa ajili yetu, tunaweza kuwa na uhakika kwamba Mungu atamsikia Mwanawe kwa niaba yetu.

> Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji. — Waebrania 4:15-16

Katika mwanzo wa safari yetu ya Kikristo huwa tunahisi kwamba Kristo anamshawishi Baba kusitisha dai lake la haki dhidi yetu la kutuua kwa sababu ya dhambi zetu. Ukweli ni kwamba Kristo anatembea nasi katika ufahamu wetu mbaya wa Baba yake, wakati wote akituvuta karibu naye ili tuanze kuona kwamba hukumu inatoka kwetu sisi wenyewe na si kutoka kwa Mungu.

Kwa uhalisia, ombi la Kristo liko kwetu kwamba tunwamini Baba yake kwamba yuko tayari kusamehe, kwamba Yeye ni mwingi wa rehema, na hatimaye kumjua Mungu kama vile Kristo anavyomjua Mungu. Kitu pekee

ambacho Kristo anahitaji kumshawishi Baba yake ni utayari wake wa kuendelea kubeba uzito wa dhambi za ulimwengu mzima. (Isaya 63:9)

> kama vile Baba anijuavyo, nami nimjuavyo Baba. Nami nautoa uhai wangu kwa ajili ya kondoo. — Yohana 10:15

Wale wanaokataa kukubali ukweli wa tabia ya Mungu, kwamba Yeye hahukumu, watastahimili hukumu ambayo wanaamini kwamba lazima Mungu aitekeleze. Katika utambuzi wa dhambi zao wenyewe wanahisi kwamba lazima wakatiliwe mbali, bila mwombezi, kwa ajili ya dhambi zao.

Mungu atawaruhusu wale wote wanaomwamini Mungu kupita katika mchakato huu. Huu ndio wakati wa taabu ya Yakobo ambao tulijadili hapo awali. Kama ambavyo sisi sote tumetiwa muhuri wa kanuni za haki za Adamu, sisi sote tutapitia mchakato katika nyakati za mwisho ambapo tutahisi kwamba tutakatiliwa mbali kwa sababu ya dhambi zetu.

> Akaona ya kuwa hapana mtu, akastaajabu kwa kuwa hapana mwombezi; basi, mkono wake mwenyewe ndio uliomletea wokovu; na haki yake ndiyo iliyomsaidia. — Isaya 59:16

Mstari huu una matumizi ya msingi kwa kuja kwa Kristo mara ya kwanza. Mungu alitafuta watu kabla ya Kristo kuja kuakisi nuru ya ukweli na kufunua tabia yake, lakini hapakuwapo. Kwa hiyo, Mungu alimtuma Mwanawe ulimwenguni ili kudhihirisha haki yake. Maandiko yanasema kwamba mambo haya yote yameandikwa ili kutuonya sisi ambao mwisho wa dunia umetujia. (1 Wakorintho 10:11). Maandiko yanazungumza juu ya wakati ambapo Kristo atasitisha kazi yake ya uombezi mbinguni.

> Hekalu likajazwa moshi uliotoka kwenye utukufu wa Mungu na uweza wake. Wala hapakuwa na mtu aliyeweza kuingia ndani ya hekalu, hata yatimizwe mapigo saba ya wale malaika saba. — Ufunuo wa Yohana 15:8

> Wakati huo Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako; na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo

> huo; na wakati huo watu wako wataokolewa; kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile. — Danieli 12:1

Wakati ulimwengu unapoingia katika machafuko makubwa katika siku za mwisho na watakatifu wa Mungu wanakabiliwa na kifo, dhambi zao zote huja mbele yao na wanajaribiwa kuhisi kulemewa.

Wale ambao wamejifunza kwamba Mungu kamwe hamtupi mtu yeyote na kwamba Yeye ni mwenye rehema sikuzote wataona kwamba "mkono wao wenyewe utawaletea wokovu na kwamba haki yake mwenyewe itamtegemeza." Hii ina maana kwamba kwa sababu wanashikilia sana ahadi za Mungu na kuamini kwamba Yesu ndiye ufunuo kamili wa Baba, na kwa hiyo Mungu hatawaacha, wanaimarishwa katika imani hii. Hii ndiyo maana ya utukufu wa Mungu kulijaza hekalu. Watu wa Mungu huona tabia ya Mungu kuwa ya rehema na neema mbele ya maisha yao ya dhambi. Kristo hahitaji tena kuketi Patakatifu pa Patakatifu kama mwombezi wa dhambi. Watakatifu wanashinda hisia zao za kujihukumu na kuacha kuamini kwamba Mungu anawahukumu. Kama Yesu alivyomwambia mwanamke, "wala mimi sikuhukumu."

Daima ni kwamba imani inayotegemeza ya watakatifu ndiyo imani halisi ya Yesu ambayo Kristo anawapa. Watakatifu hawa hawategemei stahiki zao wenyewe bali wamejifunza kumtumaini Kristo pekee. Wanatoka wakati wa taabu ya Yakobo wakiwa wametiwa muhuri katika ukweli kwamba Mungu hatawahukumu kamwe, na wanachagua kukubali hukumu yake ya upendo juu yao badala ya hukumu yao ya awali ya kujihukumia adhabu.

Hii ina maana kwamba wenye haki waaminifu wanaweza kuishi bila mwombezi wa dhambi. Dhambi ni uvunjaji wa sheria na sheria ni nakala ya tabia ya Mungu. Wale wanaoacha kuamini kwamba Mungu anahukumu na kuua wanatiwa muhuri katika imani hii kupitia jaribio la taabu ya Yakobo. Dhambi ya mwanadamu ya kuamini kwamba Mungu huwakatilia mbali watu inakuzwa katika matukio ya mwisho ya historia ya mwanadamu ili kuwatia muhuri watu wa Mungu katika ukweli. Watu wa Mungu wanapojaribiwa kwa wazo kwamba watakatiliwa mbali kwa sababu ya dhambi zao, imani ya Kristo ndani yao inajikita kwa nguvu zaidi katika

upendo wa Mungu na wanakataa kukubali mashaka; wao ni washindi; wao ni Israeli wa Mungu.

Kwa hiyo, kupitia hili wanaweza kuishi bila mpatanishi ambaye alitakiwa kufunika vichwa vyao huku wakihofu kwamba Mungu angewaadhibu na kuwadhuru. Kristo hahitaji tena kuwasaidia watu wa Mungu kwa njia hii. Wanakuja katika nuru kamili ya ukweli wa injili na Kristo anaishi milele ili kuwaombea kwa ajili ya haki na kuwapa mambo yoyote wanayomwomba. Lakini hawaogopi kamwe kuhukumiwa au kuhisi uhitaji wa kwamba damu lazima imwagike ili waokolewe. Wanaachana na mfumo wa haki wa dhabihu na sadaka.

Wale ambao hawaji katika nuru ya ukweli kuhusu tabia ya Mungu watakabiliwa na hukumu wanayofikiri Mungu ataifanya. Wanajisikia kutengwa na Mungu kwa sababu ya dhambi zao na wanahisi kwamba Kristo amewaacha kuikabili ghadhabu ya Mungu na kuhisi kutengwa.

> Kwa kuwa mtu awaye yote asiyejitesa mwenyewe siku iyo hiyo, atakatiliwa mbali na watu wake. — Mambo ya Walawi 23:29

Wale wanaojinyenyekeza katika kipindi cha mwisho cha historia ya dunia na kukiri dhambi yao ya kuamini kwamba Mungu alikuwa mharibifu mwenye kuhukumu waovu hawatakatiliwa mbali katika matukio ya mwisho ya historia ya dunia kwa sababu wanamjua Mungu wao na wamemngojea.

> Na wao wafanyao maovu juu ya hilo agano atawapotosha kwa maneno ya kujipendekeza; **lakini watu wamjuao Mungu wao watakuwa hodari**, na kutenda *mambo makuu.* — Danieli 11:32

Wale ambao hawasomi na kuyachunguza Maandiko ili kuona tabia ya kweli ya Mungu watazidiwa na dhambi zao. Kwa sababu wanashikilia mfumo wa haki wa Adamu, watakatiliwa mbali kutoka miongoni mwa watu wa Mungu.

Sababu pekee ambayo watu wa Mungu wanapaswa kupita katika jaribu la mwisho la kutokuwa na mwombezi ni kwa sababu wanadamu huamini kwamba rehema inapoisha hakuna maombezi tena. Kristo anaishi daima ili kutoa baraka, neema na upendo kwa wale wanaomwamini. Hataacha kuwapa wale wanaoamini. Itawezekana tu kuamini hili wakati wa taabu ya

Yakobo ikiwa tutaacha mtazamo wetu mbaya wa tabia ya Mungu na kuja katika mfumo Wake wa haki wa kweli. Haki yake ni kutoa rehema na kuwapa neema kwa hiari wote wanaoiomba.

Hatuna cha kuogopa wakati huu wa kuishi bila mwombezi. Wenye haki hupoteza kabisa hofu yao ya kile walichokiwazia kuwa ni hukumu ya Mungu, na kushikilia ukweli kwamba hawahitaji maombezi dhidi ya Mungu mwenye hasira ambaye atawaua kwa ajili ya dhambi zao. Kwa waovu, mawazo yao ya uongo yatawalemea na kuacha kumwomba Kristo neema, kwani hawaamini tena kwamba imetolewa. Katika kesi hii kutakuwa na kilio na kusaga meno. Njoo katika nuru ya ukweli juu ya jambo hili na ufurahie habari njema kwamba hakutakuwa na mwombezi wa dhambi mwishoni mwa rehema.

SURA YA 25

# Chronos na Kufungwa kwa Rehema

Kuna kipengele kingine muhimu kwenye kanuni za hukumu ambacho wanadamu wamekumbatia na hiki kinahusiana na saikolojia ya wakati.

Katika hadithi za Santa Claus, kuna kipengele cha wakati kinachohusishwa. Ni bora ujihadhari kwa sababu Santa Claus atakuja mjini tarehe 25 Desemba mwishoni mwa mwaka.

Tunakuzwa kama watoto wanaohitajika kufanya mitihani yenye kikomo cha muda au tarehe ya mwisho. Kwa nini neno kufa, kama ilivyo katika tarehe ya mwisho, limeunganishwa na dhana ya kikomo cha wakati?

Kuna tofauti gani ya kisaikolojia kati ya kumpa mtu zana na rasilimali zote anazohitaji kuunda kitu na kukifanya kitu hicho akiwa amepewa tarehe ya mwisho? Tarehe za mwisho ni matumizi ya nguvu ili kufikia matokeo kwa yule anayedhibiti wakati.

Unapounganisha tarehe ya mwisho na tishio la adhabu au kifo, shinikizo linalowekwa ni unyanyasaji wa kisaikolojia.

Katika utafiti wa kuchunguza uhusiano kati ya shinikizo la wakati na ubunifu, iligunduliwa kuwa:

> …shinikizo la wakati, katika viwango vya wastani hadi vya juu ambavyo kwa ujumla vinashughulikiwa katika mashirika ya kisasa,

huwa na athari hasi ya moja kwa moja kwenye mchakato wa bunifu wa utambuzi.[32]

Haionekani kuwa wazi kwa watu wengi kwamba kutishia watu kwa adhabu ikiwa hawatatenda ndani ya muda fulani kuna uwezekano wa athari tofauti kuliko matokeo yaliyokusudiwa.

Wazazi wangapi wametoa dhana za namna Hii, "Nitahesabu hadi 3, na ikiwa hutafanya kile ninachokutaka ukifanye utapata kipigo na/au kuwekwa mahabusu!"

Kutoa kikomo cha muda kunamaanisha ufuatiliaji, hukumu na adhabu kwa kushindwa kufuata. Utumiaji wa wakati kama kichocheo cha tabia hutekelezwa nje ya mfumo wa kukata tamaa ambao unatarajia anayesikiliza asifanye kazi hiyo isipokuwa kama kuna tarehe ya mwisho, na kwa hivyo shinikizo la wakati humwalika msikilizaji kuasi.

> Kutoa kikomo cha muda kunamaanisha ufuatiliaji, hukumu na adhabu kwa kushindwa kufuata.

Kwa nini wakati unaweza kutumika kama mshinikizaji? Jibu rahisi ni kwamba sisi sote tunakufa na kwa hivyo sote tunao wakati mfupi. Muda ni rasilimali adimu kwa jamii ya wanadamu na kwa hivyo unaweza kutumika kama kichocheo cha kubadilisha tabia ya mwanadamu.

Hii ni tofauti kabisa kwa Mungu.

> Maana yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele, ambaye jina lake ni Mtakatifu, asema hivi; Mimi nakaa mimi mahali palipoinuka, palipo patakatifu, pamoja na yeye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea, ili kuzifufua roho za wanyenyekevu, na kufufua moyo ya waliotubu." — Isaya 57:15

Baba yetu aliye mbinguni anakaa katika hali ya umilele. Kwa sababu ya uwepo wake wa milele, muda sio bidhaa ambayo inathaminiwa kwa jinsi tunavyouthamini. Chukulia mfumo wa usambazaji na wa mahitaji. Mungu

---

32 https://www.hbs.edu/faculty/Publication%20Files/02-073_03f1ecea-789d-4ce1-b594-e74aa4057e22.pdf

ana wakati usiokuwa na kikomo; kwa hivyo, muda hauna athari sawa kwake kama ulivyo na athari kwetu. Rejea yake ya wakati ni tofauti kabisa.

> Lakini, wapenzi, msilisahau neno hili, kwamba kwa Bwana siku moja ni kama miaka elfu, na miaka elfu ni kama siku moja. — 2 Petro 3:8

Kila siku kwake imejitosheleza katika kutunza viumbe vyake vyote. Kwa siku moja, Baba yetu anafanya kazi ya miaka 1000 katika hesabu yetu na zaidi. Kinyume chake, mtazamo Wake kwa watoto Wake na utunzaji usio na kikomo kwetu sote hufanya muda upite kama miaka 1000 kwa siku. Tunajua hisia hii tunapokuwa na wale tunaowapenda na tuko katika mazungumzo ya kina, tunapoteza habari ya wakati. Baada ya masaa kadhaa tunatazama saa na kushtuka kwamba muda umeenda. Kwa hiyo, tunaweza kuonja hisia za umilele katika nyakati hizo, lakini bado mawazo yetu kuhusu wakati ni tofauti. Hii ni kwa sababu ya ukweli mmoja rahisi: sote tunakufa.

Kifo hubadilisha thamani ya wakati. Kwa watu wengi, wakati ni wa thamani sana na kwa hivyo ni mojawapo ya bidhaa muhimu zaidi ambayo kwa hiyo tunafanya biashara. Ndiyo maana tuna usemi kama “wakati ni pesa” na “kutumia” wakati.



Kwa kutambua mambo haya, Wagiriki walikuwa na mungu aitwaye Chronos ambaye alikuwa mfano wa wakati. Hadithi za Kigiriki ni ngumu, lakini Chronos wakati fulani alichanganyikiwa na Cronus ambaye alikuwa mwonekano wa Titan wa uharibifu wa wakati juu ya watu. Kwa maana hii,

wakati huharibu watoto wake. Cronus anaonyeshwa kama mungu anayekula watoto wake mwenyewe. Hadithi ya wahusika hawa wawili iliunganishwa na kuwa Baba wakati.[33]

Pia inavutia kwamba tonote alikuwa akichukuliwa kuwa na umbo la nyoka mwenye vichwa vitatu. Vichwa hivyo vilikuwa vya mtu, fahali na simba.[34]

Chronos, anayejulikana pia kama Aeon, alijiumba na hakupokea urithi kutoka kwa mtu yeyote. Anaonyeshwa kama mzee mwenye ndevu. Anabeba kitu mfano wa mundu kuashiria uvunaji wake wa ubinadamu na uharibifu wa wakati.

Ananke lilikuwa jina la mungu mwingine wa awali katika simulizi ya Kigiriki, mtu wa umuhimu na hatima. Alionyeshwa akiwa ameshika usukani, na alikuwepo wakati ulimwengu ulipoanza pamoja na mshirika wake Chronos (wakati). Ananke na Chronos wote walikuwa na sura ya nyoka, na walikuwa wameunganishwa na kuzunguka yai la kwanza la maada.[35]

Dhana ya kiumbe ambaye ni baba ambaye hakuumbwa wala kuzaliwa ambaye ana ndevu ndefu na anayeishi milele hufanya iwe rahisi kwa watu kumfananisha na Mungu wa Biblia.

Kwa wote wanaoishi chini ya utawala na hofu ya kifo, si vigumu kuona jinsi watu wanavyoweza kumchanganya Mungu wa kweli na mambo mengi ya Chronos. Kwa wale walio na uhakika wa uzima wa milele, wakati hupoteza nguvu zake na hofu ya kifo inashindwa, na hivyo kufichua asili ya nyoka wa kweli wa mungu Chronos.

Umilele ni uwepo tofauti kabisa kuliko wakati. Wakati unaohusishwa na hofu ya kifo hutuacha tukiwa na hasira na wale "wanaopoteza" wakati wetu au wasiofanya kazi kwa ufanisi. Umilele ni uzoefu wa mapumziko kamili na amani. Ni dhana iliyounganishwa na Sabato. Katika kitabu cha Mwanzo, tunaona kwa kupendeza kwamba siku ya saba ya juma la kwanza haisemi ikawa jioni ikawa asubuhi siku ya saba. Husema hivyo tu kwa siku sita za kwanza. Kuna kuunganishwa kati ya Sabato na kutokuwa na kikomo cha

[33] https://en.wikipedia.org/wiki/Chronos
[34] https://www.greekmythology.com/Other_Gods/Primordial/Chronos/chronos.html
[35] https://www.greekmythology.com/Other_Gods/Primordial/Ananke/ananke.html

wakati. Ni siku ambayo tumeunganishwa kwa nguvu zaidi na Baba yetu wa mbinguni na tunaonja kwa undani zaidi amani ya Mungu wakati huo.[36]

Mtume Paulo, mtu msomi sana, alitoa kauli kadhaa ambazo zingewapa changamoto sana wasomaji wake wa Kigiriki.

> Basi usiuonee haya ushuhuda wa Bwana wetu, wala usinionee haya mimi mfungwa wake, bali uvumilie mabaya pamoja nami kwa ajili ya Injili, kwa kadiri ya nguvu ya Mungu; ambaye alituokoa akatuita kwa mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu sisi, bali kwa kadiri ya makusudi yake yeye na neema yake. Neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele, [G5550] [G166] [kabla ya Chronos, aeonious]. — 2 Timotheo 1:8-9

Paulo anazungumza juu ya Kristo kama aliyekuwepo kabla ya Chronos Aeon. Huu ni mtazamo tofauti kabisa wa ulimwengu na kile ambacho Wagiriki walikielewa. Neno kuu katika Kiebrania kwa umilele ni Olam; wakati ulio nje ya akili au nje ya macho; juu ya upeo wa macho. Neno hili Olam linatumika wakati wa kumzungumzia Kristo kwa njia ifuatayo:

> Lakini wewe, Ee Bethlehemu Efrata, ni kijiji kidogo tu kati ya watu wote wa Yuda. Lakini mtawala wa Israeli atakuja kutoka kwako, ambaye asili yake ni kutoka nyakati za zamani. [Olam] — Mika 5:2 (NLT)

Kwa akili ya Kigiriki, haiwezekani kwa mtu ambaye ni wa milele kuwa na mwanzo. Hili si gumu kwa akili ya Kiebrania. Kristo ana mwanzo wake ambao ni kabla ya wakati. Ni mahali ambapo ni zaidi ya akili ya asili ya mwanadamu kuelewa. Hili linaruhusu kwa urahisi mwanzo wa Kristo na dhana ya Kiebrania ya umilele kuwepo pamoja ndani yake.


Kwa akili ya Wagiriki, wakati ni mungu mkuu aliyepo. Haiwezekani kuwaza mfumo ulio nje ya wakati. Wakristo wanaotafuta kumtambulisha Kristo kama Mungu wa kweli bila kufahamu wanatoa heshima kwa Chronos kwa kudai kwamba Kristo lazima awe aliishi katika wakati wa milele na hana mwanzo. Hili ni kuufanya wakati na umilele kuwa dhana moja.

---

[36] For more on this subject see the book Fountain of Blessing at fatheroflove.info


Kutafuta kuunganisha dhana ya Kiebrania ya umilele na dhana ya Kigiriki ya Chronos kunaharibu uwezekano wa Kristo kuwa Mwana wa kweli wa Mungu aliyezaliwa katika umilele. Kimsingi, Chronos anaruka kutoka eneo la mwisho la Kigiriki la wakati hadi kwenye chumba cha enzi cha umilele na kumuua Mwana wa Yehova. Chronos anasema kwamba Mungu hawezi kuwa na Mwana wa kimungu, kwa sababu uungu kulingana na Chronos unamaanisha kuwepo bila kuzaliwa na kutokuwa na baba.

Wakristo wengi hawawezi kumkubali Kristo akiwa na mwanzo wakati fulani katika umilele kwa sababu hii, kwa njia ya Kigiriki ya kufikiri, inamfanya Yeye kuwa mdogo kuliko Chronos/Aeon. Kwa hiyo, kuwa sawa na Mungu mkuu, Kristo hawezi kuwa na mwanzo hata kidogo, hivyo kuharibu uhalisi wa urithi wake kutoka kwa Baba yake. Kama tulivyokwisha sema, akili ya Kiyunani huona wakati na umilele kama kitu kimoja, kiasi chake kisicho na kikomo. Lakini huu sio umilele, huu ni kuwa na hali ya kudumu.[37]




Dhana ya Kiebrania ni tofauti :

[37] https://en.wiktionary.org/wiki/sempiternity - states (philosophy) Existence within time but infinitely into the future, as opposed to eternity, understood as existence outside time.




Kristo alikuwepo kabla ya wakati au Chronos kama Paulo alivyoeleza. Anatoka katika ulimwengu wa milele hadi wa wakati; hata hivyo Anaishi daima katika uzoefu wa umilele kwa kuwa Haogopi kifo, wala hana kikomo cha wakati. Tena, Paulo anatuambia kuhusu kanuni hii anaposema:

> Katika tumaini la uzima wa milele, ambao Mungu, asiyeweza kusema uongo, aliahidi kabla ya [G4253] ulimwengu kuanza; [ulioahidiwa kabla ya Aeon(ios), Chronos] — Tito 1:2 (KJV)

Sababu ya uzoefu wetu wa maisha kulenga wakati kimsingi ni kwa sababu ya hofu ya kifo. Sisi ni watumwa wa Chronos kwa sababu hatuwezi kufikiria jinsi ambavyo ulimwengu ungeweza kufanya kazi bila kifo. Lakini kwa njia ya Kristo tunaweza kupata umilele sasa hivi ikiwa tuna uhakika wa uzima wa milele; si kwa kuitamani tu au kutumainia bure, bali tukijua yakini tunao katika Kristo Yesu.

Tofauti kati ya wakati na umilele inaweza kulinganishwa na muziki mzuri unaoimbwa unapopiga gitaa. Muziki una mdundo lakini hausisitizwi. Msisitizo ni juu ya maneno, na muda wa muziki huweka tu vipengele vya muziki, sauti na usindikizaji pamoja. Ikiwa kifaa kikubwa cha ngoma kingeongezwa kwenye muziki wa gitaa murua ili kusisitiza mdundo wa muziki ili ngoma zitawale muziki, itabadilisha radha kabisa. Ujumbe katika muziki umemezwa katika muda ule ambao mdundo ulipokolezw kupita kiasi wa muziki. Kuletwa kwa kifo ulimwenguni kulikuwa kama kuongeza

mdundo katika uzoefu wetu wa maisha. Muda unasonga kwa kasi katika maisha yetu kwa sababu uhaba wake hutusukuma mbele kufikia kile tunachokiweza kabla ya kifo. Tunapojua tuna uzima wa milele, mdundo unarudi katika jukumu lake la upole, la amani la kuweka mambo pamoja kwa njia iliyopangwa; utulivu unarudi na tafakuri inapanuka.

Sehemu hii ya wakati hufanya jukumu muhimu katika kuelewa mchakato wa hukumu katika Maandiko. Katika sura ya 15 tuliangalia mfumo wa kinabii unaotuambia ni lini hukumu ingeanza. Daniel aliambiwa kwamba itachukua miaka 2300 hadi Patakatifu kutakaswa, na kanuni zilizotumika wakati wa Yom Kippur zingepata utimilifu wa mwisho kuanzia 1844 na kuendelea.

Kuanzia wakati huu Mungu anachunguza vitabu vya kumbukumbu katika hukumu ili kuona ni nani anayeishi na nani anayekufa. Hata hivyo, kama tulivyogundua katika sura ya 19, muktadha wa hukumu ni kwamba Mungu anawatetea watu wake kutokana na mashtaka ya Shetani dhidi yao. Tukio hili linaonekana kupitia jicho tofauti sana na watu wengi. Hukumu inaonekana kama uzoefu wa “bora ujihadhari”.

Hukumu kabla ya marejeo ni muhimu ili kufichua ibada yetu ya kuhukumu inayotegemea wakati.

Hili linageuza hukumu kuwa uzoefu wa “una muda fulani wa kujirekebisha na kuwa sawa na usipofanya hivyo basi utauawa.” Mtazamo huu wa hukumu una athari iliyo kinyume kwa mwenye dhambi na kile kilichokusudiwa. Hofu hii hufanya kushinda dhambi kuwa jambo lisilowezekana kwa sababu hakuna hofu katika upendo (1 Yohana 4:18).

Fundisho zima la hukumu inayotokea wakati fulani kabla ya Ujio wa Pili kwa hakika huongeza msukumo wetu unaotegemea wakati na kudhihirisha ibada yetu ya sanamu kwa Chronos. Wakristo wengi hukataa wazo la hukumu kabla ya Ujio wa Mara ya Pili, hivyo basi wanaepuka utaratibu wa sheria kuingia katika mwenendo wao wa Kikristo na kusababisha dhambi zao kuwa nyingi (Warumi 5:20.) Kwa kugongomelea sheria kimakosa Msalabani, wanaiondoa njia ambayo Mungu hutumia kuonyesha dhambi zetu ili tuweze kuzileta kwa Kristo.

Hukumu kabla ya marejeo ni muhimu ili kufichua ibada yetu ya kuhukumu inayotegemea wakati. Hukumu hii ni kioo katika nafsi zetu potofu. Lakini

pale dhambi hii inapoongezeka, neema ya ajabu ya Mungu inazidi kuwa nyingi zaidi!

Biblia kwa hakika inatuambia kwamba matokeo ya hukumu ni mwisho wa Chronos.

> Na akaapa kwa yeye aliye hai hata milele na milele, aliyeziumba mbingu na vitu vilivyomo, na nchi, na vitu vilivyomo, na bahari, na vitu vilivyomo, **ya kwamba hapatakuwa na wakati** [Chronos] **baada ya haya:** — Ufunuo 10:6 (KJV)

Hukumu ya Upelelezi ni chanjo ya kiroho inayoakisi virusi vya hukumu iliyojikita katika wakati na hukumu ndani yetu. Katika nuru ya ukweli wa Kristo, ambaye hahukumu, chanjo hii inafanya kazi ya ajabu ili kutuweka huru kutokana na hukumu iliyojikita juu ya wakati. Ndiyo maana katika mchakato wa hukumu, watu wa Mungu wanaacha kuhangaikia Chronos. Wanaanza kuishi katika uzoefu wa umilele sasa kwa kuwa hawaogopi tena kifo.

Nikiwa mtoto niliogopa kifungu hiki cha Biblia.

> Akaniambia, 'Usiyatie muhuri maneno ya unabii wa kitabu hiki, kwa maana wakati huo umekaribia. Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa." — Ufunuo wa Yohana 22:10-11

Niliambiwa kuhusu wakati ambapo Mungu angechora mstari katika mchanga; wakati ambapo Mungu alisema vya kutosha na kwamba yeyote ambaye hakuwa tayari atahukumiwa. Ni kweli itafika wakati Mungu atasema wale walio wachafu waendelee kuwa wachafu, lakini hii sio kwa sababu Mungu ameishiwa na wakati na kuamua kuwahukumu wale ambao hawakumsikiliza.

Mungu amedhihirisha kupitia Mwanawe jinsi rehema inavyoweza kufungwa kwa taifa kama mfano wa wakati wa mwisho. Viongozi wa Kiyahudi walipomkataa Kristo na kukataa kabisa kumfungulia mioyo yao, alilia kwa machozi juu ya Yerusalemu. Hatimaye, Yesu alilia na kusema "nyumba yenu

mmeachiwa ninyi hali ya ukiwa" (Mathayo 23:38). Rehema haijafungwa na Mungu; imefungwa na mwanadamu na Mungu analazimika kuikubali kwa sababu anaheshimu uchaguzi wetu.

Biblia inatuambia kwamba rehema za Mungu ni za milele (Zaburi 100:5; 107:1; 136:1; Ezra 3:11; Yeremia 33:11). Muda wote Yeye yuko tayari kutuhudumia. Lakini mwanadamu anaweza kukomesha rehema za Mungu kwa kukataa kuzikubali. Katika matukio ya mwisho ya historia ya dunia hii dunia itapokea ujumbe wa tabia ya upendo usio na kikomo ya Mungu ya kutofanya uharibifu katika muktadha wa Biblia. Ulimwengu mzima utaona tabia hii ikionyeshwa kwa watu wa Mungu na kuangazwa na utukufu wake.

> Baada ya hayo naliona malaika mwingine, akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu; na nchi ikaangazwa kwa utukufu wake. — Ufunuo wa Yohana 18:1

Kila mtu atajiunga na watu wa Mungu au atawakataa na kutafuta kuwaangamiza. Kwa hivyo, ulimwengu wote utafanya uamuzi wao na mlango wa Rehema utafungwa kwa wanadamu.

Kuna wengi leo ambao wanatafuta kutabiri wakati ujao kwa kutumia chati za nyakati na unabii wenye vipindi vya wakati ambapo Mungu atakomesha muda wa matazamio kwa wanadamu. Mambo haya yote ni heshima kwa Chronos na yanaonyesha hadithi ya Santa ambayo ni bora ujihadhari!

Shinikizo la wakati linalotumika kwa watu walio na tishio la kifo halitazalisha watu ambao wametiwa muhuri wa tabia ya Mungu. Watu wanahitaji kuja katika uzoefu wa umilele na kuruhusu Chronos kuacha kutawala maisha yao.

> Katika hili pendo limekamilishwa kwetu, ili tuwe na ujasiri katika siku ya hukumu; kwa kuwa, kama yeye alivyo, ndivyo tulivyo na sisi ulimwenguni humu. Katika pendo hamna hofu; lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu, kwa maana hofu ina adhabu; na mwenye hofu hakukamilishwa katika pendo. — 1 Yohana 4:17-18 (KJV)

Hebu tuache ibada ya sanamu ya Chronos; tuivue miungu inayodai kwamba uungu unaweza tu kuhusishwa na viumbe vinavyopita jaribio la

Chronos-Aeon. Yehova na Mwanawe hawana deni kwa Chronos kuthibitisha uungu wao kwetu. Tunarudia:

> Katika tumaini la uzima wa milele, ambao Mungu, asiyeweza kusema uongo, aliahidi kabla ya Aeon(ios), Chronos. — Tito 1:2

Iwapo ni lazima kuthibitisha uungu wa Mwana wa Mungu, na tufanye hivyo kwa tabia kamilifu ya upendo aliyoidhihirisha kama mwanadamu. Hicho ndicho ambacho Mungu ametupa ili tujifunze, si kile ambacho ni olam - wakati upitao akili au usioonekana; juu ya upeo wa macho.

> Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli. — Yohana 1:14

Je! ilikuwa ni asili ya milele ya Kristo ambayo Alitaka wanafunzi Wake wajifunze alipokuwa pamoja nao kwa miaka 3 na nusu? Hapana, alitaka wajifunze tabia yake tukufu ya upendo wa agape ikifunua kwamba Mungu ni upendo na uzima; sio Chronos na kifo. Hapimwi kwa wakati; kitu alichokiumba. Hebu tuzingatie tabia ya Mungu na uhusiano anaoudumisha kwa Mwanawe, na tuache vipengele hivi visivyojulikana vya umilele hadi Baba yetu atakapotufunulia.

SURA YA 26

# Kutakasa na Kukamilisha Hekalu la Kiroho

Jiwe la msingi ambalo tumeliweka katika kitabu hiki lina baadhi ya vitu muhimu.

1. Mungu hamhukumu/hamshutumu mtu yeyote. Yohana 5:22
2. Kristo hamhukumu mtu yeyote. Yohana 8:15
3. Sheria ya Mungu ni ya kiroho na inahusika na mambo ya moyo. Ndani ya ufalme Wake, sheria ya Mungu si kanuni ya kisheria ambayo imelazimishwa kwao bali ni onyesho la tabia yake ambayo watoto Wake huiishi kwa furaha ndani yao kwa Roho Wake.
4. Kristo duniani ni ufunuo kamili wa tabia ya Mungu. Ufunuo huu huyaangaza Maandiko mengine yote juu ya tabia ya Mungu.
5. Hukumu ilianza katika familia ya kibinadamu kupitia Adamu, ambaye aliongozwa na roho ya Shetani Adamu alipomhukumu Mwana wa Mungu na Hawa kwa ajili ya dhambi yake ya kula tunda la mti wa ujuzi.
6. Haki ya Mungu inamaanisha kufanya lile lililo sahihi, na jambo linalofaa kwa Mungu ni kuwa mwenye fadhili, neema, rehema, na kuruhusu matokeo ya uchaguzi wa mtu mwenyewe kumrudia au kumwadhibu.
7. Njia ya Mungu ya kutuokoa imefunuliwa katika mfumo wa Hekalu. Kila hatua ya njia hufunua kwa mwanadamu mawazo yake mabaya. Mungu alifunua kwa wanadamu hamu yao ya dhabihu (haikuwa nia

ya Mungu) kwa kuamuru mfumo wa dhabihu; Anawaonyesha wanadamu asili yao ya kuhukumu na kushutumu kupitia mchakato wa hukumu.

8. Ujumbe wa Malaika wa Kwanza unaosema kwamba "saa ya hukumu yake imekuja" una maana kwamba sasa tunapaswa kuhukumu tabia ya Mungu; na kwa namna tunavyowazia na kuhukumu tabia yake, ndivyo tutakavyojihukumu wenyewe kwa ufahamu huo.
9. Mungu haweki kumbukumbu au orodha kwa kusudi la kuwahukumu wenye dhambi.
10. Kutokana na kisa cha mwanamke aliyekamatwa katika uzinzi, ni viongozi wa kanisa ambao walitaka mchakato wa hukumu. Mchakato wa hukumu unasababisha wa kwanza kuwa wa mwisho na wa mwisho kuwa wa kwanza, huku kila mtu akihukumu kesi yake mwenyewe.
11. Shetani ndiye mwendesha mashtaka katika hukumu. Mungu huchunguza historia za maisha yetu katika hukumu ili kututetea dhidi ya mashtaka ya Shetani.
12. Mtazamo wa Mungu juu ya wakati ni tofauti kabisa na wetu. Mungu hatumii wakati kama kifaa cha kulazimisha tabia njema kutoka kwa viumbe wake. Hukumu iliyojikita katika wakati imefunuliwa katika Maandiko ili kumwonyesha mwanadamu dhambi yake mwenyewe na kututia moyo kutubu.

Kutokana na hili jiwe la msingi la thamani linaloshughulikia hukumu tunaweza kumkaribia Mungu. Kama Maandiko yanavyotuambia:

> Nami nitawakaribia ninyi ili nihukumu; — Malaki 3:5 (KJV)

Kristo anapotukaribia kwa upendo kupitia mchakato wa hukumu, Yeye ndiye shahidi mwaminifu. Kristo anatuonyesha tatizo letu ni lipi, si kwa ajili ya kutuhukumu bali kutuponya.

Katika miaka yangu ya awali nikiwa Mkristo, nilitetemeka nilipofikiria hukumu. Wakati ambapo nilipata faraja kwa Yesu, nilijiuliza jinsi gani ningeweza kupita katika hukumu. Shinikizo la wakati lilokuwa juu yangu na wazo langu kwamba wakati fulani Mungu angedhihirisha roho ya laana kulinitia wasiwasi mkubwa.

Nilijaribu kutuliza woga wangu na, kama watu wengi wa kanisa, nilifikiria juu ya watu waovu wote ulimwenguni ambao walikuwa "wabaya zaidi" kuliko mimi. Watu wa kanisa wanahitaji watu katika ulimwengu kuwa waovu ili waweze kujisikia vizuri zaidi kuhusu wao wenyewe katika nuru ya Mungu ambaye huwahukumu na kuwaangamiza wenye dhambi ambao hawafanyi jambo sahihi ndani ya muda fulani. Katika mfumo huu wazo linatokea kwamba Mungu hakika hataua kila mtu, kwa hivyo ikiwa nitajihukumu bora kuliko kila mtu ninayemjua, ninapaswa kuishi na kufika mbinguni. Mtu katika mtazamo huu hawezi kamwe kupumzika na daima atawaona watu kama ushindani.

Ninaomba kwamba katika kitabu hiki umepata zana muhimu za kuona kwamba Mungu hajawahi kukuhukumu, hata mara moja, na kwamba Yeye hatawahi. Hili limekuwa wazo la uhuru kwangu binafsi. Imekuwa moja ya sehemu kubwa katika fumbo kwangu kuondoa hofu na kuruhusu ukweli wote kamili wa upendo wa Baba kuingia moyoni mwangu.

Katika nuru ya jiwe hili la msingi ambalo tumeliweka, tunaweza kuendelea kukamilisha hekalu la kiroho ambalo tunaalikwa kuwa sehemu yake.

> Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu. Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni. Katika yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana. — Waefeso 2:19-21

Kweli tunaweza kusema Patakatifu panaweza kutakaswa. Damu yote sasa inaweza kuondolewa kutoka Patakatifu pa Patakatifu, kwa maana Mungu hatavihitaji vitu hivi kwa ajili ya upatanisho. Lakini ni kweli kwamba alituonyesha mambo haya ili kufunua mioyo yetu yenye dhambi ili tuweze kutubu kwa kuwalaumu wengine na kutafuta mbuzi wa Azazeli ili kuondoa hatia yetu.

> Yeye ashindaye, nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu wangu, wala hatatoka humo tena kabisa, nami nitaandika juu yake jina la Mungu wangu, na jina la mji wa Mungu wangu, huo

> Yerusalemu mpya, ushukao kutoka mbinguni kwa Mungu wangu,
> na **jina langu mwenyewe, lile jipya**. — Ufunuo wa Yohana 3:12

Jina hili jipya ambalo Mungu atatupatia ni jina lisilo na hukumu na laana; jina la fadhili na rehema. Tunapomwona Baba yetu wa ajabu kupitia Mwanawe bila lawama yoyote katika mojawapo ya hao, na tugeuzwe na kufanana nao "Kama kwa Roho wa Bwana." Amina.